Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Tano – Tarehe 14 Novemba, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 54

**Tatizo la Maji katika Mji wa Namanyere**

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE (K.n.y. MHE. ALLY MOHAMED KEISSY)** aliuliza:-

Mji wa Namanyere ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi una wakazi zaidi ya 15,000, Hospitali ya Wilaya, Chuo cha Manesi, Shule za Msingi Sita, Sekondari Tatu na Kituo cha Afya, lakini una uhaba mkubwa wa maji hasa ifikapo mwezi Julai hadi Novemba.

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo hilo ili kuwaondolewa kero hiyo wananchi wa Mji wa Namanyere?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mji wa Namanyere wenye wakazi zaidi ya 19,000 unapata maji chini ya asilimia 20 kutokana na ukosefu wa vyanzo vya maji vya uhakika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kufuatia agizo la Mheshimiwa Rais, alililotoa mwezi Oktoba, 2010 imefanya upembuzi yakinifu *(Feasibility study)* ili kubaini vyanzo vipya vya maji kwa ajili ya Mji wa Namanyere. Baada ya upembuzi yakinifu gharama zimekadiriwa kufikia bilioni 1.9.

Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi katika bajeti ya mwaka 2011/2012 iliomba maombi maalum ili kupata fedha hizo kwa lengo la kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa huduma za maji. Fedha hizi hazikupatikana. Aidha, Halmashauri kupitia programu ya maji na usafi wa mazingira imeidhinishiwa shilingi 600,000,000 kwa ajili ya miradi ya maji ya vijiji kumi (10).

Mheshimiwa Spika, mipango ya Halmashauri ya kukabiliana na matatizo ya maji yaliyopo ni pamoja na kuandaa rasimu ya sheria ndogo ya uvunaji wa maji ya mvua ambayo mpaka sasa iko katika mchakato wa kukamilika, kuwekwa kwa sharti la kuhakikisha kila mchoro wa nyumba unakuwa na mfumo wa uvunaji wa maji ya mvua ili upitishwe na mamlaka zinazohusika na kufanya tathimini ya kutumia nishati ya umeme wa jua kwa ajili ya kuendesha pampu za maji. Wananchi wa Mji wa Namanyere kwa sasa wanapata maji kutoka katika visima vinne vilivyochimbwa pamoja na bwawa la Msiri ambavyo ni vyanzo vinavyotumia pampu zinazohitaji nishati ya umeme. Halmashauri imenunua *generator* ili kuvuta maji kutoka katika visima hivyo kwenda wa wananchi.

**MHE. ALLY MOHAMED KEISSY:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mji wa Namanyere ni Mji unaokua siku hadi siku na wananchi wanapata tabu hata ya kujenga nyumba, maji ya kunywa na kila kitu hivyo visima vinne havitoshi kabisa na huwa vinaharibika mara kwa mara pampu zake. Watu wa Namanyere wanapata shida siku hadi siku yaani hata maji ya kunawa hakuna na hizo alizosema shilingi milioni 600,000,000 walizotenga zimeshindwa kukidhi. Wamechimba visima kule maji hakuna na hizo fedha hazijatumika hata senti tano. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kusaidia wakazi wa Namanyere? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy, kama ifuatavyo:-

Kwanza nakubali kweli Mji wa Namanyere kutokana na ongezeko la watu mahitaji ya maji hayatoshi. Kitu kinachofanyika sasa hivi tumekasimu madaraka kwa Mamlaka ya Sumbawanga kufanya stadi tuweze kuona mahitaji, kuainisha vyanzo mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya Mji wa Namanyere na miji mingine kama Laila kwa miaka 20 ijayo kazi hiyo imeshaanza kuainishwa *term of reference* na tutaiingiza katika *program* ya maji awamu ya pili.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la Namanyere karibu linalingana na Mji Mdogo wa Mbalizi ambao una watu karibu 60,000 naomba kuuliza ni lini Mji huo utapewa maji ya uhakika kwa sababu mpaka sasa hivi kuna matatizo makubwa sana? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanjale kama ifuatavyo:-

Kama nilivyojibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Keissy Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo yote tunaifanyia stadi ili tuweze kuainisha mahitaji ya maji kwa miaka 20 ijayo ndio kazi ambayo tunaifanya sasa. *(Makofi)*

Na. 55

**Ujenzi wa Miundombinu ya Maji**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU** aliuliza:-

Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 jumla ya shilingi 534,865,999/= zilitengwa kwa ajili ya kujenga miundombinu ya maji Halmashauri ya Wilaya ya Singida likiwemo Jimbo la Singida Mashariki, lakini fedha hizo zimetengwa wakati Wilaya mpya ya Ikungi yenye majimbo mawili ya Singida Mashariki na Singida Magharibi na Halmashauri havijaanzishwa rasmi:-

(a) Je, kati ya fedha hizo ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya Wilaya mpya ya Ikungi hasa Jimbo la Singida Mashariki kwa kusudi hilo?

(b)Je, ni Vijiji na Kata zipi za Jimbo la Singida Mashariki zitanufaika na ujenzi wa miundombinu ya maji iliyotengewa fedha hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Singida katika mwaka 2010/2011 ilitengewa shilingi 664,470,000 kupitia programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini kwa ajili ya

miradi ya maji katika vijiji 10. Kati ya fedha hizo kiasi kilichopokelewa ni shilinig 532,451,429 na zilizotumika ni shilingi 379,264,336.

Fedha hizi zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida na hakukuwa na bajeti kwa ajili ya Wilaya mpya ya Ikungi na Jimbo jipya la Singida Mashariki ambayo ilikuwa haijaanzishwa wakati huo. Wilaya mpya ikiwemo ya Ikungi zitaanza baada ya kukamilika kwa hatua za mwisho za utoaji maoni, mapendekezo na pingamizi kama zipo kufuatia notisi ya kuanzisha Mikoa na Wilaya iliyotolewa tarehe 9/9/2011.

Aidha, Bajeti ya Halmashauri inayoandaliwa huzingatia vipaumbele vya miradi iliyopangwa kutekelezwa bila kujali iko katika Jimbo lipi la uchaguzi.

(b) Mheshimiwa Spika, vijiji na Kata za Jimbo la Singida Mashariki zilizopata mgao wa bajeti hiyo kwa ajili ya miradi ya maji kwa mwaka 2010/2011 ni Kijiji cha Siuyu kilichopo katika Kata ya Siuyu na Kijiji cha Nkuhi kilichoko katika Kata ya Issuna. Kiasi cha fedha kilichotumika kwa ajili ya miradi katika Vijiji hivyo ni shilingi 84,503,200.

Kati ya fedha hizo shilingi 33,484,000 zilitumika kwa ajili ya uchimbaji wa kisima kimoja (1) katika Kijiji cha Siuyu, utafiti wa maji ardhini, upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi na shilingi 51,019,200 zilitumika kwa ajili ya uchimbaji wa visima vitatu katika Kijiji cha Nkuhi, utafiti wa maji ardhini, upembezi yakinifu na usanifu wa mradi.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la nyongeza naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aliambie Bunge lako Tukufu kama ana taarifa kwamba shilingi milioni 51,000,000 zinazodaiwa kutumika Kijiji cha Nkuhi hazijatumika, hakuna maji na matokeo yake imebidi Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Singida Mashariki utoe shilingi milioni 4 ili kuwapatia wananchi wa Kijiji cha Nkuhi maji.

Kama atakubali kwamba fedha hazijatumika naomba alieleze Bunge Tukufu ni hatua gani zitakazochukuliwa na Serikali ili kushughulikia hawa ambao wanapelekewa fedha kwa ajili ya maji ya wananchi halafu anazielekeza kwingine? (*Makofi*)

**SPIKA:** Pamoja na kurudisha hela zako za jimbo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sina tatizo na anachosema Mheshimiwa Lissu, yeye kama amekwenda ametumia hela za *constituency development catalyst fund* kwa ajili ya shughuli za maji pale mimi sioni tatizo kabisa hela hizi zilikusudiwa kuchochea maendeleo ya wananchi pale walipo.

Kwa hiyo, kama ametumia Mbunge ameonyesha tu busara yake kwamba mimi nafikiria ni *priority area* kuna tatizo akapeleka pale *there is no problem.* Anachokizungumza hapa anatuambia kwamba milioni 51,000,000 ana hakika kwamba hazikuelekezwa kule zilizokwenda. Na mimi nilipokuja hapa wala sijaja hapa kwamba nakuja hivi hapa nasikia usingizi kwa sababu ya kujiandaa kwa ajili ya kujibu swali hili. *De-central contradiction* iliyoko katika vijiji hivi anavyozungumza Mheshimiwa Tundu Lissu ni kwamba visima vimekwenda vimechimbwa lakini watu hawajaanza kupata maji. Kwa maana ya kwamba hawajapeleka katika simtanki na kuanza kusambaza na kupeleka.

Wanacho kigezo walichokitumia hapa. Kuna kitu kinachoitwa *counter part fund* wakasema wale wananchi ambao wamejitoa wakatoa michango na wale ambao wamefanya kazi kwa mikono yao wanawapa kipaumbele namba moja.

Asilimia inayotumika pale ni asilimia 5. asilimia 2.5 wananchi na 2.5 kutoka kwenye Halmashauri. Wakaenda wakachukua vijiji vyote pale Singida wakaviorodhesha. Hiki kijiji kinachosemwa ninacho hapa ninacho na Mheshimiwa Lissu akitaka tutakaa tutazungumza vizuri.

Wakasema hivi tunatoa kipaumbele kwa vile vijiji ambavyo vilionyesha nia ya kuchangia mpango huu. Vijiji hivi anavyovitaja hapa havikukidhi hiyo haja vikasukumwa mbele kwa ajili ya *program* inayokuja.

Sasa mimi nataka niseme maneno yafuatayo: Ametaka kujua kwamba ni hatua gani zinazochukua? Mimi hapa nikimaliza natoka nje nazungumza na Mkurugenzi namwambia hivi taarifa mliyonipa Mbunge amekataa anasema kwamba milioni 51,000,000 hazikutumika hatuwezi tukakaa hapa ndani tukaambiwa milioni 51,000,000 hazikutumika, nitamwomba Waziri Mkuu aniruhusu kwenye Kikao hiki niondoke niende Singida nikacheki hizo milioni 51,000,000 halafu mimi nitachukua hatua pale pale. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu wa Serikali kutekeleza miradi ya Maendeleo hutumia mpango shirikishi kwa maana wananchi kukusanya nguvu zao na Serikali inawaunga mkono. Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Singida Vijijini, ina majimbo matatu na kati ya majimbo hayo wako wana siasa ambao wamewahamasisha wananchi wao kutokuchangia miradi ya maendeleo ambayo inasababisha hata Serikali isitoe fedha zake.

Je, Serikali ina mpango gani kwenda kukemea suala hili na kuwaelimisha wananchi kukumbuka dhana ya Serikali ili waweze kuwaelimisha wananchi kukumbuka dhana ya Serikali ili waweze kufaidi Serikali yao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, mimi nadhani Mheshimiwa Diana Chilolo, anatutendea haki sana katika Bunge hili. Anachozungumza hapa anazungumza namna ambavyo unaweza ukashirikisha wadau mbalimbali katika kuleta maendeleo katika eneo husika. Hakuniambia hapa kwamba ni nani hao lakini wao watakuwa wanasikia haya yanayosemwa. Nchi hii ina misingi yake, nchi hii imefika hapa ilipofika wakati ilipokwenda ikahusisha pia nguvu za wananchi zikachanganywa na Serikali na zile za Halmashauri ndipo tukapiga hatua tuliyopiga sasa.

Sasa kama kuna watu wanapitapita huko wanawaambia wananchi kwamba wasishiriki katika mipango ya maendeleo mimi nataka niseme hapa Mheshimiwa Mkuchika aliondoka hapa alikwenda Singida na akazungumza na wananchi kule akawaeleza umuhimu wa wananchi kuchangia katika miradi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiondoa habari ya wananchi kushiriki katika mipango hii ukumbuke kwamba asilimia 40 ya Bajeti ya nchi yetu inatoka nje. Maana yake pampu iko nje asilimia 60 ndizo ziko hapa. Itakuwa ni *gross contradiction* kuanza kuzungumza habari ya kuiendeleza Tanzania katika miradi yake bila kuhusisha wananchi. Shule za kata zilizojengwa katika nchi hii zimejengwa kwa misingi ya wananchi kuchangia shule hizi.

Barabara zetu tulizonazo wananchi wamechangia, zahanati na vituo vyote vimetokana na wananchi kushiriki kikamilifu kwa kupeleka nguvu zao na michango yao tukafika hapa tulipofika. Rai ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ni kwamba tuendelee kusisitiza jambo hili. Wale ambao wanafanya hivyo kupita kuwaambia wananchi wasishiriki hatutafiki huko wanafanya vibaya lazima tushirikiane wote kwa pamoja kuhakikisha kwamba tunapiga hatua kwenda mbele zaidi kwa kushirikisha nguvu za wananchi. Kwa hiyo, mimi nataka kusema kwamba hayo ndio maelezo yetu.

Na. 56

**Kujenga Nyumba kwa Ajili ya Kufikia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**MHE. JADDY SIMAI JADDY** aliuliza:-

Mara nyingi Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anapokuwa na ziara Tanzania Zanzibar hupangiwa kulala katika Hoteli ya Kempinski pale anapolazimika kulala Visiwani humo:-

Je, Serikali haioni haja ya kujenga nyumba maalum Tanzania Zanzibar kwa ajili ya kufikia Mheshimiwa Rais badala ya kufikia hotelini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mbunge wa Mkwajuni, kama ifuatavyo:-

Kimsingi, mahali rasmi pa kufikia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anapokuwa Tanzania, Zanzibar ni Ikulu ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa mfano katika safari ya Mheshimiwa Rais alipokwenda kuhudhuria msiba wa waathirika wa ajili ya *MV Spice Islander* kati ya tarehe 10 – 11 Septemba, 2011 Rais alilala katika Ikulu ya Zanzibar. Hata hivyo Rais hulazimika kufikia hotelini kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo mikutano katika hoteli husika.

Kutokana na kuwepo kwa utaratibu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufikia Ikulu ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Serikali haioni sababu za kujenga nyumba nyingine kwa ajili hiyo kwa wakati huu.

**MHE. JADDY SIMAI JADDY**: Mheshimiwa Spika, nimeridhika.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swali la sasa hivi linafanana kabisa na lile la Kaskazini Pemba na kwa kuwa lipo jengo la Jamhuri ya Muungano linalojulikana kwa jina kama Ikulu Ndogo ya Jamhuri ya Muungano, Kaskazini Pemba na kwa kuwa Serikali sasa hivi ya Jamhuri ya Muungano imeshalifanyia ukarabati mkubwa na yamebakia mambo madogo madogo hadi kukamilisha watumishi.

Je, Serikali inasemaje kulikamisha jengo hilo ili Rais atakapofanya ziara kule Kaskazini Pemba apate sehemu nzuri ya mapumziko?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maida Mohamed, kama ifuatavyo:-

Serikali itahakikisha kwamba jengo la Ikulu Pemba linakamilika haraka iwezekanavyo kuanzia katika mwaka huu wa fedha tuna fedha za kushughulikia jengo hilo.

Na. 57

**Somo la Hisabati**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** aliuliza:-

Wanafunzi wasioona hawafundishwi somo la hisabati kutokana na ulemavu wao. Lakini wanapotahiniwa ufaulu wao hushuka kutokana na kutofanya mtihani wa hisabati.

Je, ni lini utaratibu huo usio na haki utasitishwa?

**NAIBU WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa somo la hisabati katika ulimwengu wa taaluma, kazi na hata katika maisha ya kila siku ya raia wote wa Tanzania. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Wizara imelifanya somo la hisabati kuwa ni miongoni mwa somo ambalo kila mtahiniwa wa kidato cha nne hana budi kulifanya na kulifaulu. Asiyefaulu somo hili hupewa adhabu ya kiasi kwamba hata kama anafanya vizuri katika masomo mengine yote maana yake hawezi kupata cheti cha daraja la I wala la II.

Mheshimiwa Spika, somo la hisabati kwa wanafunzi wasioona linafundishwa katika shule za msingi tu. Sababu ya kufundishwa katika shule hizo ni kuwepo kwa vitabu vilivyoandikwa kwa nuktanundu *(Braille)* na kuwepo kwa walimu wataalamu wanaoweza kufunisha somo hilo.

Aidha, wanafunzi wasioona katika shule za sekondari hawafundishwi somo hilo. Hii ni kutokana na kuwa mada, maudhui na alama katika vitabu vya hisabati havijaandaliwa kwa mfumo wa nukta nundu. Vile vile, hakuna walimu wenye taaluma ya kufundisha kwa kutumia nukta nundu kwa shule za sekondar.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kutofundishwa kwa somo hilo kwa wanafunzi wa shule za sekondari kwa wasioona kulisababisha ufaulu wao kushuka na hivyo kishusha daraja la ufaulu la ufaulu katika matokeo ya mtihani wa kidato cha nne. Hata hivyo, ninayo furaha kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kuanzia mwaka 2009 watahiniwa wasioona wenye ufaulu wa kuwawezesha kupata daraja la I na la II walitunikiwa daraja hilo ijapokuwa walikuwa hawafanyi mtihani wa somo la hisabati kama kanuni inavyoelekeza. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kupitia Baraza la Mitihani walisitisha utaratibu huo ambao ulikuwa hawatendei haki wanafunzi wasioona.

Ili kukabiliana na changamoto hiyo, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba Wizara yangu kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa yanayotoa huduma za kielimu kwa wasioona, sasa itaanza kufanya maandalizi muhimu yatakayowezesha shule za sekondari zenye wanafunzi wasioona kumudu kufundisha somo la hisabati. Mipango mbalimabli imeandaliwa, kwa mfano shirika la *International Council of Education for Visual Impaired (ICEVI)* limetoa kitabu kinachotoa mwongozo juu ya namna bora ya kufundisha somo hili kwa shirika hilo. Ifikapo mwaka 2012, maandalizi yote yatakuwa yamekamilika. Walimu 20 kutoka katika shule za sekondari zenye wanafunzi wasioona somo la hisabati watapatiwa mafunzo ya muda mfupi jinsi ya kufunsisha somo hilo kwa kutumia nuktanundu. Baada ya kukamilika kwa mafunzo hayo, inatarajiwa kuwa wanafunzi wa shule za sekondari wataanza kufundishwa somo la hisabati ifikapo mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeandaa mpango endelevu ili kuwezesha chuo chetu cha ellimu maalum cha Patandi, na Chuo Kikuu cha Dodoma viweze kuandaa walimu wa hisabati katika ngazi ya Stashahada na Shahada ili wanafunzi wasioona wa shule za sekondari waweze kufundishwa na kufanya mitihani ya hisabati kama wanafunzi wengine.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu marefu tu na mazuri kiasi kutoka Serikalini. Niombe tu kuuliza hivi changamoto hii 2009 tu ndiyo mmegundua kwamba hawa watoto kwa muda wote walikuwa wanaonewa na kukoseshwa haki yao ya kufundishwa hiyo hesabu? *(Makofi)*

Pili, baada ya maelezo kwamba itakapofika na 2013 sijui ndiyo wataanza kufundishwa, je, Serikali sasa ina mkakati gani wa kuwawezesha watoto hawa kuweza kufundishwa masomo ya sayansi mengine kama Kemia na vitendo vyake, Bailojia na vitendo vyake, Fizikia na vitendo vyake. Kwa sababu nchi za wenzetu wanafundishwa, sasa sisi hii changamoto tutaitatua lini kwa sababu na hayo kwa wale wanaoweza wanapaswa kufundishwa? Naomba jibu. *(Makofi)*

**NAIBU WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia walemavu kwa nchi nzima. Mheshimiwa Mbunge huyu anafuatilia sana.

Lakini majibu tu ni kwamba nyuma huko kabla ya mwaka 2009 ni kweli Baraza la Mitihani lilikuwa haliwatunuku daraja la I na la II kwa vijana hawa kwa sababu walikuwa wanakosa somo hilo? Lakini hiyo ilitokana na kwamba Serikali ilikuwa haijajiandaa bado kuwa na vitabu, ilikuwa imeandaa vitabu vyenye nuktanundu kwenye shule za msingi lakini kwa shule za sekondari kulikuwa hakuna maandalizi hayo.

Lakini vile vile tulikuwa tumekosa walimu wa kuweza kufundisha somo hilo kwa kutumia hiyo nuktanundu. Sasa basi tumeamua kwa pamoja kwamba tumeliona hilo kwamba lilikuwa ni tatizo na mwaka kesho kama nilivyosema au mwaka keshokutwa tayari wataalam watakuwa

wameshaandaliwa katika vyuo vyetu vya Dodoma na Patandi tayari na vitabu vitakuwa vimeshaandaliwa ili watoto waweze kusoma somo hilo.

Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati Serikali imeshaliona tatizo na imeanza kutatua.

Kuhusu somo la *biology, chemistry* na *physics* kama *practical* kwa wanafunzi wasioona. Serikali lazima iseme wazi kwamba kama hawa wanafunzi hawaoni na hivi hata Sheria zile wote tumesoma sayansi, *Form I, Form II* ukiingia tu *Form I* unaambiwa sheria za maabara kwamba ukimpeleka mtu ambaye hawezi kuona mle maabara anaweza akagusa *chemicals* tena akaendelea kuharibu macho zaidi.

Kwa hiyo tuendelee kuwa na ufikirio mwingine ambapo tunawe tukawafanya watoto hawa wakapata haya masomo. Lakini kwa sasa Serikali bado haina mpango wa kuwaingiza watoto maabara ambao hawawezi kuona wasije tena wakaharibiwa zaidi. *(Makofi)*

Na. 58

**Ongezeko Kubwa la Ada kwa Shule Binafsi**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Kuna ongezeko kubwa la ada katika shule za binafsI:-

(a) Je, kwa nini Serikali isiingilie kati suala hili na kuweka viwango elekezi vya ada ili kusiwe na mkanganyiko wa kielimu?

(b) Je, Serikali haioni kuwa hali hiyo inajenga matabaka ya wenye uwezo na wasio na uwezo katika jamii?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna ongezeko kubwa sana la ada katika shule za binafsi. Hali hii imechangiwa na kupanda kwa gharama za uendeshaji pamoja na utashi wa baadhi ya wazazi kupenda kuwapeleka watoto wao kwenye shule ambazo zinatoza ada kubwa. Hata hivyo, nia ya Serikali ni kuweka usawa wa kupata elimu kwa walio nao na wasio na uwezo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Waraka Na. 19 wa mwaka 2002, ilipanga viwango vya ada kwa shule zote nchini zikiwemo shule za binafsi. Hata hivyo, kutokana na gharama za kusomesha mwanafunzi mmoja kwa mwaka au ile *(Unit Cost)* kuongezeka na kila shule kupanga viwango kwa utashi wake.

Serikali imeliona hilo, imeona umuhimu wa kutoa waraka mwingine kuhusu viwango vya ada za shule za Serikali na shule binafsi vitakavyoendana na gharama halisi za uendeshaji wa shule kwa wakati sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hayo, Wizara yangu imeandaa rasimu ya maoni toka kwa wadau mbalimbali wa elimu ili wapitie na kuamua kwa pamoja juu ya viwango vya ada kwa shule zote za serikali na za binafsi kwa nchi nzima. Aidha, Wizara yangu, itahakikisha kuwa viwango vya ada vitakavyotolewa vitazingatia gharama halisi *(Unit cost)* ya kila mwanafunzi na kuweka uwiano katika ulipaji na utoaji wa ada hiyo.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Pamoja na majibu mazuri yenye ufasaha ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mengine mawili ya nyongeza. La kwanza, je, ni lini sasa Serikali itatoa

waraka huu mapema ukizingatia kwamba tupo katika kipindi cha mwisho wa mwaka na Januari mwaka 2012 muhula mpya utaanza?

Swali la pili, je waraka Na. 19 uliotoka mwaka 2002 ulipanga viwango vya ada. Je unasemaje juu ya ada kwa sekondari kwa shule binafsi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu ni lini rasimu hiyo au waraka huo utatoka, ni kwamba tayari iko katika mchakato wa kufanya hivyo na kwa kutambua kwamba tuko mwisho wa mwaka nakuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba kabla ya mwezi Desemba haujaisha tayari waraka huo utakuwa umeshatoka unaoelekeza na kutoa mipangilio yakinifu ya namna ya ada kwa shule za binafsi zitakazotoza. Ni pamoja na shule za Serikali. Kwa sababu kidogo toka sasa ni miaka kumi waraka ulipotolewa mwaka 2002 uliokuwa ukielekeza viwango vya ada ambavyo sasa hivi viko chini sana.

Lakini vile vile umeuliza mwaka 2002 huo waraka namba 19 ulikuwa unasemaje. Kwa niaba ya Waziri kwa Watanzania wote ni kwamba mpaka sasa tuna waraka huo unaosema kwamba shule binafsi kwa *boarding* ada yake ni laki tatu na themanini.

Jambo ambalo tayari wadau wengi wa elimu wamelilalamikia sana na ada kwa *Form I* mpaka *Form VI* shule za *day* ni laki moja na nusu huo ndiyo waraka unaotumika mpaka sasa. Ndiyo maana umeona sasa shule binafsi wameanza kuchaji wanavyoona wao na Serikali tumeingilia tuweze kuunda waraka utakaopeleka kuwaelekeza hao watu wa *TAMOSCO* na wamiliki wa shule binafsi.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza dogo. Kwa kuwa kumekuwa na mtindo wa kujenga shule binafsi hapa nchini na kuwaingizia wazazi hasara kubwa na shule hizi zimekuwa hazijasajiliwa. Mnakuwa hawa watu mkiwakamata mnawachukulia hatua gani?

**SPIKA:** Msabaha ukiuliza maswali ambayo siyo yale yale ya mwanzo basi tatizo. Haya Mheshimiwa Naibu Waziri najua unafahamu hilo kwa sababu ulishughulikia hivi karibuni.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba lazima tutambue kwamba Sera ya Elimu ya mwaka 1995 inaweka wigo mzuri na uwigo mpana na ruksa kwamba mwananchi yoyote Mtanzania, Mashirika ya dini na Mashirika mengine au *NGOs* kama ziko tayari kuwekeza katika elimu kuweza kuwasaidia wanafunzi hasa kwenye masomo ya Sekondari, tumesema ni ruksa ili mradi wafuate sheria zilizowekwa pale na kanuni kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Sasa kinachoonekana mpaka sasa kwamba wamiliki hawa au wale wadau wanaotaka kuanzisha shule hizi za binafsi wanajianzishia kiholela maeneo ambayo hayana kiwango na hakuna mawasiliano na Ofisi ya Kamishna wa Wizara ya Elimu na Ofisi za Ukaguzi Kanda.

Mheshimiwa Spika, nadhani utaona kwamba mimi mwenyewe nimechukua jukumu hilo la kutembelea baadhi ya shule kwa ziara za kushitukiza. Nikiona kuna shule ambayo haina viwango, haijasajiliwa na inaendesha masomo mengine hata kwa mfumo usio rasmi na shule zingine tumezifungia zinaendesha masomo hata kwa lugha zingine za Kikongo huko. *(Kicheko)*

Hakuna mawasiliano kabisa na Serikali ya Tanzania. Hii hatuwezi kuipeleka elimu tunakoweza kwenda. Kwa hiyo, tumeamua angalau kusitisha waweze kufuata utaratibu wa kusajili shule. Kwa hiyo, mimi natoa wito kwa wadau wote wanaotaka kuanzisha shule za binafsi kwamba wafuate sheria. Ukaguzi Kanda wana sheria zote, wana utaratibu wote wa namna ya kuanzisha hizi shule za *private.*

Na. 59

**Kuungua moto kwa kituo cha Polisi Mkokotoni**

**MHE. JUMA OTHMAN ALI** aliuliza:-

Hivi karibuni kituo cha Polisi Mkokotoni kiliungua moto na kusababisha maafa makubwa kwa mali na vifaa vya walinzi wetu:-

(a) Je, kuna uchunguzi uliofanyika ili kujua hasara iliyopatikana kimaafa na kifedha?

(b) Je, nini matokeo ya uchunguzi huo?

(c) Je, ukarabati wa kituo hicho utaanza lini ili kuinusuru hali mbaya ya kituo hicho iliyopo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali na Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mbunge wa Tumbatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baada ya kuungua kwa jengo hilo uchunguzi ulifanyika na hasara iliyopatikana ni pamoja na jengo lenyewe kuteketea kabisa, samani, silaha, vielezo mbalimbali, majalada ya kesi, pamoja na nyaraka nyingine. Hasara iliyotokea jumla yake ni milioni 60.

(b) Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchunguzi yamebainisha kwamba moto huo ulisababishwa na hitilafu ya umeme iliyotokea kwenye paa eneo la iliyokuwa Ofisi ya Mkuu wa Kituo.

(c)Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli kwamba jengo hilo liliteketea kabisa Serikali ipo katika hatua ya kumpata Mkandarasi ili ujenzi wa jengo hili uanze mara moja.

**MHE. JUMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Spika, nimeridhika na majibu hayo.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kuniona. Tarafa ya Ndagalu katika jimbo la Magu ina kituo kimoja cha Polisi ambacho kiliungua moto kama ambavyo ilivyotokea toka kwenye swali la Mheshimiwa Mbunge alilouliza. Halmashauri ya Wilaya ya Magu imetenga kiasi cha fedha na wananchi wamechangia.

Je, Serikali Kuu iko tayari kuchangia ili kituo hiki kiweze kuanza kufanya kazi kwa sababu kinahudumia tarafa nzima yenye Kata nne?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, taarifa kweli tunazo kuhusu uunguaji wa kituo hicho cha Mangu na niseme kwamba sisi tumekuwa tunavutiwa sana kwa jitihada ambazo wewe umekuwa unazifanya lakini pia Halmashauri imekuwa inafanya katika kuhamasisha wananchi katika ujenzi wa kituo hicho. Nitake kumhakikishia kwamba tutaelekeza watu wetu kule uongozi wa Polisi kuona ni mchango gani wanaweza wakafanya. Lakini niseme kwamba tunakupongeza katika hatua hizo ambazo unachukua katika ujenzi wa Kituo. *(Makofi)*

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Pamoja na kwamba hivi vituo vingine vimeungua, lakini swali langu liko sawasawa tu kwamba na kituo chetu cha Kyaka cha Polisi ni kituo kipya ambacho mpaka sasa hivi hakina choo, hakina maji, na wananchi wapo pale maisha yao ni magumu sana hata watu wakiwekwa mahabusu wanatumia hali fulani ambayo hata kutamka siwezi kutamka. Nauliza Mheshimiwa Spika, Waziri ana mpango gani na kituo cha Kyaka kwa sasa hivi cha Polisi?

**SPIKA:** Wenzako viliungua sasa wewe kituo chote, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, hizi taarifa kusema kweli tulikuwa hatuna. Lakini maadhali tumezipata tutazifanyia kazi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hata mimi inanihusu kwa sababu anazozielewa yeye mwenyewe.

**SPIKA:** Ahsante. Sisi hatuzielewi. *(Kicheko)*

Na. 60

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi na Nyumba za Polisi Mangaka**

**MHE. JUMA A. NJWAYO (K.n.y. DUNSTAN D. MKAPA)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi na nyumba za Polisi Mangaka ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Nanyumbu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa kujenga vituo vya Polisi vyenye hadhi ya daraja "A" kwenye Makao Makuu ya Wilaya zote nchini. Mpango huo unatekelezwa kwa awamu. Ujenzi wa Kituo cha Polisi Mangaka, pamoja na nyumba za askari umezingatiwa katika mpango endelevu na wa muda mrefu wa kukabiliana na tatizo hili kubwa katika jeshi letu la polisi.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini itambulike kuwa Wilaya hii ya Nanyumbu ni miongoni mwa Wilaya mpya na ambazo zina matatizo makubwa ya nyumba na makazi ya wafanyakazi.

Je, Wizara yake iko tayari kutoa kipaumbele maalum kwa Wilaya hii?

Pili, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba katika Bajeti iliyopita ilitenga milioni 10 na ilitoa eneo la kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya *OCD* kwenye Wilaya ya Tandahimba.

Je, sasa Wizara inaweza kwenye Bajeti ijayo itafanya kila linalowezekana kuhakikisha inamalizia ujenzi wa eneo lingine la jengo hilo lililobakia haraka iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mara kadhaa ninapokuja hapa masuala kama haya yanajitokeza na ni jitihada tunazifanya; mimi nina uchungu kama yeye na kama Wabunge wengine. Mimi nikiwa kama Mbunge mwenzenu, tatizo kubwa tulilonalo maana hili ni tatizo la Kitaifa, nyumba za askari, ujenzi wa vituo, vitendea kazi, na kadhalika. Tatizo kubwa ambalo tumekuwa nalo ni tatizo la rasilimali fedha. Ndio maana tumefanya mpango, tunakwenda awamu kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, zipo Wilaya kadhaa hii ikiwa ni mojawapo katika Wilaya Mpya ambazo zimekuwepo nikisema pia na Mikoa Mipya ambayo imewekwa na yote inataka itizamwe, yote inataka iwekewe *facilities* kama hizi.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, asiwe na wasiwasi jitihada zitafanyika na mimi na yeye kama tunavyozungumza, tutakwenda hatua kwa hatua kuona ni maeneo gani tunaweza tukaanza nayo lakini umuhimu wa jambo hili tunauzingatia.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ashante sana kwa kunipa nafasi ya swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, katika Bajeti ya 2008/2009 Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Polisi Wilaya ya Namtumbo. Lakini mpaka leo hakijaanza kujengwa.

Mheshimiwa Spika, je, ni nini kinachozuia kuanza kwa ujenzi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema Waheshimiwa Wabunge, mimi nina uchungu kama ninyi katika maombi na katika matashi ya kuwa na Vituo vya Polisi, kama mnavyosema hapa. Lakini niseme tatizo kubwa ambalo tumekuwa nalo na ni tatizo ambalo mnalielewa, ni hali nzima ya kuwa na rasilimali fedha ya kuweza kutengeneza maeneo ambayo tunatengeneza. Ni kweli wakati mwingine katika Bajeti tunakuwa tumeweka maazimio kwamba, maeneo fulani tutayafanyia kazi, likiwemo hili eneo la Namtumbo, lakini pia katika utekelezaji wa Bajeti huwa kuna mambo mengine ambayo yanajitokeza na inakuwa ni bahati mbaya kwamba, rasilimali fedha hiyo, inabidi igawanywe hapa na pale.

Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hili bado tunalo na nimwambie kwamba, tutalifanyia kazi na hata katika Bajeti hii ya sasa tunafanya kila jitihada kuona kwamba, uanzishaji wa kutengeneza kituo hiki cha Namtumbo, unafanyika.

Na. 61

**Mlima Kilimanjaro Kutangazwa Kwa Bidii Kiutalii**

**MHE. ALI JUMA HAJI** aliuliza:-

Mlima Kilimanjaro ni wa Tanzania, lakini wageni wengi wanaokuja kuuona mlima huo, hupitia Kenya kwa sababu Kenya wanautangaza kwa nguvu kuwa uko nchini mwao:-

(a)Je, Serikali ina mpango gani wa kukanusha au kukubali kuwa mlima huo ni mali ya Tanzania au Kenya?

(b)Je, Serikali imejipanga vipi katika kutangaza Mlima Kilimanjaro kuwa upo Tanzania na kuwafanya wageni wapitie Tanzania moja kwa moja badala ya kupitia Kenya?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mbunge wa Chaani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi huru na inaeleweka kwa mipaka yake iliyowekwa kwa mujibu wa sheria. Mipaka ya Tanzania inaeleza wazi kuwa Mlima Kilimanjaro uko nchini Tanzania. *(Makofi)*

Kenya, haijawahi kutangaza kuwa mlima Kilimanjaro uko nchini kwao, bali kwa kipindi kirefu wamekuwa wakitangaza kuwa ukiwa Kenya, utauona vizuri Mlima Kilimanjaro. Aidha, kuna tofauti kati ya kupanda mlima na kuona mlima.

Mlima Kilimanjaro una njia kuu 6 ambazo ni Marangu, Rongai, Mweka, Machame, Londrosi na Umbwe, ambazo ziko Tanzania hivyo, ili kuweza kupanda Mlima Kilimanjaro ni lazima Mtalii afike Tanzania ndipo aweze kuupanda. Hivyo, inaeleweka wazi kuwa Mlima huo uko Tanzania na wanaoupanda wanapanda kwa kuingia Tanzania.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Utalii Tanzania imekuwa ikitangaza vivutio vya utalii ukiwemo Mlima Kilimanjaro kwa kutumia njia mbalimbali zinazothibitisha kuwa Mlima huo uko Tanzania.

Kwa mfano, kumekuwepo mabango ya vivutio vya utalii vya Tanzania yaliyowekwa kwenye mabasi Jijini London, miaka michache iliyopita, tovuti ya *TTB* imekuwa ikieleza vivutio vya

Tanzania ukiwemo Mlima Kilimanjaro, kumekuwepo na utaratibu wa kuleta nchini waandishi wa habari na watu mashuhuri, kuweka vipeperushi na majarida mbalimbali kwenye ndege *(inflight magazines)*, kuweka matangazo katika ligi kuu ya mpira wa miguu nchi za nje. Mfano ligi kuu ya Uingereza pamoja na njia nyingine mbalimbali ikiwemo kushiriki kwenye maonesho ya utalii.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Bodi ya Utalii ilikuwa ikiratibu zoezi la kuupigia kura Mlima Kilimanjaro ili uingizwe kwenye maajabu saba mapya ya Dunia, mashindano yaliyokamilika hivi karibuni. Ni kampeni pia iliyokuwa ikilenga kuutangaza Mlima huu ambao ni kivutio cha utalii kilichoko Tanzania.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kumwuliza Mheshimiwa Waziri, maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, amekubali kwamba Wakenya wamekuwa wakitangaza kwamba ukiwa Kenya utauona vizuri Mlima huu wa Kilimanjaro. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba, bado Wakenya wanatumia ujanja huu wa kuwapitisha watalii kwao ili kupata mapato?

Mheshimiwa Spika, la pili. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba katika kuutangaza Mlima Kilimanjaro, kumekuwa na zoezi la kuupigia kura Mlima huu ili kuingia katika maajabu bora saba ya Dunia. Lakini kwa matokeo yaliyotoka hivi karibuni, Mlima huu hatukufanikiwa kuuingiza katika maajabu hayo saba.

Je, Mheshimiwa Waziri, anaweza kuwaeleza nini Watanzania, kwa nini hatukuingia? Au tupo katika mtindo uleule wa *Miss Tanzania?*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mlima huu uko Tanzania lakini pia ni kweli kwamba, mlima huu unaonekana ukiwa Kenya. Kwa maana hiyo, Kenya wamekuwa mbele sana kwenye utangazaji na hili sio kosa. Wamefanya kampeni kubwa na wamefanikiwa sana.

Lakini sababu nyingine ambayo imefanya Kenya ikawa ni lango kuu la kuingilia wageni kwa Afrika Mashariki ni kwa sababu ya hali ya mawasiliano, kwa maana ya mawasiliano ya anga. Shirika la ndege la Kenya ni *strong* na limeingia makubaliano na Mashirika mengine kama *KLM.* Kwa hiyo, wageni wanafika Kenya kwa urahisi zaidi. *Connection* ya kuja Tanzania, kiasi inakuwa ni ngumu na inafanya safari za kuja Tanzania, kidogo ziwe juu ukilinganisha na wenzetu wa Kenya.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara ambacho tunakifanya kwa sasa hivi ni kufanya kampeni kubwa zaidi. Jinsi watu watakavyojua kwamba, Mlima huu upo kwetu na baadhi ya vivutio vyetu na kupenda kuvitembelea, wataongezeka katika kuja wakati tukiendelea kuboresha mambo mengine ikiwemo kuimarisha shirika letu la ndege la Tanzania *(ATCL).*

Mheshimiwa Spika, kuhusu zoezi la kuupigia kura Mlima Kilimanjaro. Ni kweli kwamba kulikuwa na mashindano ambayo yalilenga kuibua vivutio vipya saba, ikiwemo viwili vya Afrika ambavyo ni *Table Mountains* ya Afrika Kusini pamoja na mlima wetu wa Mlima Kilimanjaro.

Kwa bahati mbaya sana zipo sababu kadhaa zilizosababisha sisi tusipate kura nyingi; moja ni kwa sababu ya *access* ya *internet.* Kwa sababu, kwa muda mrefu kura zilikuwa zikipigwa kwa kuingia kwenye *web site.* Watanzania walio wengi ukilinganisha na wenzao wananchi tuliyokuwa tukishindana nao, *access* yao kwenye *internet* ilikuwa ni ndogo.

Lakini vilevile baada ya kuwa tumefikia makubaliano na vyombo vya habari hasa mashirika au kampuni za simu, kuanza kupiga kura kwa *sms,* kidogo kura zikawa zimeongezeka. Tulifikia hatua hiyo kwa kuchelewa, jambo ambalo lingeweza kutusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo si kwamba, kufanya kampeni hiyo au kupiga kura hizo ni kama mambo yalivyo kwa *Miss Tanzania,* isipokuwa tu hatukuwa tumejiandaa vizuri kuanzia *connections* zetu zilivyo, lakini pia kuweza kufanya mawasiliano na kampuni za simu. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri mwezi uliopita alifanya ziara katika Jimbo la Rombo kwa ajili ya kuhimiza utalii, hasa wa Mlima Kilimanjaro pamoja na utalii wa ndani. Na kwa kuwa, nimekuwa nikipokea simu nyingi sana kutoka kwa wananchi wa Rombo, wakimpongeza Mheshimiwa Waziri wa ziara yake na mimi mwenyewe ninampongeza kwa ziara hiyo ambayo ilikuwa ya kihistoria.

Mheshimiwa Spika, Je, Mheshimiwa Waziri, yuko tayari kupokea pongezi hizo na kuharakisha yale ambayo aliahidi kwa wananchi wa Rombo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Selasini, kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba nimshukuru sana yeye pamoja na wananchi wa Rombo kwa ushirikiano mkubwa walionipa kwenye ziara ile. Lakini niwashukuru sana kwa pongezi ambazo wanazitoa kwa Wizara yetu kwa jitihada tunazozifanya. Nimhakikishie kwamba, pongezi hizo na kutuunga mkono kunatupa moyo na kutufanya tufanye kazi kwa bidii zaidi.

Nimhakikishie pia kwamba, yale tuliyoahidi kuyafanya na kama nilivyomwambia kuna mambo tutahakikisha *by December* tutakuwa tumeyakamilisha ikiwemo kulipa kifuta machozi kwa wananchi walioharibiwa mazao yao. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba, kama ambavyo nilisema kwenye ziara; tutahakikisha tunayafanya.

Na. 62

**Mikakati ya Kuendeleza Sekta ya Utalii**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Jimbo la Mbogwe, limejaliwa kuwa na Hifadhi ya Misitu na Wanyamapori ya Kigosi-Moyowosi:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuendeleleza Sekta ya Utalii na kuitangaza hifadhi hiyo ndani na nje ya nchi ili nayo iweze kuchangia katika pato la Taifa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mapori ya akiba ya Kigosi na Moyowosi kwa kipindi kirefu yameendelezwa kwa ajili ya matumizi ya uwindaji wa kitalii, ambao pia ni aina mojawapo ya utalii na kampuni za uwindaji zipatazo nne zimekuwa zikifanya shughuli hiyo. Katika kuendeleza sekta ya utalii kwenye maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuyatangaza mapori hayo na kuyaendeleza kwa ajili ya uwindaji wa kitalii.

Mojawapo ya jitihada ambazo Serikali imekuwa ikifanya ni kuyatangaza mapori hayo kwenye maonesho ya *“Reno Convention”* ambayo huandaliwa na kampuni ya *Safari Club International* na kuhusisha wadau wa Utalii kutoka nchi tofauti duniani, ambao hukutana katika mji wa Nevada, nchini Marekani kila mwaka kwa lengo la kutangaza vivutio vinavyopatikana kwenye maeneo ya nchi zao. Mikakati zaidi ya kutangaza mapori haya kwa utalii inaendelea kufanyika,

ikiwamo kuyatangaza kupitia maonesho ya uwindaji yanayofanyika Abu-Dhabi katika Jumhuri ya Falme za Kiarabu, ambayo tumeshiriki toka mwaka wa 2009.

Mheshimiwa Spika, fursa hii ya kuendeleza na kuyatangaza maeneo hayo, imechangia kuvutia wageni hususan kutoka Marekani na Ulaya na hivyo kuchochea ukuaji wa Utalii wa maeneo husika pamoja na kuongeza pato la Taifa. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita toka mwaka 2008, jumla ya kiasi cha dola za Marekani 1,613,322 kilikusanywa, zikipatikana kutokana na watalii 154 wa uwindaji waliotembelea maeneo hayo. Sambamba na kuongezeka kwa pato hilo, Wilaya za Kahama na Bukombe zinanufaika na mchango wa 25% wa mapato yanayotokana na uwindaji huo.

Mheshimiwa Spika, ili kupanua wigo wa utalii katika maeneo hayo, Sheria Namba 5 ya mwaka 2009 ya Wanyamapori, imeruhusu utalii wa aina nyingine, ukiwemo utalii wa picha, kufanyika kwenye maeneo ya vitalu vya uwindaji pale ambapo uwindaji unakuwa haufanyiki. Wizara yangu kwa kushirikiana na wawindaji ambao wamepata *concession* kwenye maeneo hayo, itahimiza ufanyikaji au uendelezaji wa utalii wa picha kwenye maeneo ya Bokombe na Mbogwe.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kumwuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza. Ni lini Serikali sasa itaanza kutenga fedha kwenye Bajeti yake kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara katika hifadhi ya Moyowosi na Kigosi pamoja na kuimarisha *game Rangers Posts?*

Mheshimiwa Spika, ni vigezo vipi vinatumika kuyapandisha hadhi mapori ya akiba kuwa *National Parks?* Na ni lini sasa Kigosi-Moyowosi itageuzwa kuwa *National Park* katika nchi hii?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Agustino Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu utengaji wa Bajeti za kuimarisha miundombinu. Wizara imekuwa ikitenga fedha kila mwaka na hata Mwaka huu wa Fedha, kuna fedha ambazo tumetenga kwa ajili ya kuimarisha barabara za maporini lakini vilevile kujenga vituo vya nje *(Out Posts For Game Rangers).* Aidha kuna kituo kimoja kidogo tunajenga Wilaya ya Mbogwe, ambayo zamani eneo hilo lilikuwa Wilaya ya Bukombe. Wizara itaendelea kufanya hivyo kwa kadiri fedha zinavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupandisha mapori ya akiba kuwa *National Parks,* utaratibu ambao upo unafanyika ni kuanzia kwenye ngazi za Mikoa inayohusika na kwa sasa tunaanzia kwenye Kamati ya Wilaya, kwa maana ya Kamati ya Ushauri ya Wilaya, *DCC.* Wakishakaa wakalijadili suala hilo wakaona kwamba linakubalika na baadaye wanajadili kwenye *RCC,* baada ya hapo wanatuletea taarifa hizo Wizarani. Wizara inafanya mchakato wa kisheria unaokuwa umebakia kwa ajili ya kutangaza eneo hilo kuwa *National Park.*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru wananchi wa Mbogwe na Bukombe na maeneo mengine ambao wanaona jambo hili kwamba ni la muhimu, hasa kutokana na *pressure* iliyoko katika maeneo yaliyohifadhiwa.

Lakini pia niwashukuru wananchi wa Kusini wa Mkoa wa Mtwara, ambao pia wamekuwa wakizungumzia kupandisha hadhi mapori ya Msanjesi na yenyewe kuwa *National Park.* Sisi kama Wizara wakishakamilisha mchakato kwenye *RCC,* tutaendeleza hatua itakayokuwa imebaki.

**MHE. PAULINA P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa, kumekuwa na migogoro mingi katika hifadhi nyingi Tanzania sasa hivi kuongeza mipaka yake na hivyo kusababisha maeneo ya wananchi wengi kuchukuliwa. Mfano mzuri ni wananchi wa Wilaya ya Babati, Vijiji vya Ayamango, Mijedabu na Gedamar. Maeneo yao yamechukuliwa na Hifadhi ya Tarangire na hadi leo hawajalipwa fidia.

Je, ni lini sasa Serikali itawapa wananchi wa maeneo hayo fidia ya maeneo yao yaliyochukuliwa na Hifadhi ya Tarangire?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati wa kujumuisha mjadala wa Bajeti ya Wizara yangu, mwezi wa nane mwaka huu 2011. Nilisema miongoni mwa maeneo ambayo mjadala au mzozo au ubishi ambao umekuwepo kuhusu mipaka ni pamoja na eneo hili alilolitaja Mheshimiwa Mbunge.

Eneo hili, mzozo umekuwepo kwa muda mrefu na majadiliano sasa hivi yameshakamilika kati ya wananchi na hifadhi na kinachofanyika sasa hivi ni kupitia uongozi wa Mkoa, kutafuta eneo la mbadala kwa ajili ya wale wananchi ambao kwa hiyari yao wamekubali kuhama, baada ya kukubali kuondoa kesi waliyokuwa wameweka Mahakamani.

Niombe tu kwamba Mheshimiwa Mbunge na Uongozi wa Mkoa, waongeze ushirikiano kwa Wizara yangu kuhakikisha kuwa suala hili linaisha. *(Makofi)*

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, iliiomba Wizara kuchukua pori lake la akiba la *Rwafi Game Reserve* kwa makubaliano ya kurekebisha mipaka ili kuwaachia wananchi matumizi ya eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Je, Wizara imefikia hatua gani katika kurekebisha mipaka hiyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Wizara iliombwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi kuchukua pori la Rwafi ambalo liko chini ya Halmashauri, ili liweze kusimamiwa na Wizara. Tulisema kwamba, kuanzia mwezi Julai mwaka huu, eneo hilo tutaanza kulisimamia.

Tayari tumeshatuma watu kwenda kule kwa maana ya askari ambao watakuwa wanafanya kazi kwa kuanzia kwa kushirikiana na askari wa Wilaya au Viongozi wa Wilaya. Katika kufanya kazi hiyo, Uongozi wa Mapori ya Akiba ya Rwati, utashirikiana na Uongozi wa Wilaya ya Nkasi katika kupitia upya mipaka.

Kwa hiyo, kwa sasa hivi mchakato wa kupitia mipaka unaendelea na utaratibu wa kusimamia umeshaanza.

Na. 63

**Utekelezaji wa Mradi wa Visima Vya Maji**

**MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE (K.n.y. CATHERINE V. MAGIGE)** aliuliza:-

Mwaka 2008/2009 Halmashauri ya Arusha ilihamasisha wananchi katika vijiji mbalimbali wilayani humo, kuchangia mradi wa uchimbaji wa visima vya maji ya kunywa uliopangwa kutekelezwa chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi hao waliochangishwa fedha zao?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Watendaji wanaokwamisha utekelezaji wa mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa wananchi katika vijiji vya Halmashauri ya Arusha, wamechangia fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika vijiji vyao. Wananchi kuchangia miradi ya maji ni maelekezo ya Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002. Lengo la uchangiaji huo ni kuwapa umiliki wa miradi wananchi watakaonufaika na kuonesha uwezo wao kuiendesha.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Miradi ya Maji utafanyika kwa awamu, kufuatana na upatikanaji wa fedha. Wananchi waliochangia fedha wawe na subira kwa kuwa Miradi yote inatekelezwa kwa awamu. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, hadi kufikia tarehe 28 Oktoba, 2011, visima sita vilikuwa vimechimbwa katika Kijiji cha Bwawani visima viwili, Loovilukuny visima viwili na Ngaramtoni visima viwili. Kati ya visima hivyo, visima ambavyo havina maji ni katika Vijiji vya Bwawani kisima kimoja na Ngaramtoni kisima kimoja. Kwa Vijiji vya Oloitushula, Nengung'u, Losikito na Likamba, vitatumia kisima kimoja kitakachochimbwa eneo la Shamba la Magereza ambalo lina maji mengi.

Vijiji vya Nduruma, Oloigeruno na Ikirevi, vitapata maji kupitia Mradi wa Maji ya Mtiririko, ambapo usanifu katika Kijiji cha Oloigeruno na Ikirevi umekamilika na makabrasha ya usanifu yamewasilishwa Wizarani kwa ajili ya kupitiwa. Jumla ya shilingi bilioni 807.6 zimetengwa katika bajeti ya mwaka huu wa 2011/2012, kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto mbalimbali zilizosababisha utekelezaji wa Miradi katika Vijiji Kumi nchini kuchelewa ikiwa ni pamoja na uchache wa Wataalam Washauri na Wataalam kwenye Halmashauri kukosa ujuzi wa manunuzi kwa kufuata taratibu za Benki ya Dunia. Hata hivyo, ninashauri kuwa, iwapo kuna Watendaji waliokwamisha utekelezaji wa Miradi kwa makusudi kwenye Halmashauri, Wakurugenzi husika wanaagizwa wachukue hatua stahiki.

**MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, ningependa kuuliza maswali yafuatayo:-

(i) Je, ni lini hasa Mradi huo wa *World Bank* utaanza kutekelezwa kwani Wanawake wengi wa Mkoa wa Arusha wanapata shida ya maji. *(Makofi)*

(ii) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji yuko tayari kuja Mkoani Arusha ili aone hali ngumu ya maji inayowakabili Wanawake wa Mkoa huo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waone wanawake hata huku wamebeba ndoo, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Namelok Sokoine, kama ifuatavyo:-

Anauliza ni lini Mradi utatekelezwa; katika jibu la msingi nimeeleza kwamba, tumeshaanza kuchimba visima na kazi inayoendelea sasa hivi ni kujenga miundombinu. Kwa hiyo, Mradi unaendelea kutekelezwa kwa awamu.

Kuhusu mwaliko wa kwenda Arusha, ninaomba nimuahidi kwamba, nipo katika mipango ya kwenda Arusha kuangalia matatizo ya Mradi huo. Ahsante.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Kwa kuwa Mradi huu wa Maji chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia umekuwa na matatizo maeneo mengi nchini na hasa katika maeneo yote ambayo Miradi imekuwepo; je, Serikali inatumia jitihada gani kuhakikisha kwamba Miradi hii inakamilika kwa wakati mwafaka?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakosi, kama ifuatavyo:-

Kweli tunatekeleza Mradi wa Vijiji Kumi nchi nzima na kama nilivyosema, tumekuwa na changamoto mbalimbali; changamoto moja kubwa ni upatikanaji wa fedha za kutosha kwa sababu Miradi hii mwanzoni ilikuwa imefikiriwa kwamba, ingejenga visima. Baada ya kufanya usanifu ikaonekana sehemu nyingi tunahitaji Miradi Mikubwa ya Mtiririko au kuchukua maji kwenye mito au mabwawa ambayo yanahitaji fedha nyingi. Sasa mipango ya Serikali tumeamua kwamba, maji ni kipaumbele katika Mpango wa Miaka Mitano, tutawekeza fedha nyingi zaidi kwenye Sekta ya Maji. Kwa hiyo, tutakuwa na uwezo zaidi wa kufikia maeneo mengi.

Na. 64

**Bodi ya Kahawa Kuandikisha Mashamba ya Wakulima**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO** aliuliza:-

Sheria ya Kahawa inataka Bodi ya Kahawa Tanzania *(TCB)* kuandikisha mashamba ya wakulima:-

Je, ni lini Bodi ya Kahawa itafanya kazi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Kahawa Na. 23 ya Mwaka 2001 na Kanuni zake za Mwaka 2003, Bodi ya Kahawa Tanzania, inawajibika kuwaandikisha wakulima wote wa kahawa nchini ili kuwa na takwimu sahihi kwa ajili ya mipango ya kuendeleza zao hilo. Ili kutekeleza Sheria hiyo, Bodi ya Kahawa ilianza kutekeleza agizo hilo kwa majaribio katika Mkoa wa Mbeya mwaka 2010 na matokeo ya majaribio hayo yametumika kukamilisha nyaraka zinazotumika sasa kuandikisha wakulima wa kahawa katika nchi nzima.

Zoezi la kuwaandikisha wakulima wa kahawa nchini, lilianza tarehe 7 Oktoba, 2011 ambapo uzinduzi wa kazi hiyo ulifanyika Wilayani Muleba, Mkoa wa Kagera. Kazi hiyo ya uandikishaji wa wakulima imepangwa kukamilika kabla ya tarehe 31 Desemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, manufaa ya kuwa na Daftari ya Wakulima ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kupata takwimu za kutumia wakati wa kupanga mipango ya maendeleo ya Zao la Kahawa;

(ii) Kurahisisha makadirio ya mahitaji ya tasnia ya kahawa hususan katika miundombinu na kuimarisha upatikanaji wa huduma za ugani, pembejeo na miche bora; na

(iii) Kusaidia kupata taarifa za uzalishaji ili kusaidia uwekezaji katika usindikaji na upatikanaji wa masoko mazuri.

Ninapenda kutumia fursa hii, kuwaomba wakulima wote wa kahawa nchini, kushiriki kikamilifu katika zoezi hili la uandikishaji wa mashamba.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa kuwa jibu la Serikali limeeleza wazi manufaa ya zoezi hili na yapo manufaa matatu; na kwa kuwa Sheria hii ni ya 2001 maana yake ni kwamba miaka kumi imepita bila kutekelezwa;

na kwa kuwa wakulima hao wa kahawa wamepunjwa hata ule msingi kutokana na kutokutekelezwa Sheria hii:-

(i) Je, Serikali ipo tayari kuwaomba radhi wakulima wa kahawa kwa kuwachelewesha namna hii na hivyo kuishi katika umaskini na hasa tukizingatia kwamba huu ni mwaka wa 50 wa Uhuru wetu na ni Jubilee na kadiri ya misingi ya Biblia inatakiwa kusameheana?

(ii) Mheshimiwa Waziri amesema kwamba zoezi hili litaisha kabla ya tarehe 31 Desemba, 2011 na leo ni tarehe 14 Novemba; kwa hiyo ni kabla ya tarehe 31 Desemba, 2011. Je, zoezi hili litaanza lini na litaisha lini katika Jimbo la Mbinga Mashariki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba majibu yawe kwa kifupi kwa sababu muda umetupita.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Ushirika, ninaomba niwahakikishie kwamba, tulianza kufanya majaribio katika Mkoa wa Kagera na uzoefu uliopatikana ndiyo tunaoutumia sasa kueneza katika nchi nzima. Sasa tumeshakamilisha zoezi hilo, zoezi linakwenda vizuri na ndiyo maana nina hakika kwamba, ifikapo tarehe 31 Desemba, 2011 tutakuwa tumekamilisha zoezi hili, maana sasa linaendelea kwa nguvu zote. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Kayombo, aelewe kwamba, zoezi hili linakwenda vizuri na hatimaye wakulima wa kahawa wote watasajiriwa katika daftari hili.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa utaratibu huu wa kuwaorodhesha wakulima wa kahawa unafanana sana na utaratibu wa kuwaorodhesha wakulima wa mahindi katika kupatiwa vocha; na kwa kuwa utaratibu wa kuwaorodhesha wakulima wa mahindi na kupatiwa vocha umesababisha uzalishaji mkubwa sana wa Zao la Mahindi katika Jimbo la Peramiho:-

Cha kusikitisha wakulima wale mpaka sasa wanahangaika hawajalipwa fedha za mazao waliyouza na mazao yao mengine yapo yananyeshewa na mvua katika vituo vya kununulia mazao hayo, hakuna majibu na hakuna maelezo. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kupokea maelezo yangu binafsi kwa niaba ya wakulima wale wanaohangaika bila mwenyewe na yeye kuyatolea majibu ndani ya Bunge hili ili kuwapa matumaini mapya ya maisha yao*? (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, swali zito sana, hawa watu mahindi yao yamenyeshewa hebu jibu hilo.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri. Swali la msingi lilikuwa *enumaration* ya wakulima wa kahawa; ninapenda nitoe jibu kuhusu suala la mahindi kama ifuatavyo:-

Kwanza, katika eneo analolisema Mheshimiwa Mbunge, mvua zilianza mapema kabla ya wakati wake na kwa sababu hiyo, Serikali ilichukua jukumu kuyachukua mahindi yote ambayo yalikuwa kwenye vituo vya ununuzi, kuyapima na kuchukua dhamana yake. Katika wiki hii, wakulima ambao mahindi yao yalikuwa kwenye vituo na yakachukuliwa na Serikali, yataanza kulipwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchukua mahindi yale ya mwanzo, Serikali iliwatangazia wakulima wasubiri wasilete mahindi katika vituo kwa sababu kulikuwa hakuna matayarisho ya kutosha kuhusu malipo kwa wakulima wengi ambao wameleta mazao.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya, kuna wakulima ambao hata baada ya kutangaziwa kwamba wasipeleke mahindi kwenye vituo, waliyapeleka na mahindi hayo yataanza kununuliwa katika wiki hii. Ahsante.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara inayofuata ya Uchukuzi; Mheshimiwa Deo Filikunjombe atauliza swali hilo, kumbe upo, lilishataifishwa hilo swali, haya Mheshimiwa Filikunjombe.

Na. 65

**Ahadi ya Meli ya Tani 400 Ludewa**

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE** aliuliza:-

Rais Jakaya Mrisho Kikwete aliahidi kuwanunulia meli ya tani 400 Wananchi walio karibu na Ziwa Nyasa (Ludewa):-

(a) Je, utekelezaji wa ahadi hiyo umefikia wapi?

(b) Je, ni maandalizi gani ya kimiundombinu kama ujenzi wa magati na bandari yaliyokwishaanza kwa ajili ya kupokea meli hiyo kubwa na mpya?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imeshaanza mchakato wa kutafuta pesa za ununuzi wa meli moja mpya kwa ajili ya Ziwa Nyasa. Serikali kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la Denmark *(DANIDA),* imefanya upembezi yakinifu na kubaini mahitaji ya ukarabati mkubwa wa meli zilizopo na ununuzi wa meli mpya katika Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria, kulingana na mahitaji. Upembuzi yakinifu umekamilika mwezi Septemba, 2011 na umeonesha kuwa meli moja ya kisasa itanunuliwa kwa ajili ya Ziwa Nyasa. Meli hii itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 320 na mizigo tani 180 na itagharimu Dola za Kimarekani milioni tisa. Ujenzi wa meli mpya unatarajiwa kuanza mwaka 2013 na utakamilika mwaka 2015. Aidha, ripoti ya upembuzi yakinifu imewasilishwa Serikali ya Denmark, kwa ajili ya kuomba ufadhili wa ujenzi wa meli hizo.

(b) Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari, inaendelea na juhudi za kuboresha miundombinu katika bandari za Ziwa Nyasa kama ifuatavyo:-

(i) Kuanza ujenzi wa gati jipya la kuhudumia abiria na mizigo mwezi Desemba, 2011 na ukarabati wa jengo la abiria *(passenger lounge)* katika Bandari ya Kiwira unaendelea na utakamilika katika Mwaka huu wa Fedha wa 2011/2012;

(ii) Ujenzi wa ghala la mizigo katika Bandari ya Kiwira utaanza mwaka 2012/2013;

(iii) Kuondoa mchanga na ukabaratabi wa Gati la Itungi katika kipindi cha mwaka 2011/2012 kwa kushirikisha sekta binafsi itakayowekeza katika kuchimba na kusafirisha shehena ya makaa ya mawe kupitia bandari hii; na

(iv) Upanuzi wa gati katika Bandari ya Mbamba Bay ambapo ujenzi umepangwa kufanyika katika kipindi cha Mwaka huu wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Kapteni Komba ananisikia kwa hilo. Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kupitia Mpango Kabambe wa Bandari *(Ports Master Plan),* inatarajia kujenga miundombinu katika Bandari za Manda, Liuli na Ndumbi katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013. Aidha, uboreshaji wa miundombinu hii umezingatia mahitaji ya miundombinu kwa ajili ya kuhudumia meli zilizopo sasa na meli mpya itakayonunuliwa.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niliuze swali la nyongeza. Nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(i) Vituo ambavyo Mheshimiwa Waziri amevitaja kwamba wanajenga magati au kukarabati ni Kituo cha Manda peke yake. Wananchi wa Ludewa wanahudumiwa na Kituo cha Lupingu. Kituo cha Lifuma ni kwa ajili ya Makonde pamoja na Msisi. Pia kuna Kituo cha Ifungu kule Kilondo na Kituo cha Matema. Vituo hivi mlivyoviacha hamwoni kwamba Wananchi hawa wa Ziwa Nyasa watakosa huduma hii ya meli mpya? *(Makofi)*

(ii) Ninapenda kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri; tumejadili sana humu ndani, je, meli hii inayokuja Ludewa itakuwa mpya au itakuwa chakavu; kwa sababu tusingependa Ludewa yatokee yale ambayo yalitokea kwa MV Bukoba au yaliyotokea kule Nungwi?

Mheshimiwa Waziri kwenye maelezo yako umetaja pia maneno mengi sana kuwa juhudi zinaendelea, upembuzi yakinifu unafanyika, mchakato, Wananchi wa Ludewa hawataki majibu haya ya mchakato na upembuzi yakinifu, tunataka meli. Tunaomba kupata kauli yako thabiti Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Unajibu maswali mawili tu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe, mimi pia nimekwenda naye mpaka Manda, hali kule nimeiona; ni kweli Wananchi wa maeneo ya Lupingu na Lifuma katika sehemu ya Nsisi na Kilindo mpaka Matema, wanategemea usafiri wa maji pekee kwa sababu kule hakuna barabara.

**SPIKA:** Ninaomba majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Ndiyo, Wizara kwa kulitambua hili, imeanza kufanya *study* itakayopelekea kujenga magati, yaani *jet* katika maeneo hayo. Hivyo, nitoe wasiwasi wa Mheshimiwa Filikunjombe na Wananchi wa maeneo hayo kwani Serikali yao inatambua mahitaji yao.

Kuhusu suala la meli chakavu, katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, tumezungumzia kwamba, tunapeleka kule meli mpya, lakini nisisitize tu hata meli ambayo ni kuukuu, ikifanyiwa ukarabatiwa inaweza kufanya kazi ya uhakika kabisa.

**SPIKA:** Iliyotumika tunasema hivyo, Mheshimiwa Capt. Komba, yeye ndiyo anatoka huko huko.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA**: Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza. *(Kicheko)*

Katika Ziwa lile kuna meli moja tu ambayo inafanya kazi sasa MV Songea na katika ... *(Kicheko)*

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA**: Mnacheka nini?

**SPIKA:** Endelea tu unawasikiliza nini?

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA**: Katika kuwafanya Wananchi wale waweze kupata usafiri wa uhakika; meli hiyo itakarabatiwa lini; na kama itakarabatiwa hivi karibuni ili watu wapate meli ya uhakika ya usafiri nini mbadala wake?

**SPIKA:** Wanachosema, *ze commedy* hawajakosea! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kapteni Komba, kama ifuatavyo:-

Nimeeleza katika jibu langu la msingi kwamba, tumefanya *study* hizi ili zifanyiwe matengenezo. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi, hivi sasa tunaendelea na matengenezo, meli hizi zitatengenezwa ili ziungane na MV-Songea.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini. Muwe mnaangalia muda Waheshimiwa, sasa nitamwita Mheshimiwa Livingstone Lusinde, aulize swali hilo.

Na. 66

**Kupeleka Umeme Jimbo la Mtera**

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE** aliuliza:-

Bwawa la Mtera ni chanzo kikubwa cha kuzalisha umeme nchini na kipo kwenye Jimbo la Mtera ambalo lina vijiji 62 na kati ya hivyo ni vijiji viwili tu vyenye umeme:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme kwa Wananchi wa Jimbo hilo na Taasisi zilizomo humo ndani Shule za Sekondari?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kutowapatia umeme Wananchi wanaozunguka Bwawa la Mtera kunawavunja moyo wa kutowajibika kikamilifu katika kutunza mazingira ya Bwawa hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mbunge wa Mtera, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ninaomba nirejee maelezo niliyoyatoa humu Bungeni kuhusu namna ambavyo Serikali imeweka kipaumbele cha kufikisha huduma ya Nishati ya Umeme kwa maeneo maalum kama sehemu za huduma za afya, elimu, hususan pale ambapo pana maabara na mabweni, pampu za maji na kadhalika. Ninaomba nisisitize kwamba, hii ni sehemu ya mkakati wa Serikali kufikisha huduma hii muhimu kwa Wananchi wake na kikwazo kikiwa ni upatikanaji wa fedha na siyo ukosefu wa mpango. Aidha, Serikali inashirikiana na Wakala wa Nishati Vijijni na *TANESCO* ili kubaini njia mbadala za kufikisha Nishati ya Umeme kwa ajili ya madhumuni hayo yaliyotajwa.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa vijiji viwili ndiyo vimepatiwa huduma ya umeme katika Jimbo la Mtera, Wilaya ya Chamwino. Vijii hivyo ni Mvumi Makuli na Mvumi Mission. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 Serikali kupitia Mradi wa *Millennium Challenge Coorperation (MCC),* imepanga kupeleka umeme katika Jimbo la Mtera, Wilaya ya Chamwino, kwenye Vijiji vya Iringa Mvumi, Makang'wa, Nkulabi na Mlowa Barabarani. Utekelezaji wa Mradi huu tayari umeanza tangu mwezi Mei, 2011. Aidha, katika Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Umeme Msongo kV 400 kutoka Mtera hadi Shinyanga kwa kupitia Dodoma na Singida, Vijiji vinavyopitiwa na njia hii vya Fufu, Manzase, Chipogolo, Kisima na kadhalika vitapatiwa huduma ya umeme. Kwa hiyo, mpaka zoezi hilo litakapokamilika, vijiji kumi vilivyotajwa vitakuwa vimepatiwa umeme.

(b) Mheshimiwa Spika, ninapenda kumsihi Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wote wanaozunguka Bwawa la Mtera, kutambua kuwa, Serikali inafahamu uhitaji wao wa huduma mbalimbali za kijamii ikiwa ni pamoja na umeme na kwamba inaendelea kutafuta fedha za utekelezaji wa miradi ya kufikisha umeme vijiji vinavyozunguka Bwawa la Mtera kama ilivyo kwa maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufafanuzi huu, ninapenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mtera, Serikali haidhamirii kuwavunja moyo Wananchi wake; hivyo, tunawaomba Wananchi wote wakiwemo wa Jimbo la Mtera na Wananchi wa vyanzo vingine vinavyoleta maji Mtera, kuwa wavumilivu na waendelee kulinda na kutunza mazingira pamoja na miundombinu ya umeme.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, majibu ya leo siyo makavu sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na vijiji alivyovitaja vingine siyo vya Jimbo la Mtera kama Mkulabi ipo Dodoma Mjini, Kisima hakipo kwangu, kwa hiyo ni vijiji vinane tu.

Kwa kuwa umeme umepita katika Kata ya Muungano na Kata ya Muungano walishakuwa wamehamasika kung'oa ile nguzo kwa sababu hawaoni faida yake maana wao hawana umeme lakini nguzo zimepita kwenye kijiji chao; na kwa kuwa hata katika mpango huo haijatajwa Kata ya Muungano na vilevile Shule ya Sekondari ya Handali iko jirani sana na Mvumi Mission:-

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari kuongozana na mimi kwenda kuona ukaribu huo na mahitaji ya Wananchi ili mimi na wewe tuweze kuwashauri waweze kuingiza katika mpango huo na waweze kuvuta subira ya kung'oa ile nguzo? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Lusinde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba nikubali kwamba, tutaongozana kwenda kuangalia hali halisi ya Kata ya Muungano na pia tutachukua Wataalamu wa TANESCO ili wakabainishe kama nyaya zinazopita pale ni za msongo wa kV 33 au 11, ni nyepesi zaidi kupooza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie kwamba, tutakwenda, *Inshallah!*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu mtiririko alioutaja wa Vijiji amevitaja Vijiji vya Jimbo la Mheshimiwa Lusinde na Vijiji vya Jimbo la Kibakwe ambalo ninatoka na katika kutaja kwake ule mtiririko hauko sawasawa kwani vingine vimerukwa katika *line* inayokwenda kwa Mheshimiwa Lusinde; na kwa kuwa ahadi ya Makamu wa Rais ni kupeleka umeme katika Kijiji cha kutoka Kisima, Chipogolo, Mtamba mpaka Rudi; sasa kwa mchoro huo ninachokiona ni mkanganyiko mkubwa:-

Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari tukakae ili asije akatuletea ugomvi huko kwa sababu vijiji vimeongezeka; kwa mfano cha Msisiri na Kibwegere sasa ni vijiji na ndivyo vinavyozunguka lile Bwawa; sasa sijui hali ikoje kwa sababu alichokisema hapa ni tofauti na hali halisi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa George Simbachawene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Miradi ailiyouliza Mheshimiwa Lusinde, inategemeana pia na *connectivity* na *transmission* walizopanga wenyewe *TANESCO* za namna ya kupelekea umeme, inawezekana mingine ikaenda kwenye jimbo lingine.

Mheshimiwa Spika, katika utaratibu huo huo pia kuna *transmission* nyingine inakwenda kwa Mheshimiwa Chibulunje, ambayo pia ni Jimbo la Chamwino.

Mheshimiwa Spika, mimi ninadhani niwasihi Waheshimiwa Wabunge wote watatu, kwa maana ya Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Livingstone Lusinde na Mheshimiwa Chibulunje, nikae nao ili waniambie katika ile njia ambayo nguzo zinapita, tujue namna ambavyo tutaweza kushusha umeme na upatikanaji wa vifaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimelikubali.

Na. 67

**Wilaya ya Kasulu Kupatiwa Umeme**

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA** aliuliza:-

Wilaya ya Kasulu ni miongoni mwa Wilaya kongwe lakini mpaka sasa haijapata umeme wa uhakika licha ya kuwepo kwa Mto Malagarasi ambao ungeweza kutumika kuzalisha umeme lakini hauzalishi kutokana na kuwepo kwa vyura.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutafuta eneo lingine mbadala la kuzalisha umeme kwani vyura hawapo sehemu zote?

(b) Je, Serikali ipo tayari kutekeleza Mradi wa Mto Malagarasi ambao ulishaandaliwa na ukaahirishwa tu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa maeleo mafupi kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumeeleza humu Bungeni awali, Mradi wa Umeme katika Mto Malagarasi ulihusu ujenzi wa Kituo cha Umeme chenye uwezo wa kufua umeme wa megawati nane lakini kwa sababu ya mazingira na taarifa za Wataalamu zilizobaini mazingira na viumbe adimu, Mradi ule umehama.

Kwa hiyo, kufuatia taarifa hiyo, upembuzi yakinifu *(feasibility study)* wa Maporomoko ya Igamba III na tathmini husika zote, zikiwemo athari za mazingira kwa eneo jipya la Igamba III, ulianza mwanzoni mwa Julai, 2010 na kukamilika Septemba, 2011, kama ilivyoelezwa hapa Bungeni tarehe 8 Novemba, 2011. Taarifa ya upembuzi yakinifu imekamilika na kukabidhiwa kwa Serikali kwa ajili ya kujadiliwa na Wataalamu wa *TANESCO* na Taasisi nyingine husika.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, pamoja na kuzingatia maelezo haya, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Buyogera kama ifutavyo:-

(a) Serikali imeona umuhimu wa kutafuta eneo lingine mbadala la kuzalisha umeme na kulifanyia upembuzi yakinifu, ambalo limebaini kutokuwa na athari za mazingira kama ilivyo kwenye eneo la Igamba I.

(b) Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO),* ipo tayari kutekeleza Mradi huo wa Umeme katika Maporomoko ya Igamba III unaotarajiwa kuzalisha MW 44.7 na sasa tunaelekea kwenye hatua za kutafuta fedha kwa ajili ya kuuendeleza tena Mradi huo.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba nishukuru kwa majibu mazuri, lakini pia niishukuru Serikali kwa kusimamia vyema ahadi za Mheshimiwa Rais kwa kufikisha umeme Wilaya ya Kasulu. *(Makofi)*

Baada ya utangulizi huo, ninaomba niendelee kwa kusema kwamba, Mheshimiwa Rais alipotembelea Mkoa wa Kigoma alituahidi kwamba umeme utakapowaka Kasulu watahakikisha Serikali inafikisha umeme Kijiji cha Kabanga, kutokana na huduma muhimu zilizopo pale kama vile Chuo cha Ualimu, Chuo cha *Nursing*, Hospitali ya Kabanga, Shule Maalum ya Mazoezi, Kituo cha Walemavu wa Ngozi na Gereji kubwa iliyopo katika Kijiji cha Kabanga:-

(i) Kwa kuwa Serikali kupitia *TANESCO* imeshafanya upembuzi na kubainisha kwamba Mradi ule unaweza ukakamilishwa kwa shilingi milioni 368; na kutokana na umuhimu huo Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu imepitisha shilingi milioni 108 ili kuonesha umuhimu wa kupata umeme Kijiji cha Kabanga; je, Serikali ipo tayari kutoa fedha hizo ili Kijiji hiki cha Kabanga kipate umeme?

(ii) Kwa kuwa Bunge lililopita Mheshimiwa Naibu Waziri aliniahidi kuunganisha umeme na Shirika la Wasambazaji wa Umeme Vijijini *(REA)* ili Jimbo la Kasulu Vijiji tuweze kupata umeme kupitia *REA*; na kwa kuwa umeme uliopo Kasulu…

**SPIKA:** Ninaomba ufupishe maswali yako umechukua dakika nzima.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Umeme uliopo Kasulu hakuna kijiji hata kimoja cha Kasulu Vijijini ambacho kimenufaika nao; Mheshimiwa Waziri upo tayari kutusaidia kupata umeme kupitia *REA* hasa kwa Shule za Sekondari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu maswali kwa kifupi kabisa, hizo zote zilikuwa ni hotuba tu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Agripina Buyogera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba nimshukuru kwa yeye mwenyewe kushukuru kwa kitendo cha kufikishiwa umeme na Serikali hii.

La kwanza la Kabanga, tumeshakubaliana; Halmashauri ya Kasulu, kwa kuzingatia umuhimu wa kupeleka umeme Kabanga wamejadiliana na wao wenyewe wametenga shilingi milioni 108 na taarifa niliyokuwa nayo mimi ni kwamba, hapa katikati ya mwezi huu wa Novemba, yaani tarehe 15, wamekubaliana wajadiliane kama malipo yale ya shilingi milioni 108 yatakuwa yameshakwenda.

Kwa hii shilingi milioni 200 iliyopungua, tumeshakubaliana kwamba, Serikali itaweka hii kupitia *TANESCO,* kwa hiyo, ni utaratibu tu wa wao kukubaliana, wakishaafikiana hayo malipo chini ya utaratibu wa ushirikishwaji wa kuchangia maendeleo, hili jambo tumeshalifanyia maamuzi linafanyika.

Kuhusu swali la pili, ninaomba nimuahidi kwamba, kazi ya kwanza ilikuwa kupeleka umeme Kasulu chini ya utaratibu wa Makao Makuu ya Wilaya. Sasa kwa sababu pale pana umeme wa ziada, kulingana na ule uliokuwepo pale, ninaomba nimuahidi kwamba, tutawaagiza *TANESCO* wafanye tathmini kwa yale maeneo yaliyokuwa jirani waende wakaangalie uwezekano wa kupeleka umeme kuunganisha maeneo mengine ya ziada.

Mheshimiwa Spika, tutalifanyia kazi.

Na. 68

**Wafanyabiashara wa Zanzibar Kulipishwa Kodi Tanzania Bara**

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS** aliuliza:-

Kero nyingi za Muungano zimekuwa zikitatuliwa kwa mazungumzo katika vikao:-

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza kwa vitendo kero ya Wafanyabiashara wa Zanzibar kulipishwa kodi mara ya pili wanapoleta bidhaa zao Dar es Salaam?

(b) Je, ni kwa nini Serikali ya Muungano imekuwa na kigugumizi kwa muda mrefu kuondoa kero hii hali ikijua kuwa inadhoofisha uchumi wa Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, Mbunge wa Chonga, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania, imechukua hatua madhubuti zinazolenga katika kuboresha huduma zinazotolewa katika kutoa na kuingiza bidhaa nchini, ikiwa ni pamoja na kuondoa kero ya ulipishwaji wa kodi itokanayo na tofauti ya thamani ya bidhaa kwa wafanyabiashara wanapoingiza bidhaa Tanzania Bara kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa katika kuondoa kero hii ni pamoja na kuanzishwa kwa mfumo ambao ushuru kwenye bidhaa zinazoingia Tanzania Bara unakadiriwa katika Ofisi moja tu, yaani *Central Data Processing Office* iliyoko Dar es Salaam. Vituo vingine vyote vya Forodha Tanzania Bara kama vile Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Julius Nyerere, Namanga, Bandarai ya Tanga, Sirari, Tunduma, Holili na Hororo, vinashughulikia ukaguzi wa bidhaa baada ya ushauri kukadiriwa katika Kituo cha Huduma za Forodha Dar es Salaam kwa kutumia mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu umeweka usawa katika ukadiriaji wa ushuru na kuondoa tofauti zilizokuwepo za ukadiriaji tofauti baina ya kituo na kituo. Ufumbuzi wa kudumu ni kwa SMZ kujiunga na mfumo huu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Muungano haina kigugumizi kuondoa kero zote zinazotokana na kulipishwa ushuru mara mbili kutokana na tofauti ya tathmini ya bidhaa zinazopitia Zanzibar kuingiza Bara na tayari inaamini kuwa, suluhu ya tatizo hilo imepatikana kwa kutumia mfumo wa *Central Data Processing Office* niliouelezea katika jibu la swali (a).

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu ya ki-*technically* aliyoyajibu Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, ninapenda nisahihishe jina langu ni Haroub Mohamed Shamis na siyo Shami.

(i) Je, Serikali ya Muungano haioni kuwa mfumo huu ulioanzishwa wa *Central Processing Data Office* umebuniwa makusudi ili kuiua kabisa Zanzibar kiuchumi?

(b) Serikali ya Muungano mara nyingi au daima imekuwa ikiiwekea vikwazo Zanzibar katika jitihada zake za kujikwamua kiuchumi. Je, nchi hii ina nia kweli na ustawi wa kiuchumi wa Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (GREGORY G. TEU):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kwanza, ninaomba radhi kwa kukosea jina lake badala ya Shamis nimeita Shami.

Mheshimiwa Spika, anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba mfumo wa *Central Data Processing Office* ulibuniwa kwa ajili ya kuiua Zanzibar kiuchumi, ninapenda nimweleze kwamba; siyo kweli. Lengo la mfumo huu ulioundwa lilikuwa ni kuweka usawa tu katika ukadiriaji wa ushuru na kuondoa tofauti ambazo zilikuwepo kati ya kituo na kituo kingine ikiwemo na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mfumo huo kabla ya kuanza ilikuwa vituo vyote hivi ambavyo vimevitaja katika jibu langu la msingi vilikuwa vinaweza kukadiria bidhaa moja, lakini makadirio yalikuwa tofauti, bei ilikuwa tofauti na ilikuwa inaleta mkanganyiko mkubwa sana. Sasa baada ya mfumo mpya kuanza ambao ni wa *Central Data Processing Office* ni kwamba, tayari kuna uwiano, vituo vyote ambavyo nimevitaja vikikadiria bidhaa, ushuru wake unakuwa ni mmoja kuliko ilivyokuwa zamani na ndiyo maana ninasema suluhu hapa ni Zanzibar kuingiza katika mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, anavyosema kwamba Serikali ya Muungano haina nia njema na ustawi wa kiuchumi wa Zanzibar, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ya Muungano ina nia njema sana na ustawi wa uchumi wa Zanzibar endapo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itajiunga na mfumo huu ambao unaboresha mapato ya nchi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante. Muda umekwisha na maswali ya msingi yote yamejibiwa.

Nina matangazo ya wageni na wageni waliopo katika Ukumbi huu ni Viongozi watano wa kikundi cha Ombeni Bila Kukoma Ministry cha Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Ndugu Joyce Elisha. Kwanza, Ndugu Joyce Elisha asimame kama yupo na kikundi chote kisimame. Ninaona watakuja baadaye.

Pia tuna wageni wa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, ambao ni Viongozi tisa wa Baraza la Vijana la CHADEMA. Karibuni sana, ahsanteni sana.

Kuna Viongozi sita kutoka Shirikisho la Vyuo vya Elimu ya Juu CCM Dar es Salaam. Hawa wageni wameletwa na Mheshimiwa Azzan Zungu. Karibuni sana na ahsanteni, kwani vijana ndiyo nguvu ya Taifa, tumieni ujana wenu kama ipasavyo.

Sasa ni matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala Bora, Mheshimiwa Pindi Chana, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuwa, kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo leo baada ya kipindi cha maswali katika Ukumbi Namba 231 uliopo ghorofa ya pili.

Mheshimiwa Diana Chilolo, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo watakutana kwenye kikao chao saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa B.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 7.00 mchana nao pia watakutana katika Ukumbi Na. 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 7.00 mchana, watakuwa na Mkutano katika Ukumbi wa Pius Msekwa C.

Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, Mheshimiwa John Mnyika, anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kuwa, leo saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao chao kwenye Ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Jengo la Utawala.

Tangazo lingine la Ofisini linasema kwamba, katika kuadhimisha Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania, taarifa zinahitaji kutambua Watanzania waliowahi kuliletea Taifa heshima kwa kupata medali, tuzo au heshima maalum za Kitaifa katika nyanja mbalimbali kama vile za kiuchumi, kijamii, sanaa, ugunduzi, uandishi, michezo na kadhalika. Kaimu *DAP* anasema ninaomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge juu ya suala hili ili kama wapo waliowahi kupata heshima hizo, tupate majina yao ili waweze kutambulika na Taifa. Ninaomba waandikishe majina yao mapokezi. Sasa kama mnawajua watu huko, wenye sifa hizo, basi tena mnatangaziwa.

Wakati ninasoma wageni waliopo hapa, ninayo heshima sana kutangaza kwamba, mbele ya Jukwaa la Spika tuna Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Abubakar. Mheshimiwa Abubakar, tumekuwa naye humu Bungeni, kiti chake kilikuwa pale; tunakupongeza sana kwa nafasi mpya uliyopata na tunakutakia mafanikio mema katika shughuli hiyo yote. Ahsante, karibu sana. *(Makofi)*

Sasa nina tangazo lingine; Waheshimiwa Wabunge, ninafikiri wiki iliyopita, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bunge, aliwatangazieni kuwa, zinatolewa Fomu za Maadili ya Viongozi, pale *reception*. Waheshimiwa Wabunge, ninawaombeni kwa moyo wote mkachukue zile fomu. Mwaka wa kwanza wamewahurumieni kwa sababu mlikuwa hamjui, sasa hivi kutokujua siyo msamaha wa kutokufanya inavyostahili. Tarehe 31 haipo mbali, kwa hiyo, mkiondoka hapa bila kujaza zile fomu, mjue mtasahau. Kwa hiyo, ondokeni hapa mkachukue zile fomu, mkazijaze vizuri, mzipeleke kwa wakati unaohusika. Mtakosa Ubunge wenu hivi hivi kwa urahisi tu na mali yenyewe hamna lakini mnashindwa kujaza fomu; kwa nini? *(Kicheko)*

Tunaendelea, halafu hawa jamaa wanaoacha vikaratasi wajifunze kuandika mambo ya Kiserikali, yanakuja kwa maandiko vizuri. NCCR-Mageuzi kupitia Katibu wao, Mheshimiwa Machali,

anaomba niwatangazie Wabunge wake kuwa watakutana saa 7.00 mchana *basement;* yaani ukumbi wote watu wanne tu! Ukumbi wote wa *basement;* kwanza mngeweza kuambiana hapa hapa.

Waheshimiwa Wabunge, nimemaliza matangazo. Katibu endelea na hatua inayofuata.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Kuhusu nini maana hatujafanya kitu chochote. Eeh!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI**: Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako; ninatumia kifungu cha 47 na 48, ninajua maudhui ya vifungu hivyo vya 47 na 48, lakini nimeona ni busara utupe mwongozo wako.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita imekuwa na matukio makubwa mawili katika nchi yetu; tukio la kwanza limetokea Mjini Mbeya, ambapo kulikuwa na vurugu Siku ya Ijumaa, tarehe 11 na Siku ya Jumamosi, tarehe 12 Novemba, 2011. Vurugu hizi zilisababisha mtu mmoja kufariki na watu wengine kadhaa kupigwa risasi na kujeruhiwa na wamelazwa hospitali na wengine kadhaa wamekamatwa wapo ndani.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mjini Tabora, lilitokea tatizo lingine kubwa ambalo tumeambiwa Vijana wa JKT Masange walivamia soko moja pale na kupiga Wananchi na kupora mali zao. Sasa haya ni matukio makubwa sana, ambayo katika busara ya kawaida ilikuwa ni vyema Serikali hapa Bungeni ingesimama na kutoa maelezo kwa Watanzania ili waweze kujua yaliyojili. Sioni kama busara Serikali ikaendelea kunyamaza wakati Watanzania wengi wamepata madhara na matukio haya makubwa. Ninaomba mwongozo wako katika hilo.

**SPIKA:** Ahsante. Tumekubaliana watafanya hivyo kesho.

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2011**
***(The Public Procurement Bill, 2011)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipoahirisha Shughuli za Serikali, Siku ya Ijumaa, tulikubaliana kwamba, leo mtoa hoja atatoa maelezo juu ya hoja mbalimbali zilizotolewa na Wabunge halafu tuingie kwenye hatua zingine.

Mimi niliambiwa mnakwenda moja kwa moja kwa mtoa hoja. Ninaomba muwe wachangamfu kidogo; Mheshimiwa Naibu Waziri halafu baadaye mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU):** Mheshimiwa Spika, ninapenda nikushukuru sana wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kwanza. Ninaunga mkono hoja iliyo mbele yetu kuhusu Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninapenda kutumia fursa hii, nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii, kwa umahiri na uwezo mkubwa walionao na kazi nzuri waliyoifanya katika kuboresha Muswada huu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, ambao ni nyenzo muhimu katika kutekeleza Bajeti ya Serikali ya Mapato na Matumizi. Aidha, ninawashukuru sana Wabunge wote, kwa michango yenu mizuri, ambayo imesaidia sana kuboresha Muswada huu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma. Wabunge waliochangia kwa kuzungumza na wale waliochangia kwa maandishi watatambuliwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atakapokuwa anahitimisha hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ninapenda niseme kwamba, Muswada huu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, una mchango mkubwa sana katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, kwa kuwa sehemu kubwa sana ya bajeti, hutekelezwa kupitia Sheria ya Ununuzi wa Umma. Jitihada zozote za kuimarisha Ununuzi wa Umma ni jitihada za kuimarisha udhibiti na matumizi ya Serikali. Hivyo, kutungwa kwa Sheria hii kunaendana na dhamira ya Serikali ya kukidhi matumizi yake, jambo ambalo linasisitizwa na Umma wa Watanzania wote. Kwa maana hiyo, Sheria hii ni muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, ninapenda kuchukua nafasi hii, kuchangia baadhi ya hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 kama ifuatavyo:-

Hoja nyingi zilizojitokeza zinalenga kuboresha Sheria hii ya Ununuzi wa Umma na hoja chache zinazohusu Sera zitafanyiwa kazi kwa kuwa ni za Kisera. Hoja ya kwanza ilikuwa inasema kwamba, Sheria iweke vifungu ambavyo vitawezesha makampuni ya ndani kupewa zabuni iwapo fedha zitakazotumika ni za ndani. Kwa maana nyingine *Local contractors* wapewe kipaumbele wakati wa kupewa zabuni; hii ndiyo hoja. Suala hili limezingatiwa katika Muswada kupitia vifungu vya 54 na 55.

Mheshimiwa Spika, Hoja nyingine Serikali itoe kauli kuhusu gharama kubwa za ununuzi wa bidhaa na huduma kulinganisha na bei zilizopo katika soko. Hali halisi wakati mwingine inaonesha kuwa, bei ya sokoni ni ndogo iliyooneshwa na kupitishwa katika *tender.* Gharama za ununuzi zitapungua kwa kiwango kikubwa, baada ya kuanza kutekeleza utaratibu wa kununua bidhaa mtambuka kwa kutumia *framework agreement* kupitia Wakala wa Huduma za Ununuzi *(GPSA).* Aidha, *PPRA* ipo katika mchakato wa kuandaa orodha ya bei elekezi kwa bidhaa na huduma mbalimbali ambazo zitasaidia katika kukadiria gharama wakati wa kufanya tathmini ya zabuni. Vilevile masharti ya kudhibiti bei katika ununuzi yataainishwa kwa kina katika Kanuni ambazo zitatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, Hoja nyingine ilikuwa tatizo la baadhi ya taasisi kutofuata Sheria ya Ununuzi wa Umma *(non compliance).* Baadhi ya taasisi kutofuata Sheria ya Ununuzi ni kutokana na bei za *tender* kuwa kubwa kuliko bei halisi za soko. Kwa hiyo, wengi au taasisi nyingi huwa zina utaratibu wa kukiuka Sheria hiyo. Suala hili limezingatiwa katika Muswada kupitia vifungu vya 16, 20 na kifungu cha 104.

Mheshimiwa Spika, Hoja nyingine ni Sheria itoe tafsiri ya neno *"Specification"*. Suala hili limezingatiwa na limewekwa kwenye Jedwali la Marekebisho. Tafsiri ya neno *"Specification"* itaonekana huko. Hoja nyingine ni *PPRA* hutoa adhabu ya Watendaji wa Taasisi za Ununuzi badala ya taasisi peke yake; suala hili limezingatiwa katika Muswada kupitia vifungu vya 16, 20 na kifungu cha 104(3).

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 51(2) kinatoa sharti kwa wazabuni wa ndani kuthibitisha nyaraka muhimu za usajili kwenye Bodi za Kitaalamu. Ninapenda ieleweke wazi kwamba, kifungu hiki hakiweki sharti la kumtaka mzabuni kuthibitisha usajili kwenye Bodi za Kitaalamu, bali kinapewa sharti kwa Kampuni ya ndani inayoshiriki zabuni iwe imesajiliwa kufanya biashara kulingana na sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, Hoja ni kwamba nyaraka za zabuni ziandaliwe kwa Lugha ya Kiswahili na Kiingereza; ni sahihi nyaraka za zabuni kuandaliwa katika Lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Suala hili limezingatiwa katika Muswada kupitia kifungu cha 57. Aidha, *PPRA* tayari imeandaa baadhi ya nyaraka za zabuni kwa Lugha ya Kiswahili, zinazohusu manunuzi madogo madogo yanayofanywa kwa njia ya *quotations*. Zoezi la kukamilisha nyaraka zote za zabuni kwa Lugha ya Kiswahili linaendelea.

Mheshimiwa Spika, Hoja nyingine ni kwamba, kifungu cha 50 kinachohusu matumizi ya huduma mtambuka kiwekewe msisitizo hasa kwenye Halmashauri. Serikali imeupokea ushauri huo na itazingatia ushauri uliotolewa. Kifungu cha pili cha Muswada, Taasisi zizingatie uuzaji wa vifaa

vya Serikali kwa njia ya zabuni. Uuzaji wa vifaa vya Serikali kwa njia ya zabuni unaleta uwazi. Hivyo, Serikali itazingatia ushauri uliotolewa.

Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi (*Performance Audits)* za *PPRA* zipelekwe kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC),* Kamati ya Hesabu za Serikali za Mashirika ya Umma *(POAC)* na Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC).*

Serikali inakubaliana na ushauri huo. *Oversight Committees* za Bunge zitapelekewa Taarifa za Ukaguzi wa Ufanisi za *PPRA* kwa taarifa na matumizi yao kama inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, kutoa vipaumbele katika ununuzi wa bidhaa au vifaa vinavyozalishwa nchini badala ya vinavyotoka nje ya nchi. Mheshimiwa Spika, *"Charity begins at home";* ni vyema kupewa kipaumbele katika ununuzi wa bidhaa na vifaa vinavyozalishwa hapa nchini ili kuwapa moyo na kuhamasisha uzalishaji wa ndani. Pendekezo hili limezingatiwa katika Muswada kupitia kifungu cha 54(2).

Mheshimiwa Spika, Hoja ni Miradi Mikubwa ya Umma ifanywe kwa ubia na Wazalendo au Makampuni ya nje yaingie mkataba wa uendeshaji na utekelezaji ufanywe na Watanzania badala ya kazi zote kufanywa na Makampuni ya nje. Suala hili litafanyiwa kazi kwa kuwa ni la Kisera.

Mheshimiwa Spika, Hoja nyingine inahusu Makampuni makubwa yanayopewa kandarasi, yawekewe sharti la kutenga asilimia kadhaa ya thamani ya Miradi kwa ajili ya kujenga ujuzi au *skills* kwa Watanzania wanaofanya kazi katika Makampuni hayo. Suala hili nalo litafanyiwa kazi kwa kuwa ni la kisera. Tunashukuru kwa ushauri huu mzuri, unaolenga kujenga ujuzi kwa Watanzania wanaofanya kazi katika Makampuni hayo ya kigeni/makubwa.

Mheshimiwa Spika, Hoja nyingine ni kwamba, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa na Kanuni zake, zifanyiwe marekebisho. Serikali ya Halmashauri za Mitaa (TAMISEMI), tayari imeanza kulifanyia kazi pendekezo hili. Hoja nyingine ilikuwa ni kuwashirikisha wadau wafuatao katika masuala ya ununuzi; Wizara ya Sayansi na Teknolojia na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS).* Serikali imepokea ushauri huu na inaahidi kwamba, wataalam husika watashirikishwa katika kuandaa viwango vya ubora. Hoja nyingine ni kwamba, kuwe na tovuti maalum kwa ajili ya masuala ya ununuzi. Tovuti kwa ajili ya masuala ya ununuzi zipo tayari nazo ni *www.ppra.go.tz, ppra.go.tz* na *www.gpsa.go.tz,* ambazo zinaweza kutumika na Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Hoja nyingine *PPRA* ifungue Ofisi za Kanda. Suala hili linazingatiwa na tayari lipo katika muundo wa Mpango Mkakati wa *PPRA* ambapo Ofisi nne za Kanda zitafunguliwa. Lingine ni kwamba, kuwepo kwa uwazi na kutocheleweshwa kwa mchakato wa zabuni. Suala hili limezingatiwa katika Muswada kama inavyoonekana katika vifungu vya 47, 48 na kifungu cha 104. Kanuni iainishe namna gani utaratibu wa *Force Account* unaweza kutumika katika kuleta tija. Utaratibu wa *Force Account* unatambuliwa na Kanuni za Ununuzi chini ya Sheria ya Mwaka 2004. Hata hivyo, utaratibu huu utaainishwa na kuboreshwa katika Kanuni zitakazotungwa chini ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya mafupi, ninaunga mkono hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii, kukushukuru wewe binafsi, Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Kambi ya Upinzani pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia kwa kuzungumza na wale waliochangia Muswada huu kwa maandishi. Maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge, yatasaidia sana katika uboreshaji wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kama ifuatavyo:-

Nianze na majina ya wachangiaji waliozungumza. Kwanza, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mheshimiwa Alphaxard Kangi Ndege Lugola, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba, Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa, Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mheshimiwa Mch. Peter Simon Msigwa, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Subira Khamisi Mgalu, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba na Mheshimiwa Rosweeter Kasikila.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Ester Matiko, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Henry Shekifu, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Omari Nundu, Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Gregory Teu, Naibu Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, majina ya waliochangia kwa maandishi ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Catherine Magige, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Ester Matiko, Mheshimiwa Namelok Sokoine, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Sylvestry Koka na Mheshimiwa William Mgimwa.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mheshimiwa Shaffin Sumar, Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Engineer Gerson Lwenge, Mheshimiwa Abdulsalaam Selemani Amer, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Kapteni John Komba, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, Mheshimiwa Zakia Meghji, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Amina Clement, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Amina Mwidau, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Regia Mtema, Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mheshimiwa Felista Bura, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Augustine Mrema, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mheshimiwa Aliko Kibona, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Fatuma Mikidadi, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu na Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi.

Mheshimiwa Spika, zipo baadhi ya hoja zilizotolewa na baadhi ya Wabunge ambazo ni muhimu na nitazitolea maelezo ya ujumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja mahususi ya kwanza ilihusu ununuzi wa vifaa maalum vilivyotumika. Hoja ya ununuzi wa vifaa vilivyotumika imechangiwa na idadi kubwa ya Waheshimiwa Wabunge kama siyo wote. Ninapenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, uamuzi wa Serikali katika suala hili, umezingatia mambo mengi ya msingi ikiwa ni pamoja na hali

halisi ya uwezo wa nchi yetu kiuchumi na kwamba nchi nyingi zinazoendelea zinatumia utaratibu huu katika kukabiliana na ushindani katika utoaji huduma za usafiri wa anga, majini na reli.

Mheshimiwa Spika, sekta binafsi pia inanufaika na utaratibu huu. Serikali haikusudii kutumia utaratibu huu kununua vifaa chakavu kama ambavyo imetafsiriwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Utaratibu huu unalenga kununua vifaa vilivyotumika *(used)* na kwamba utaratibu maalum utawekwa ili kuhakikisha kuwa muda wa matumizi ya vifaa hivyo tangu vilipotengenezwa pamoja na ubora wake unazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na maoni ya Waheshimiwa Wabunge juu ya kurekebisha kifungu cha 66 cha Muswada kinachoainisha kupata idhini ya Baraza la Mawaziri kabla ya kununua vifaa vilivyokwishatumika na baadala yake inapendekezwa kwamba, Waziri wa Fedha ndiye atakayekuwa anatoa idhini hiyo.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha ataunda Kamati Maalum, yaani *Ad hoc,* itakayokuwa na jukumu la kumshauri juu ya ununuzi wa vifaa vilivyotumika unaokusudiwa kabla ya kutoa kibali kwa taasisi husika. Aidha, Kamati hii Maalum itateuliwa kila mahitaji yatakapojitokeza kwa taasisi itakapotaka kufanya ununuzi wa vifaa vilivyotumika. Baada ya jukumu la kumshauri Waziri kukamilika, Kamati Maalum hiyo itakuwa imemaliza majukumu yake. Baada ya Waziri kutoa kibali, Taasisi ya Ununuzi itaendelea na taratibu za ununuzi kama itakavyoainishwa kwenye Sheria na Kanuni. Suala hili litaainishwa kwa kina katika Kanuni zitakazotungwa. Kutokana na maelekezo haya, Jedwali la Marekebisho kuhusu kifungu cha 66 limerekebishwa

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, wameelezea wasiwasi wao kuhusu suala la uadilifu katika ununuzi wa vifaa vilivyotumika. Ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, suala hilo litapewa msisitizo katika Kanuni ili masharti yanayopaswa kuzingatiwa na Taasisi ya Ununuzi kabla ya ununuzi kufanyika, yataainishwa kwa lengo kuhakikisha kuwa vifaa vitakavyonunuliwa vitakuwa na ubora unaokubalika. Kanuni hizo pia zitawezesha kudhibiti mianya ya matumizi mabaya ya fedha za umma. Baadhi ya masharti hayo ambayo yataainishwa katika Kanuni ni kama yafuatayo:-

(a) Kanuni za Ununuzi wa Umma, zitaweka masharti ya kuzitaka Taasisi za Ununuzi husika kwa ajili ya kutoa taarifa *PPRA* kabla ya kuanza mchakato wa ununuzi wa vifaa vilivyotumika. *PPRA* itafuatilia kwa karibu mchakato wa zabuni husika na iwapo itabaini ukiukwaji wa Sheria, Taratibu na Kanuni zilizowekwa, itasitisha mchakato wa zabuni hiyo kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifingu cha 19 cha Muswada huu.

(b) Ulinganifu wa gharama za ununuzi wa vifaa vilivyotumika na gharama za kukodi au kununua vifaa hivyo vikiwa vipya utafanyika kabla ya kufanyika uamuzi wa kununua vifaa husika.

(c) Mmiliki wa vifaa husika atapaswa kuwasilisha kumbukumbu za utunzaji, yaani *maintenance* na matengenezo yaliyofanyika.

(d) Vifaa vitakavyonunuliwa havitahusisha vifaa vilivyowahi kupata ajali.

(e) Umri wa vifaa vitakavyonunuliwa utabainishwa kulingana na aina ya vifaa ambapo uthibitisho wa umri husika utakuwa ni tarehe ya kutengenezwa.

(f) Mmiliki wa vifaa husika atapaswa kuwasilisha uthibitisho wa hali ya vifaa hivyo kutoka kwenye vyombo vinavyotambulika Kitaifa na Kimataifa kulingana na vifaa husika, yaani *certificate of worthiness from recognized national and international bodies.*

(g) Mtengenezaji wa vifaa husika, atawajibika kutoa uthibitisho kwamba ataweza kufanyia matengenezo vifaa hivyo katika kipindi kitakachokubalika kulingana na aina ya vifaa hivyo na upatikanaji wa vipuri.

(h) Timu ya wataalam waliobobea kutoka ndani na nje ya nchi itaundwa kwa ajili ya ukaguzi wa ubora wa vifaa husika vinavyohitajika kabla ya kupokea, yaani *pre-shipment inspection and destination inspection.*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali itakuwa makini katika kuhakikisha Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma, inazingatiwa katika suala zima la ununuzi wa vifaa vilivyotumika.

Mheshimiwa Spika, pili, utaratibu wa Madiwani kushiriki katika mchakato wa ununuzi; hoja ilikuwa Serikali ifafanue iwapo kifungu cha 31(3) cha Muswada kinawezesha kuwepo kwa mfumo katika Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma za Serikali za Mitaa, kuwawezesha Madiwani kusimamia masuala ya Ununuzi katika Halmashauri kupitia Kamati ya Fedha na Mipango kama ilivyoelezwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa ufafanuzi kwa Bunge lako Tukufu, kuhusu kifungu 31(3) cha Muswada. Kifungu hiki kimeelekeza kuwa uundwaji wa Bodi za Zabuni katika Halmashauri na uendeshaji wa shughuli katika Bodi hizo, ufafanuliwe chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa. Sheria hii katika kifungu cha 98 imempa Waziri wa TAMISEMI, mamlaka ya kutengeneza Kanuni za Uundaji na Uendeshaji wa Bodi za Zabuni kwenye Halmashauri. Kanuni hizi ambazo ni Tangazo la Serikali Namba 177 la Mwaka 2007, zimeainisha pamoja na mambo mengine, uundwaji wa Bodi za Zabuni, utaratibu wa kuendesha shughuli zake ikiwemo kuidhinisha zabuni na kusaini Mikataba ya Ununuzi. Hivyo basi, Waziri wa TAMISEMI kwa mamlaka aliyopewa chini ya kifungu 98 cha Sheria ya Fedha ya Serikali ya Mitaa, Sura 290, atatunga Kanuni kurekebisha Tangazo la Serikali Namba 177 la Mwaka 2007, kwa kuweka vifungu ambavyo vitawezesha Kamati ya Fedha na Mipango katika Halmashauri kushiriki katika kuidhinisha katika mikataba kabla haijasainiwa na Mwenyekiti wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa marekebisho ya Kanuni za *Local Government Authority Tender Boards*, yaani *Establishment and Proceedings* za Mwaka 2007, Tangazo la Serikali Namba 177, yanajumuisha nia ya Serikali ya kuwahusisha Waheshimiwa Madiwani katika kumshauri Mwenyekiti wao kabla hajasaini mikataba. Serikali inafanya marekebisho yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kifungu kipya cha 31(4) kimeongezwa ambacho kitamwezesha Waziri wa TAMISEMI kujumuisha ushiriki wa Madiwani katika kusimamia na kudhibiti masuala ya Ununuzi.

(b) Kifungu cha 60(4) kimeongezwa ambacho kinamtaka Afisa Masuuli kabla ya kuwaarifu wazabuni walioshiriki katika zabuni husika juu ya kusudio la kutoa zabuni kwa mzabuni aliyeshinda, kuwasilisha maamuzi ya Bodi ya Zabuni kwenye Kamati ya Halmashauri inayosimamia masuala ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kujiridhisha, yaani *scrutiny* kama Sheria na Taratibu zimefuatwa. Iwapo Kamati husika itabaini ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Ununuzi wa Umma kwenye zabuni husika, itasitisha zabuni hiyo mara moja na italipeleka suala hilo *PPRA* kwa ajili ya uchunguzi na ushauri.

Mheshimiwa Spika, tatu, Kifungu cha 101, Usuruhishi wa Migogoro ya Ununuzi. Suala hili linashughulikiwa katika kifungu cha O(o) cha Jedwali la Marekebisho, ambapo mzabuni ambaye hakuridhika na maamuzi ya *PPAA* ana haki ya kuomba mapitio ya Mahakama Kuu, yaani *Judicial Review* na pale ambapo Taasisi ya Ununuzi haikuridhika na uamuzi wa *PPAA*, Taasisi hiyo itakuwa na haki ya kuwasilisha maelezo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupinga uamuzi huo. Mwanasheria Mkuu amepewa Mamlaka ya kupitia maelezo ya Taasisi ya Ununuzi pamoja na maelezo ya *PPAA* na kuwasilisha suala hilo Mahakama Kuu kwa uamuzi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuelezea upungufu wa Sheria ya sasa, kifungu kwa kifungu na namna ambavyo upungufu huo umerekebishwa katika Muswada huu. Upungufu uliojitokeza katika Sheria ya Mwaka 2004 ni mwingi na ulijadiliwa na Wadau pamoja na Kamati.

Hata hivyo, baadhi ya upungufu huo umeleezwa katika hotuba yangu niliyoitoa wakati ninawasilisha Muswada. Baadhi ya maeneo yenye upungufu katika Sheria ya Mwaka 2004 ni pamoja na Sheria hiyo kutotoa uwezo wa *PPRA* kusitisha zabuni pale ambapo taratibu hazifuatwi na kuweka utaratibu wa kushughulikia malalamiko unaochukua muda mrefu kwa takriban siku 105. Muswada huu umepunguza muda huo hadi siku 59. Idara ya kusimamia Sera ya Ununuzi wa Umma haikuwepo katika Sheria ya Mwaka 2004. Aidha, viwango vya adhabu kutokana na ukiukwaji wa Sheria vimeongezwa kutoka faini ya shilingi laki tano katika Sheria ya Mwaka 2004 hadi shilingi milioni kumi au zaidi katika Sheria hii mpya.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu Sheria ya Mwaka 2004, ambayo inapendekezwa kufutwa, imetumika kwa miaka sita tu. Serikali itoe maelezo kuhusu hasara iliyopata kwa kutungwa Sheria ya Mwaka 2004 na kufutwa baada ya miaka sita tu. Marekebisho ya Sheria ni jambo la kawaida kwani baada ya Sheria kutumika, upungufu huweza kuonekana na hivyo kuhitaji marekebisho. Sheria ya Mwaka 2004 pamoja na marekebisho yanayopendekezwa sasa, bado ilikuwa na ufanisi katika kuweka misingi bora ya ununuzi wa umma. Lengo la markebisho haya ni kuifanya Sheria iweze kuleta ufanisi zaidi kwa kuzingatia mabadiliko ambayo yanaendelea kujitokeza katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu tafsiri ya neno *successful tender* lilekebishwe ili kuondoa maneno *lowest evaluated cost*. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tafsiri ya maneno *lowest evaluated cost* ni tofauti na maneno *lowest cost*. Tafsiri ya *lowest evaluated cost* inazingatia ubora, uwezo pamoja na bei, wakati *lowest cost* inahusu bei peke yake. Kwa upande wa uuzaji wa vifaa kwa ajili ya zabuni au ukusanyaji wa mapato, neno linalotumika ni *highest evaluated price,* ambalo limejumuishwa kwenye Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilihusu uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ufanywe na Bodi badala ya utaratibu wa sasa wa kuteuliwa na Rais. Serikali ina utaratibu wake wa kufanya uteuzi wa Viongozi katika ngazi mbalimbali, ambao unazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Wapo Viongozi wanaoteuliwa na Bodi, wapo wanaoteuliwa na Waziri mwenye dhamana na wapo wanaoteuliwa na Rais kutokana na uzito na dhamana ambayo taasisi husika imekabidhiwa ambapo *PPRA* ni mojawapo katika hizo taasisi zenye dhamana kubwa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma iwezeshwe kifedha na rasilimali watu. Vilevile *PPRA* na *PPAA* ziwe na bajeti zake zinazojitegemea. Tumepokea maoni ya Kamati na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na Serikali itayafanyia kazi. Hoja nyingine ilihusu Idara ya Usalama wa Taifa na Balozi zetu za Tanzania, zihusishwe katika kuhakikisha Serikali haiingii Mikataba na Makampuni hewa. Suala hili tayari limezingatiwa katika Muswada chini ya kifungu cha 53(3).

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu kifungu cha 65(3) kifutwe na kifungu cha 65(4) kirudishwe ili kuondoa uwezekano wa Afisa Masuuli kufanya maamuzi peke yake katika ununuzi wa dharura. Kifungu cha 65(3) kimefutwa kupitia Jedwali la Marekebisho. Aidha, kifungu cha 65(4) kimependekezwa kufutwa kupitia Jedwali la Marekebisho kwani kiliwekwa kwa lengo la kutekeleza kifungu kidogo cha tatu ambacho tayari kimefutwa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu itengwe asilimia katika Mikataba Mikubwa ambayo itasaidia kujenga uwezo wa vyombo vinavyohusika katika kusimamia ununuzi. Serikali inakubaliana na hoja hii. Kwa kuwa suala hili ni la kisera, Serikali italifanyia kazi. Hoja nyingine ilihusu uamuzi wa kutambua hali ya dharura ushirikishe Menejimenti au Bodi za Wakurugenzi badala ya Afisa Masuuli peke yake na apate kibali cha *PPRA.* Ushauri wa kushirikisha Menejimenti na Bodi za Wakurugenzi utazingatiwa. Hata hivyo, haitakuwa busara kwa *PPRA* kushiriki katika kutoa kibali, kwani kwa kufanya hivyo itakuwa imeshiriki mchakato wa zabuni na hivyo kukinzana na dhana ya udhibiti. Hoja nyingine ilihusu Sheria hii itungiwe Kanuni itakayoainisha jinsi ya kuwashughulikia watakaokiuka Sheria na jinsi Bunge litakavyoshirikishwa.

Mheshimiwa Spika, Muswada tayari una vifungu ambavyo vimeainisha hatua ambazo zitachukuliwa kwa wale watakaobainika kukiuka Sheria. Kwa mfano, vifungu vya 16, 20 na 104 vya Muswada, vimeweka hatua zitakazochukuliwa dhidi ya watendaji watakaokiuka Sheria. Vilevile

Kanuni zitatoa ufafanuzi zaidi kuhusu hatua zitakazochukuliwa kwa makosa mbalimbali. Aidha, Bunge litahusika kupitia Kamati zake za Kudumu ambazo ni Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma na Kamati ya Hesabu za Serikali wakati zinapitia Taarifa za Ukaguzi za *PPRA.*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu kifungu 50 cha Muswada, kinachohusu manunuzi ya *common use items and services,* kinaipa ukiritimba *GPSA*, hali inayoweza kuleta ucheleweshaji wa upatikanaji wa huduma. Kwa mujibu wa Muswada, *GPSA* hainunui vifaa na kuhodhi bali inateua wazabuni wa kutoa huduma kwa taasisi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu adhabu zitakazochukuliwa kwa watendaji watakaokiuka Sheria hii ambazo zimeainishwa katika Muswada huu na hazikuainishwa katika Sheria ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, adhabu zimeongezwa kupitia kifungu cha 104, kinachoainisha makosa na adhabu ambazo zimeongezeka. Kwa mafano; adhabu ya kifungo imeongezeka kutoka miaka mitatu hadi mitano, faini imeongezeka kutoka shilingi 500,000 hadi shilingi 10,000,000 au zaidi. Aidha, makosa ya adhabu yameongezeka kulinganisha na yale yaliyoko katika Sheria ya sasa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine; Serikali itoe tamko kuhusiana na taarifa zilizopo kwamba, kuna mabehewa yaliyotumika huko Japani yenye mionzi ya nyuklia ambayo Serikali ina mpango wa kuyanunua baada ya Muswada huu kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali haijapendekeza kifungu cha 66 cha Muswada kwa lengo la kuagiza mabehewa kutoka Japani. Ninapenda kusisitiza kwamba, kifungu cha 66 kimewekwa na Serikali kwa nia njema na kwa kuzingatia sasabu nilizozieleza katika hotuba yangu wakati ninawasilisha Muswada huu na kufafanuliwa zaidi katika maelezo yangu ya hotuba hii. Ninaomba kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge kama Viongozi, washirikiane na Serikali kuuelimisha umma ili usiyumbishwe na taarifa zisizo na ukweli.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu kuongeza orodha ya vifaa maalum vilivyotumika katika siku za usoni chini ya kifungu cha 66 cha Muswada. Serikali itazingatia ushauri uliotolewa kadiri ya mahitaji yatakavyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihusu kuweka kifungu kitakachozuia ununuzi wa vifaa na samani kama meza, viti na kadhalika kutoka nje ya nchi. Serikali inakubali na itazingatia ushauri uliotolewa. Utaratibu kuhusu ununuzi wa samani za ofisi katika Serikali, utaainishwa katika Kanuni zitakazotungwa baada ya Waheshimiwa Wabunge kupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao mizuri na yenye hekima na ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

***Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2011***
***(The Public Procurement Bill, 2011)***

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha pili, *subsection (1)* inapoanza: *"This Act shall apply*... lifuatiwe na neno *"to"*, kwamba; *This Act shall apply to... then* yaendelee yale maneno mengine... *all procurement and disposal* na pale chini... *non-government*, badala ya kuweka maneno tu kuanzia kwenye (a) na (b). Ukienda sehemu ya tatu itakataa (c) kama ukianza na ilivyoanza. Kwa hiyo, nilikuwa nimependekeza kwamba isomeke: *"This Act shall apply to ...then* zifuate (a), (b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilikuwa na masahihisho mengine hapa ambapo kuna *section* ya tatu nay a nne na nilikuwa nimependekeza kwamba, kwa sababu sasa manunuzi ya Jeshi yameingizwa kwenye sheria kwamba yasiwepo kwenye kifungu cha *application*; nikapendekeza tuanzishe kifungu kipya cha 57.

Waziri hajasema hivyo na bahati nzuri nina Kanuni za *Procurement* ambazo suala la Jeshi kununua limeelezwa vizuri sana ndani ya Kanuni. Sasa kama tunalileta kwenye sheria ni vizuri tukaanzisha kifungu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ngoja kidogo tukuelewe; ile ya kwanza ni kuhusu ibara ya (2); haya unayoeleza yanahusu ibara gani?

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ibara hiyo hiyo.

**MWENYEKITI:** Haya, tuendelee! Endelea na maelezo; Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ile ya kwanza *section 2(1)*, inaweza kuwepo kama alivyosema, sina matatizo na hiyo. Ingawa pia ungeweza kuhamisha ile (2) ukapeleka kwenye (c). Kwa uandishi mzuri, tuiweke ile (2) pale juu kwenye ile anayosema ya *Diffence, National Security*, maoni yetu, ya Serikali na maoni ya Kamati ni kwamba, yabaki kama yalivyo na utaratibu wa *procurement* kwenye vyombo vya kijeshi uwe kama ambavyo vifungu vya sheria hii vinasema huko mbele ya safari.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujua kama itabaki kama ilivyo maana yake kwenye kanuni tutaondoa? Nilitaka nijue hivyo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Mheshimiwa Zambi mwenyewe hakwenda kwenye Kamati kueleza msingi wa mapendekezo yake haya. Kama utakavyoona katika vifungu vinavyofuata, utaratibu wa *procurement* ndani ya jeshi umeelezwa kwenye vifungu *specific*. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba, vifungu *subsection (2)* mpaka *subsection (5)* vibaki kama vilivyo. Tutakapofika kwenye vifungu *specific* tutasema.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 3

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili, ninaishukuru Serikali imekubaliana pia na mapendekezo niliyokuwa nimeyaweka.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mnyika.

**MHE JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Katika eneo hili nilikuwa na mapendekezo mawili; ninashukuru kwamba, Serikali imeyakubali mapendekezo yote mawili. Ila ningependa kupata ufafanuzi kidogo ili niridhike na marekebisho ambayo Serikali imeyafanya kwenye tafsiri ya neno *specifications*, neno *services* halijajitokeza. Sasa, ningetaka kujua sababu ya kutojumuishwa kwa neno *services* kwenye tafsiri ya neno *specifications,* kwa sababu kwenye *further schedule of amendment* tuliyoipokea, inaeleza *specifications means a description of any commodity or works* ...na inaendelea.

Mwisho pale kwenye *line* ya nne kwenda mwisho kwenye tafsiri ya neno *specification*, kuna neno *commodity or works*. Kwa hiyo, ningependa kupata uhakika kutoka kwa upande wa Serikali kwa sababu wameichukua hiyo tafsiri wameiunganisha na kutengeneza hii tafsiri ambayo ni bora ila sioni neno *services* kama *commodity and works* inajumuisha moja kwa moja *services*. Ninataka uhakika, kama haifanyi hivyo basi kuongezwe neno *services* hapo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mnyika. *Services, specification* siyo *term of Act, specification* ni neno la Kiingereza. *Specification* unaitumia kwenye *commodities* na *works*. *Services,* kwa mfano, ufundishaji, sasa huwezi kufanya *specification* kwenye ufundishaji, ndiyo tofauti tu ndugu yangu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 9

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa wakati anajibu hoja, nimekubaliana naye.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na marekebisho yaliyofanywa na Serikali kwenye Jedwali la Kwanza, ambayo yame-*take into consideration* hoja ambayo nilikuwa ninaisema.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 16

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa napo ninaomba nishukuru kwamba, Serikali imezingatia msingi wa hoja niliyokuwa ninaisema na imefanya marekebisho kwenye nyongeza ya marekebisho ambayo yamezingatia suala ambalo nilikuwa ninataka lizingatiwe.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 17
*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 21
Ibara ya 22

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Ibara ya 23 inahusu uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Ununuzi *(PPRA)*. Ibara ya 23(1) inasema; *there shall be a Chief Executive of the Authority who shall be appointed by the President on such terms and condition as officer the President determines...* Hapa kulikuwa na marekebisho mawili ambayo niliyapendekeza. Marekebisho ya kwanza ni kuondoa haya maneno ambayo inaelekea yameingia kimakosa; *the officer of the President.* Marekebisho hayo Serikali imeyazingatia katika Jedwali la Kwanza.

Marekebisho ya pili ambayo Serikali haijayazingatia; Kambi ya Upinzani ilipendekeza kwamba, Afisa Mtendaji Mkuu ateuliwe na Bodi. Mimi kwenye Jedwali la Marekebisho nimependekeza kwamba, mamlaka haya ya Rais ya uteuzi nime-*recommend* hapa yaongezwe maneno kabla ya maneno *the President*, kwa maana kabla ya Rais kuteua, kuwe na maneno *upon recommendation of the Board of Directors,* yaani, kabla ya Rais kuteua, apate mapendekezo kutoka kwa Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, Mheshimiwa Waziri katika majumuisho ya hoja, ameizungumzia hii hoja na kueleza kwamba, katika uteuzi, Serikali inazingatia Sheria za Uteuzi wa Mashirika ya Umma na mambo mengine ambayo Waziri ameyaeleza. Maelezo haya mimi sikubaliani nayo kwa sababu wakati Bunge linapitisha Maazimio ya Ripoti ya Kamati Teule mwaka 2008 kuhusiana na Richmond, katika eneo hili la Sheria ya *Procurement*, Bunge liliazimia kwamba, Sheria ibadilishwe ili kuipa mamlaka zaidi hii Mamlaka ya Ununuzi. Sasa, katika mahali pa kuipa mamlaka, kwa kuwa Rais ameshapewa mamlaka haya kwa mujibu wa Sheria kuchagua Mwenyekiti wa Bodi; ni vizuri Bodi ikapewa mamlaka ya kuteua yule Mtendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda kwenye *middle ground*, siyo Bodi kuteua moja kwa moja bali Bodi kupendekeza ili misingi ya uteuzi itokane na mapendekezo ya Bodi ili Bodi iwe na mamlaka dhidi ya yule mtendaji. Tuna *experience* ya mashirika mengi na taasisi nyingi ambazo kitendo cha Mwenyekiti kuteuliwa na Rais na Mtendaji wa Bodi naye kuteuliwa na Rais, kimefanya Bodi iwe kama vile iko chini ya mtendaji ama iko sawa na mtendaji na kupoteza uhuru wa Bodi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningedhani kwamba, kwa *interest* ya kutekeleza yale Maazimio ya Bunge na kwa *interest* ya kufanya chombo hiki kifanye kazi kwa ufanisi, ni vizuri Serikali ikalikubali hili pendekezo la kuingiza haya maneno kwenye Sheria hiyo *upon recommendation of the Board* ili kabla ya Rais kuteua, yatoke mapendekezo kutoka kwenye Bodi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili lilijitokeza kwenye Kamati, tena tulilizungumza kwa kina. Utaratibu ulivyo sasa hivi, ndivyo hivyo ambavyo Mheshimiwa Mnyika anazungumza. Kabla Mtendaji Mkuu wa Shirika lolote la Umma hajateuliwa, Bodi ama huwa inatangaza au inatafuta utaratibu wowote ambao unafaa kuweza kumpata *Chief Executive Officer*, wanafanyiwa udahili. Mara nyingine wanafanya Kamati ya Bodi, mara nyingine udahili unafanywa na Shirika ambalo linateuliwa kufanya udahili huo. Baada ya hapo, inapeleka majina matano kwa Waziri mwenye dhamana wakipendekeza moja, mbili, mpaka tano ya jinsi ambavyo waliwadahili wale watu. Waziri kwa kushirikiana na *system* nyingine za Serikali, wanafanya kazi

nyingine na kupeleka majina matatu kwa Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais, anateua mmoja kati ya wale watu watatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo utaratibu uliopo sasa kwa mashirika yote ya umma. Kwa hiyo, tukasema kwa sababu mashirika yote ya umma yapo hivyo, hakuna sababu ya shirika moja tu tuwe na kipengele mahususi cha aina hiyo. Tunapendekeza kwamba, utaratibu ubaki jinsi ulivyo na uendelee hivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwani mkiandika inadhuru nini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Labda swali liwe kwamba tukiandika ina faida gani?

**MWENYEKITI:** Sawa yote mawili.

**WAZIRI WA FEDHA:** Pengine ni kwamba, tukiliandika hili lina faida gani, maana ndivyo linavyofanyika. Ukishamchukua Mkurugenzi Mtendaji wa *NDC* inafanyika hivyo, ukitaka kumtafuta hata Gavana wa Benki Kuu licha ya kwamba chombo kile ni *sensitive* kweli kweli, haisemi mahala, lakini uteuzi wake hata mimi ninahusika kama Waziri na unatoka kwenye Bodi.

**MWENYEKITI:** Ninasema kama inafanyika ukiandika itadhuru nini? *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo ukisema yakiandikwa hayana athari mojawapo ni hili. Tunachosema hapa ni kwamba, Rais atapelekewa jina la mtu mmoja na Bodi, halafu atamteua yule mtu. Bodi inaweza isiwe na uwezo wa kumfahamu vizuri, ndiyo maana utaratibu huo wa mchujo tunaona ni vizuri uendelee kama ilivyo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na hayo maelezo. Kwanza, maelezo yanajichanganya; Waziri amesema majina matano au matatu, Mwanasheria anasema linakwenda jina moja. Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitunga hii sheria kwa kadiri ilivyo …

**MWENYEKITI:** Hii ya Mwanasheria Mkuu hujamwelewa alivyosema anasema, tukitumia ushauri wako wewe kwamba Bodi inachagua, kwa hiyo huyu anapelekewa pengine jina moja tu, siyo kwamba ndivyo ilivyo, alikuwa anajaribu kufafanua utaratibu unaosema wewe. Sasa endelea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa ufafanuzi huo. Msingi wa *upon recommendation by the Board* haumaanishi kwamba lazima liwe jina moja, yanaweza yakawa matatu, manne na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda niseme kwamba, tukiipitisha hii sheria kama ilivyo, kwa maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, tunakwenda kutunga sheria ambayo inakinzana na sheria nyingine na kumekuwa na *trend* ya hayo maelekezo kukinzana na sheria. Hapa ninayo nukuu ya sheria aliyoi-*refer* Waziri ya *The Public Corporation Act, Cap. 257, 2002* pamoja na *amendments* zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *section* 13 inasema, nanukuu: "*Appointment of Chief Executive of Public Corporation…* Inaendelea: "The *Board of Directors shall with prior consent of the Minister responsible for the Parent Ministry, appoint Chief Executive of that Public Corporation,* tafsiri yake ni nini? Kwa Sheria tulizotunga za nchi hii, uteuzi wa Rais wa Watendaji Wakuu wa Bodi kwa sheria hii ni batili. Kwa sababu Sheria inasema Bodi ndiyo itakayoteua. Sasa ili tusiendelee kukiuka sheria *at least* twende kwenye *middle ground* kwa sababu tumekuwa tukikiuka Sheria kwa Wakurugenzi wa Halmashauri, tunakiuka sheria kwenye uteuzi wa Wakurugenzi wa Bodi, sasa ili tusiendelee kukiuka sheria, angalau Rais kabla ya *appointment* apate kisheria *recommendation* ya Bodi, la sivyo tutaendelea kukiuka hii sheria *forever*. Kwa sababu sheria imesema bayana uteuzi wa Maafisa Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma unafanywa na Bodi, siyo Rais kwa mujibu wa sheria hii.

**MWENYEKITI:** Haya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la Mheshimiwa Mnyika linaongeza *transparency* kwenye *public functions*, lakini unajua *Chief Executive of the Authority, that authority is not a public corporation*. Kwa hiyo, hiyo sheria unayoi-*site doesn't apply here* na bado tunafikiri kwamba ilivyo hapa ni sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*
Ibara ya 29

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuafikiwa kwa marekebisho kwenye Ibara ya 29, hoja yangu kimsingi Serikali imei-*take into consideration* kwenye *schedule* ya ziada kipengele kimojawapo kuhusiana na taarifa maalum za ukaguzi. Kwa hiyo, nashukuru.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 30

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 31, mwanzoni tulikuwa tunasema kwamba kwa sababu tunataka Madiwani wawe na maamuzi ya moja kwa moja na yaonekane kwenye sheria, mapendekezo ambayo nilikuwa nimeyatoa Serikali imekubaliana nayo, kwa hiyo, sina lingine, naishukuru Serikali.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na Serikali kukubaliana na mapendekezo ya Mheshimiwa Zambi pamoja na mimi ambayo tuliyatoa na kuingiza hiyo Ibara, ningependa bado kusisitiza umuhimu wa kuingiza haya maneno kwenye Ibara Ndogo ya (3) cha Ibara ya 31. Naomba nifanye *reference*; Ibara ya 31(3) inasema; "*The composition of the Local Government Authority tender board*…inaendelea; mwisho inasema: …*Regulations made pursuant to the provision of the Local Government Finances Act"*. Kwa Ibara ya (5) kilichoongezwa kimezingatia tu kuingizwa kwa Madiwani na Kamati za Fedha ambacho nakubaliana nacho na naunga mkono kabisa pendekezo la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna umuhimu bado kwenye Ibara ya tatu (3) mbele ya maneno *Local Government Finances Act,* kuongeza maneno niliyoyapendekeza hapo *or any other Local Government Written Law*. Kwa sababu uendeshaji wa Halmashauri hauzingatii tu peke yake Kanuni zinazotungwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha, unazingatia vile vile Kanuni zingine zinazotungwa kwa mujibu wa sheria nyinginezo za Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna masuala ya ununuzi na uuzaji wa mali za Halmashauri ambayo yamekuwa *referred* kwenye sheria nyingine, kwa hiyo tukifunga hapa kwamba Kanuni atakazotengeneza Waziri zitatokana tu na Sheria ya Fedha peke yake bila kuzingatia sheria

zingine kuna fursa itakosekana wakati wa utengenezaji wa Kanuni, hususan kuhusiana na mamlaka ya Kamati za Fedha na Mipango kwa Halmashauri za Vijijini na mamlaka ya Kamati ya Fedha na Uongozi kwa Manispaa kama ya kwetu ya Kinondoni katika utendaji kazi kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, ningeshauri haya maneno, *Provisions of Local Government Finances Act,* kuongezwe maneno yanayosema *"and or any other Local Government Written Law"* kwa maana ya ama sheria nyingine yoyote ya Serikali za Mitaa yazingatiwe.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SHERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mbunge wa Kinondoni...

**MWENYEKITI:** Ubungo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** *Ooh! sorry*, Ubungo.

**MWENYEKITI:** Halmashauri ya Kinondoni. (*Kicheko*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi siyo Diwani, lakini nafahamu kwamba *practice* ya maeneo yetu yanatofautiana kutoka Ismani mpaka Ubungo, ni tofauti kabisa. Sasa hatuwezi kutunga sheria ambayo itakidhi matakwa ya kila Halmashauri. Lakini tulichofanya kwa kuzingatia haya ambayo anazungumza Mheshimiwa Mnyika, tumeongeza Ibara nyingine ya Nne (4) ambacho kinasema kwenye *further schedule of amendments* ukurasa wa pili, ambacho tunafikiria kwamba kina-*take into account* haya ambayo ameyazungumza Mheshimiwa Mnyika. Kwamba "*The Regulations made pursuant to subsection* (3), hii ambayo ameisoma Mheshimiwa Mnyika, *shall, inter alia, provide for the procedure under which a Local Government Authority through its committee responsible for finance and planning shall perfom its oversight function on public procurement matters."* Kwa hiyo, tunafikiri kwamba hii ita-*take into account* mazingira tofauti katika Halmashauri zetu. Lakini ile ambayo tunazungumza, *actually* tunazungumzia Sheria ya *Local Government Finances Act, Chapter* 290 ambayo ni *uniform* kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri nimeeleweka, ahsante sana.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa *uniformity* na pendekezo nililopendekeza hapa siyo la Kinondoni wala siyo la Ubungo, ni la nchi nzima. Kwamba Waziri katika kutunga Kanuni, kwa sasa sheria ilivyo tukiipitisha kama ilivyo inasema, Waziri atatengeneza Kanuni kwa kuzingatia sheria ya fedha za Serikali za Mitaa basi. Ninachopendekeza baada ya maneno haya kuongezwe maneno ambayo nimeyasema kwa Kiingereza sasa niyaseme kwa Kiswahili; "ama Sheria nyingine zozote za Serikali za Mitaa". Kwa sababu kwenye *discourse* ya Serikali za Mitaa ukiondoa Sheria ya Fedha, mjini sisi tuna *Urban Authorities Act, Local Government Act*, Vijijini huko wana sheria nyingine za *Rural* na kadhalika zina taratibu zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Waziri azizingatie hizo taratibu zote za nchi nzima, wakati anatengeneza kanuni asiitazame Sheria ya Fedha peke yake atazame na sheria nyingine. Hili jambo lina msingi wake kwa sababu sheria ya fedha Ibara ya 68 nimesoma sheria yote. Kifungu 68 cha Sheria ya Fedha ambacho ndiyo sasa Waziri anakitumia kutengeneza Kanuni za ununuzi hakijaelezea masuala ya ununuzi, kinaelezea masuala ya makusanyo ya mapato, matumizi na mambo mengine. Sasa kwa sababu manunuzi yapo kwenye sheria nyingine ikiwemo uuzaji wa mali za Halmashauri na nini, turuhusu Waziri wakati anatengeneza kanuni atumie vile vile sheria nyingine, ndiyo msingi wa pendekezo langu ambalo lipo *obvious* sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ku-*commit* hiki walichosema wenzio kwamba hawakatai mapendekezo yako, isipokuwa yamekuwa *relevant* kwa haya mabadiliko uliyofanya, mbona hu-*comment* kwa haya waliyofanya wao, unge-*comment* haya kwamba yana upungufu gani ukilinganisha na unayosema.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe taarifa tu ili ikusaidie kwenye kufanya maamuzi.

**MWENYEKITI:** Sasa tusome hiki walichopendekeza.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ibara inayoongezwa inahusu jambo moja tu, Ibara ya tano, inahusu mamlaka ya Madiwani kupitia Kamati za Fedha na Uongozi ama Kamati za Fedha na Mipango, kusimamia mchakato wa tenda baada ya Bodi ya Zabuni kumaliza kazi yake. Ibara tunayoizungumzia hapa *subsection* (3) inahusu *procedure* za uundaji wa Bodi ya Zabuni na namna ambavyo Bodi ya Zabuni itafanya kazi ndiyo Ibara inayohusika hapa. Sasa katika *procedure* hizi za uundaji wa Bodi ya Zabuni na namna ambavyo Bodi ya Zabuni itafanya kazi, ninachokisema ni kwamba, jambo hili haliongozwi kwa Sheria ya Fedha peke yake, kwa sababu *section* 68 ambayo Waziri anaitumia kutengenezea Kanuni, haina vitu vingi ambavyo vingine viko kwenye Halmashauri zetu, kwenye sheria zingine iwe ni mjini au ni kijijini. Kwa hiyo, yakiongezwa hayo maneno kutafanya wakati Waziri anatengeneza hizi Kanuni azi-*consult* sheria nyingine katika maeneo ambayo yanamtaka kutengeneza kanuni *related* kwa jukumu hili ambalo anakwenda kulifanya, ndiyo msingi wa hili pendekezo. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri kwamba tusome sheria kwa vifungu vyote, kwa sababu ukienda mbele Ibara ya 60 ambayo imefanyiwa marekebisho mara mbili, ilikuwepo kwenye *schedule* ya kwanza, lakini kwenye *schedule* ya pili ukurasa wa pili, ukisoma maudhui yale ambayo yapo kwenye Ibara ya 31 pamoja na *amendment* tuliyofanya kwenye kifungu kipya cha Nne ambayo nimeisoma, nikasoma na ile Ibara ya 60 unaona kwamba hakuna haja ya kuongeza haya maneno ya *"any other law"* kwa sababu ukiongeza *any other law* pale haikusaidii lolote, na ukisema kwamba kama haiharibu kitu, basi tuiweke, huo siyo uandishi mzuri wa sheria na tutakuwa tunawanyong'onyeza wale watalaam wetu wa kuandika sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha msingi hii sheria siyo mwisho na wala siyo muarobaini wa kila kitu, tutakapomaliza hapa ni lazima pia tutembelee sheria ya *Local Government Finances Act*, pamoja na hizo sheria za *Local Government* kwa ajili ya kuingiza mambo ambayo yataoana na sheria hii. Kwa hiyo, nafikiri kwamba Mheshimiwa Mnyika ungekubali kwamba tupitishe halafu baadaye sasa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikia na *Local Government* ipitie hii sheria ya *Local Government Finance Act* pamoja na sheria nyingine ili tu-*harmonise position* ya sheria hii na hizo sheria. Nafikiri ndiyo itakuwa njia nzuri zaidi na mawazo yako ni mawazo mazuri lakini kwenye sheria zile ambazo ni za *Local Government*.

**MWENYEKITI:** Ibara hii…aah samahani kuna Mheshimiwa Mpina naye alileta *amendment, I forgot you*. Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Vile vile nami niungane na wenzangu kuishukuru sana Serikali kwa kukubaliana na utaratibu huu wa kuwahusisha Waheshimiwa Madiwani katika kusimamia shughuli za manunuzi kabla hazijafikia hatua zaidi, ni kitendo ambacho hata Waheshimiwa Madiwani nchi nzima wamekipongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninachokisema ni kwamba, kama ilivyoletwa katika marekebisho na Waziri wa Fedha na kama ilivyopendekezwa pia na Mheshimiwa Zambi, kwanza katika yale marekebisho yangu, pale kwenye *public procurement* imeandikwa *regulations* irekebishwe pale isomeke *regulatory*. Baada ya marekebisho hayo nataka niwataarifu Waheshimiwa Wabunge, nimtaarifu Waziri wa Fedha kwamba kwa jinsi ilivyorekebishwa hapa ni kama hakuna marekebisho yoyote kwa sababu *oversight function* waliyokuwa wanaifanya Waheshimiwa Madiwani siyo kwamba haikuwepo kabisa, Madiwani walikuwa wana-*perfom* ile *oversight function* lakini tatizo ilikuwa ni *timing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaletewa taarifa ya mchakato mzima wa manunuzi mkataba ukiwa umeshasainiwa, ujenzi ukiwa tayari unaendelea na pengine umeshamalizika, kwa sababu sheria iliyokuwepo bado ilikuwa inawataka bodi pamoja na kufanya hizo *awarding* zao na nini,

lakini walikuwa wanalazimika wapeleke taarifa ya utoaji tenda kwenye Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango ndivyo ilivyokuwa.

Sasa katika hili pendekezo langu....

**MWENYEKITI:** Wewe unapendekeza nini?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Ndiyo maana katika pendekezo langu nakubaliana na maelezo yote mpaka pale ambapo, kwanza nisahihishe kwa kusema kwamba, ilipoandikwa *Finance and Planning* siyo *Finance and Planning,* Kamati ile inaitwa *Finance, Admnistration and Planning,* yaongezwe maneno pale baada ya kuanza na yale maneno ya "*The regulations made pursuant to subsection (3) shall, inter alia, provide the procedure under which a Local Government Authority through its committee responsible for finance, administration and planning shall perfom its oversight function before the signing of any contract; and the Public Procurement Regulatory Authorithy (PPRA) to be consulted before any further process of signing of the contract in the event of the dissatisfaction by the Finance, Administration and Planning Committee of the intended award.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nipendekeze ili ku-*cupture* kabisa lengo la Kamati ya Fedha na ku-*capture* mazungumzo tuliyokubaliana na Waziri wa Fedha pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Fedha, kwamba *immediately* kabla Mkurugenzi wa Halmashauri na Mwenyekiti wa Halmashauri hawajasaini mkataba wapeleke taarifa hiyo kwenye Kamati ya Fedha na kama kutatokea kutokuelewana ile *Board* ikaendelea kusimamia tulivyo-*award* ni sahihi na *procedure* tumezifuata na Kamati ya Fedha na yenyewe ikasema kwamba sisi hatujaridhika na *process* zote zilizofuatwa. Sasa unakwenda kwenye Ibara ya 9(1)(a) ambacho ikitokea hali ya namna ile *PPRA* ina-*intervene*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hiki cha kwangu kichukuliwe kwa sababu ndiyo hasa kime-*focus* kwenye *point* yenyewe. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, bahati nzuri sasa tunatunga sheria, ni maneno gani unaongeza na yapi unayatoa, kwa sababu hapa umetuhutubia wenzio. Wewe unataka tutoe nini na tuingize nini.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nimesema ...

**MWENYEKITI:** *Refer* vizuri, *paragraph* gani iliyopo hapa na ni mstari gani unaozungumzia wewe.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Kwa sababu hii imekuja kwenye *schedule of amendment...*

**MWENYEKITI:** *Amendment?*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Eee! Kwa sababu kule kwenye sheria haipo hii Ibara, ipo kwenye *schedule of amendment* ya Waziri wa Fedha. Pale kuna kitu kimeandikwa *public procurement matters*, ndiyo hicho ninachokisema kwamba, hilo suala lilikuwepo, lakini nilichokiongeza ni maneno haya yaondolewe, yale ya *Public Procurement matters* yawekwe yale maneno yangu yanayosema "*oversight function before a signing of any contract."* Kwa hiyo, ile *oversight function* ifanyike wakati gani, ndiyo tatizo hasa lililokuwa kubwa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya, jina la Kamati kwa sababu ya *purpose* ya hii, huhitaji kama inavyoitwa kule kwa sababu tunayozingatia ni *the function of finance*, kwa hiyo usiite jina la mtu yeyote wakati *functions* zingine unaweza ukabadilisha, ndiyo maana tunasema Kamati ya Fedha kwa sababu hii tunazungumzia mambo ya fedha siyo *administration* au kitu kama hicho. Mwanasheria Mkuu!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe taarifa tu kwamba, maoni mazuri ya Mheshimiwa Mpina Mbunge wa Kisesa yamezingatiwa kwenye mabadiliko yetu,

Ibara ya 60, *second schedule of amendment,* ukurasa wa pili. (4) inasema "*subject to subsection (3) the Accounting Officer of a Local Government Authority shall, before issuing a notice of intention to award a contract, submit the award decision to the Committee responsible for Finance and Planning, for scrutiny, and where the committee is dissatisfied with the decision of the tender board, it shall request the Authority to conduct an investigation pursuant to section 33(3)".* Kwa maana kwamba kama mamlaka hiyo imetoa *tender* na mtu ameshinda kabla ya kumjulisha kwamba bwana umeshinda, ile Kamati inapeleka suala hilo kwenye Kamati ya *Finance and Planning* ya Halmashauri. Sasa wakiona kwamba kuna mizengwe au kuna kuchakachukua kwa lugha ya kisasa, basi wataiomba mamlaka hii iingilie kati kabla yule mtu mwingine aliyeshinda ile *tender* hajajulishwa, ndivyo inavyozungumzwa, nafikiri tumeikamilisha kwa njia hiyo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru mno.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 32

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33
Ibara ya 34

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 35

*(Ibara iliyotajwa hapo juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 36

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho)*

Ibara ya 37
Ibara ya 38

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 39

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 45
Ibara ya 46

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 47

*(Ibara iliyotajwa hapo juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 48

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 49

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru katika ile ibara ya 49 nimependekeza kwamba katikati ya maneno *its annual* iongezeke neno *detailed*. Kuongezeka kwa neno hili *detailed* maana yake umuhimu wake kwamba huu mpango wa manunuzi siyo kwamba hatukuwa nao lakini kwa jinsi ulivyokuwa ukithaminiwa na kwa jinsi ulivyokuwa ukitumika si hivyo ilivyokuwa inatarajiwa iwe. Sasa neno *detailed* litaongeza uthamani wa hii *annual procurement plan* kwa maana huu mpango wa manunuzi utawezeshwa kuletwa ukiwa na vielelezo vya kutosha na kuwawezesha wasimamizi wote iwe Kamati za Serikali za Mitaa, iwe Bodi za Mashirika ya Umma na iwe Kamati za Kibunge kuwawezesha kufuatilia mchakato mzima wa manunuzi ulivyoanza, utawezesha kuwalazimisha watendaji kuhakikisha kwamba, mpango wa manunuzi unapowasilishwa uwe umekamilika kwa maana ya kwamba, kama ni ujenzi utakuwa na michoro, utakuwa na *BoQs*, utakuwa umeeleza njia inayotumika katika manunuzi ya shughuli hiyo husika. Kwa hiyo, naomba sasa hili neno *detailed* wewe mwenyewe Mwenyekiti ni mhasibu unajua lina thamani kubwa sana kihasibu likiongezwa pale.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu pia kwamba wako wahasibu wengi pamoja na wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, hili neno *detailed* ni kisifa, bahati mbaya Mheshimiwa Kahigi hayupo hapa mwalimu wa Kiswahili, ni kisifa ambacho kina-*qualify*, yaani kinawekea sifa *annual procurement plan.* Sasa wewe unaweza kusema ni *detail* mwingine anaweza kusema *detail and correct* na mwingine anasema maneno mengine. Kinachozungumzia ni *annual procurement plan*. Kama siyo *detailed is not an annual plan*. Kwa hiyo, nafikiri kwamba neno detailed halina sababu ya kuingizwa pale. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Kwa maneno mengine ni kwamba, tunatunga sheria, sasa tukianza kui-*describe* kabisa ile sheria kwa namna hiyo, kwa sababu *procurement plan* zina sifa fulani, ikikosa sifa hizo siyo *plan*.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Nilishafanya *ruling* kwa sababu naona ni kitu kidogo sana, kwa hiyo, tusitumie muda mwingi.

Ibara ya 50

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natatizwa na kwenye Ibara ya 50 *framework agreements*. Kwa sababu kwenye sheria tumesema tunaanzisha pia PMU *user* ambazo tunataka tuzi-*staff* na wafanyakazi ambao wana sifa na vyovyote vile ambao wakiangalia watakuwa na maadili. Lakini sasa tukifanya hivyo majukumu yote ya *procurement* hata kama ni *common used items* zote tunazipeleka kwenye *GPSA,* nafikiri si sahihi sana. Kwa hiyo, nimeleta marekebisho yale kwenye Ibara ya 50 na sina sababu ya kuyasoma kwa sababu wote tunayo. Pamoja na kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali anasema sikuingia kwenye Kamati lakini niseme kwamba nilikuwa na majukumu mengine na Mwenyekiti wa Kamati nilikuwa nimemuarifu. Lakini pale ambapo nafikiri ni vizuri sheria ibadilike, nadhani nina wajibu wa kusema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali isilazimishe kwamba *common used items* zote lazima ziende kwenye *framework agreements*. *PMU user* kama nilivyoandika pale ziwe pia na mamlaka ya ku-*procure* kwa sababu wakati mwingine imeonekana bidhaa ambazo kwenye *framework agreements* hawa *tenders* ambao wamepewa zinakuwa na bei kubwa zaidi kuliko ukienda kwenye uhalisia wenyewe. Kwa hiyo, *GPSA* kwa maana ya kutoa *list* ya bei chini ya utaratibu huu tumeziingizia hasara kwenye kuzigharamia bidhaa ambazo kama PMU zingeifanya katika maeneo hayo sisi tungekuwa tumepata faida kubwa zaidi. Kwa hiyo, napendekeza maoni niliyoyatoa pale kama Serikali itaona inaridhia, basi iyachukue.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mawazo ya Mheshimiwa Zambi ukisoma ibara ya 50 pamoja na marekebisho tuliyofanya yanakwenda pale pale. Ile *version* yake tuliyoisoma tumeona kwamba haturidhiki nayo. Tunashauri Mheshimiwa Zambi akubaliane na mabadiliko yaliyoko kwenye Ibara ya 50 yaliyoletwa na Serikali kama yanakidhi hicho anachokizungumza. Ahsante.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana Mwanasheria Mkuu wa Serikali yuko sahihi lakini bado ziko hoja kwamba inatokea zile bei ambazo ziko chini ya utaratibu wa *framework agreements* ni kubwa zaidi kuliko maduka mengine ambayo labda hayajawa *identified* na *GPSA* hata kama ni huko huko. Sasa kwa nini tusingezipa mamlaka ambazo ziko kule zione bei ambazo zimetolewa chini ya utaratibu wa *framework agreement* ni kubwa zaidi, basi *PMU use* katika maeneo ziwe na uhuru wa kwenda katika maduka ambayo hayatambuliwi na mamlaka hii. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina matatizo na mapendekezo ya Mheshimiwa Zambi, tunayakubali.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni suala la kisheria, Waziri akisema haina matatizo maana yake nini na hapa tunatunga sheria.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana hamna matatizo kwa maelezo, lakini kwa Ibara ilivyoandikwa hapa yapo matatizo. Ukisoma ile Ibara ya 50.

**MWENYEKITI:** Kama ilivyo kwenye Sheria.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kama ilivyo kwenye sheria. Sasa pamoja na marekebisho yaliyoletwa na Serikali na yale ambayo pia yamekuwa *accommodated* kwenye maoni ya Mheshimiwa John Mnyika, tunaona kwamba, hivi ilivyo inatosha ndivyo tunachosema. Sasa kama Mheshimiwa Waziri anasema haina matatizo hilo ni jambo ambalo ni la baadaye. Lakini kwa Ibara ya 50 ilivyo sasa pamoja na marekebisho tuliyofanya, tunashauri kwamba huo ndio uwe msimamo na namshauri Mheshimiwa Zambi akubali tuendelee na kama atakuwa na wasiwasi sheria inaweza kurekebishwa wakati wowote tuendelee kuzungumza huu siyo mwisho wa kutunga sheria tutayafikiria hayo mawazo kwa uzuri zaidi baadaye. Ahsante.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mapendekezo ya marekebisho ya aina mbili kwenye hiyo Ibara. Rekebisho la kwanza, ni kuingiza neno *services* kwa sababu Ibara ya 50(2) kilikuwa kinasema *common used items,* kwa hiyo hakukuwa na *services* kwa maana ilikuwa ni *goods* peke yake. Nashukuru kwamba, Serikali imekubali kuingiza neno *services*.

Pendekezo la pili lilikuwa ni kuongeza neno *arrangement* kabla ya *framework agreements*. Kwa sababu *internationally* kwenye masuala ya *procurement* unapoweka hizi *framework agreement* nyingine zina sura ya *contracts*, wakati mwingine unataka uhuru wa manunuzi ambayo ndio dhana ambayo Mheshimiwa Zambi alikuwa akiizungumza kwenye kuzipa nafasi *PMU*. Kwa hiyo, kuweka neno *arrangement* inge-*provide* kwamba kuna fursa ya kuendelea kutumika. Serikali imeleta marekebisho kwenye hili jedwali la nyongeza, wamepanua wigo wa neno *agreement* kwa kuongeza maneno *closed of open framework agreement means an agreement with specified terms and conditions with or without agreed price respectively.* Kwa hiyo, maana yake wamekubali kuongeza dhana ya kwamba kuna *agreement* nyingine zitakuwa zimejifunga, zinaweza zikawa na bei na kadhalika na mipaka, kuna *agreement* nyingine zinaweza zikawa *open* kwa maana zinaweza zisiwe na bei na kadhalika.

Sasa ili niweze kuridhika kama kweli hii dhana mpya ya kuweka tafsiri ya *open and close agreement* imebeba ile hoja ya *arrangment* ningependa kupata ufafanuzi sasa hivi Serikali za Mitaa au Halmashauri zinalalamika kwamba mamlaka ya ununuzi yametoka kabisa kwenye Halmashauri kwa kiwango kikubwa sana yamerudi kwenye Serikali Kuu kupitia Wakala wa Ununuzi wa Serikali *GPSA*. Sasa ningetaka *clarity* tu hapa kwa maana ya hii tafsiri ya *open agreement* je, inamaanisha kwamba kwa upande wa Halmashauri hata kama ni *items* ambazo ni *common used*

kwa nadharia ile ile ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya upelekaji wa madaraka Mikoani, zitafanya *procurement* hazitaingiliwa na Serikali Kuu kwa kiwango kikubwa? Napenda kupata *clarity* hapo, la sivyo itabidi ile dhana ya *arrangement* iwepo ili kuweza kupanua wigo na kuruhusu Halmashauri kuweza kuwa na hiyo fursa. (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutafsiri uandishi wa sheria ulivyo ndivyo anavyosema Mheshimiwa Mnyika kwamba, sasa Halmashauri zinapewa mamlaka hayo, ndivyo ninavyotafsiri hiyo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53
Ibara ya 54
Ibara ya 55

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 56

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 57

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pale mwanzo nilikuwa nimesema Ibara ambayo kinahusu manunuzi ya jeshi ambacho kiko kwenye *application* kiondoke na tukianzishie *clause* mpya lakini *AG* alisema tusubiri tutakwenda mbele. Msingi wa mapendekezo yangu ni kwamba, hapa ambapo kimewekwa sasa hivi kwenye sheria ni sehemu ya *application*. Kwa hiyo, napendekeza, badala ya *procedure* yote inayohusu manunuzi kwenye jeshi kuwa kwenye sehemu ya *application,* tutaje tu kwamba, sheria hii ita-*apply* katika taasisi za Serikali lakini pia na katika jeshi, lakini zile *details* au *procedures* ziwe ndani ya sheria na hivyo ndivyo mapendekezo yangu yalivyo nikapendekeza Ibara mpya ya 57.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mapendekezo yangu yalizingatia kanuni za *procurement* ambazo ukienda ukurasa 114 wa *regulations* zimetajwa shughuli hizi za *procurement* chini ya jeshi. Kwa hiyo, nikasema vifungu hivi kwa sababu vimetajwa vizuri ndani ya kanuni na sasa tunavihamishia kwenye sheria visiwe kwenye *application*, tuvianzishie kifungu kipya sioni kama kuna ubaya wa hilo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuona hakuna ubaya. Lakini ukifikiria utaona kwamba unajivua nguo kwa mambo ambayo pengine tunavyofanya ndivyo inavyostahili. Ninavyofahamu Kamati ilikataa mapendekezo hayo kwamba, hivi vifaa vya jeshi viwe na utaratibu ule ambao uko kwenye *application*. Tusifanye vitu ambavyo kama vile tunajenga Mbingu duniani kwa sababu tunaweza kupata maadui zetu na wakatujua tukoje kwa kusoma sheria zetu. Kwa hiyo, nafikiri, ni vizuri utaratibu huu uwe kwenye *application provisions* kama ilivyo kwenye Ibara ya pili.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, katika marekebisho ambayo nimeyaleta hakuna kipya ambacho nimekiandika kwamba kinaingia, *argument* yangu ni kwamba Ibara ya (3) na cha (4) ndivyo vihame vianzishe *clause* mpya sijasema tu-*disclose* yale mambo mengine ambayo ni *restricted* chini ya utaratibu wa ununuzi wa jeshi. Nilichokuwa nasema pale, kwenye *application* kuwe na kifungu kitakachosema *procurement and disposable by tender by Defence and National Security Organs* ndio ibaki tu kwenye *application* lakini Ibara ya (3) na cha (4) ndivyo vi-*move* sasa vianzishe *clause* mpya ya 57. Hiyo ndiyo *argument* yangu wala sisemi kwamba tunatoa *details* nyingine upya.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kama ndivyo katika hali ya utunzaji wa sheria sioni kwa nini kihame kwenye sehemu ya kwanza kwa sababu hapa ni kama vile unabadilisha kiatu cha kushoto kwenda mguu wa kulia na haina mantiki yoyote kabisa. Kwa hiyo, nafikiri kwamba Mheshimiwa Zambi akubali tu kwamba ilivyo kwenye *application there is no harm*. Unaweza kuhamisha kifungu chochote kwenda mahali popote, lakini sisi ndivyo tulivyosema kwenye utangulizi kwamba mambo haya ya *Defence* yakae pale hata yakiingia pale kwenye *body, it does not make any difference*. Lakini kwa sasa tunafikiri yabaki kama yalivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika unasemaje kwenye Ibara hii kipya?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mapendekezo kwenye Ibara hiyo *unless* kama tumehamia Ibara ya 57.

*(Ibara Mpya iliyopendekezwa na Mheshimiwa Zambi ilikataliwa na Kamati ya Bunge Zima)*

Ibara ya Awali ya 57

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zambi kuna lingine katika Ibara ya 57?

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Hakuna.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa lugha ya Kiswahili kuzingatiwa kwenye masuala hayo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 58
Ibara ya 59

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 60
Ibara ya 61
Ibara ya 62

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 63

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 64

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 65

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nilikuwa nimependekeza marekebisho kwenye hiki Ibara inayohusu manunuzi ya dharura na mapendekezo ambayo nilikuwa nimeyapendekeza ni mawili. La kwanza, ni kufutwa kwa Ibara ya (3) ambayo inaruhusu Mamlaka ya manunuzi kununua mtambo wowote chakavu ama iliyotumika, mashine yoyote iliyotumika ama mtambo wowote uliotumika kwa masharti ambayo yameelezwa. Kwa hiyo, Ibara hii nilipendekeza ifutwe kwa sababu inatoa mwanya mpana sana wa manunuzi ya vitu vilivyotumika. Sasa nashukuru kwamba Ibara hii Serikali kwenye *schedule of amendment* imeifuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la pili lilikuwa ni la kuweka mipaka kwa uamuzi unaofanywa na Afisa Masuhuli, *Accounting Officer* ambao uko kwenye Ibara ya 65(1) kinasema;

*the emergency procurement may be made where the Accounting Officer determines that it is in the public interest that the goods, works and services be procured as a matter of urgency.*

Hii Ibara kwa tafsiri imetoa mamlaka makubwa sana ya Afisa Masuhuli kuamua moja maslahi ya umma ni yapi na maslahi ya umma anayoyaona kuwa ni ya haraka yeye Afisa Masuhuli. Sasa Afisa Masuhuli kama ni kwenye Wizara ni Katibu wa Wizara kama ni kwenye Halmashauri ni Mkurugenzi na kuendelea. Sasa nikawa nimependeza kuongezwe maneno kwa sababu haya matumizi ya dharura ni *sensitive* sana, ni nyeti, kuwekwe maneno kabla yatakayofanya aweze kuwa na chombo fulani ambacho ana-*consult* nacho kwanza. Kwa hiyo, nikaweka kwamba *upon consultation with the Tender Board.* Sasa hili jambo ni vizuri likapata mjadala mpana kidogo kwa sababu mapendekezo ambayo Serikali imeyaleta kwenye *amendment* yana hatari zaidi. Kwa sababu Serikali kwenye *amendment* iliyoileta wanakusudia kipengele cha (4) cha Ibara hiyo ya 65 ifutwe, Ibara hii inasema *upon satisfying the provision of subsection (3)...*

**MWENYEKTIKI:** Ngoja kwanza.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuja hapo kwa sababu najengea hoja kwenye ile hoja yangu ya kwanza ya *Tender Board*.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo umefuta ile ya kwako, sasa unajadili hii ya Serikali?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *no,* kwa sababu na hii nayo nina mapendekezo, nimependekeza kwenye eneo hilo vile vile katika hiyo Ibara husika.

**MWENYEKITI:** Haya.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema, hicho Ibara inasema, hiyo ninayoitafuta inayosema *procuring entity shall seek approval of the cabinet* na kadhalika. Sasa nilishauri badala ya *cabinet* kuwe *Government Procuring Services Agency,* nikashauri kuwe na neno *agency*, sasa uamuzi wa Serikali kuleta *schedule* ambayo haijakubaliana na hilo pendekezo la kuweka *agency,* lakini imeiondoa *cabinet* bila kuweka mbadala wa *cabinet* tafsiri yake ni kwamba, kwa sheria hii ikipata na mapendekezo yaliyopendekezwa na Serikali, huyu mamlaka ya ununuzi huyu *Accounting Officer* ataamua yeye, yapi ni maslahi ya Taifa ya dharura na ya haraka na atanunua na hakuna chombo cha juu yake cha kuidhinisha wala hakuna chombo cha ku-*consult* jambo ambalo ni hatari, tena hatari sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge na kwa msingi huo, marekebisho tuliyofanya sisi ni kukifuta Ibara Ndogo ya (3) cha Ibara ya 65(a), (b) na Ibara ya (4) na tukabakiza vifungu vile vya (5) ambavyo sasa vinaandikwa upya kama tunavyoonesha na tunafanya hivyo kwa sababu sio kwamba Mamlaka yale yanaachwa kwa *procuring entity* au *procuring person* kwa sababu bado *Authority* kwa mujibu wa sheria hii bado inayo nafasi ya ku-*check.* Kwa sababu tunachozungumzia hapa *essentially* ni *process* ya *cheques and balances* na tunafikiri kwamba ilivyo sasa hiyo *process* ni nzuri zaidi kuliko vile ambavyo tulikuwa tumesema kwamba ni *cabinet.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nimelisema nilirudie tu kwa maneno rahisi sana. Kama umeshampa mamlaka *Accounting Officer* kwa *provision* 65(1) kwa kufanya manunuzi ya dharura kwa kuangalia mambo aliyoyaona yeye ni maslahi ya Taifa na ya haraka. Halafu umefuta kipengele cha (4) cha Ibara hiyo, ambayo ilikuwa imeweka chombo cha juu yake cha kuidhinisha kwamba hayo aliyoyaamua yako sawa, kwa hiyo umeacha utupu. Nakubaliana kabisa na *logic* ya kuiondoa *cabinet* kwa sababu ukiondoa *cabinet* maana yake

unamwondoa Rais *which is okay*, naiunga mkono kabisa, lakini hii *logic* ilipaswa kuwa na *replacement*, hiyo *vacuum* imeacha mamlaka makubwa sana kwa Afisa Masuhuli, mamlaka ambayo *provision* inayofuata ambayo sasa inakuwa *renumbered* (5) ya *Minister shall make regulations* hayawezi kuya-*oversee* kwa ukamilifu wake manunuzi ya dharura yalipaswa kuwa *overseen* kwa mujibu wa sheria. Tukiitunga hivi hii sheria, itakuwa bado haijasimamia, haijaweka mipaka ya manunuzi ya dharura jambo ambalo ni la hatari, hili tuliliona kwenye kashfa zingine za matumizi hayo hayo ya dharura kwa hiyo nadhani tukubaliane na turudi nyuma kwenye *spirit* ya maazimio ya mwaka 2008 ya Bunge kuhusiana na *Richmond* ili tuweze kuweka hapo mamlaka ya kudhibiti haya manunuzi ya dharura ili tusirudi huko. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tuta-*draft a new clause* kwa kuzingatia hicho ambacho anazungumza *strongly and with commitment* Mheshimiwa Mnyika, nafikiri tunamwelewa. Kwa hiyo, naomba Waandishi wa Sheria waniletee kifungu sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Wakati tunasubiri tunaendelea na Ibara inayofuata. Waheshimiwa iko hivi, kama kuna mtu ame-*move,* ngoja kwanza, kama kuna hawa ndugu wana *move amendment,* akishaeleza yule aliyekuwa na *amendment* yake kama mtu anataka kuongeza au kupunguza anasema kabla ya upande wa pili wa Serikali haujajibu, akishajibu Serikali wengine hamsimami, atabakia yule aliyeleta *movement* basi. Kwa hiyo, kwa Ibara hii tunangoja kwanza tupate maneno yanayostahili, kwa hiyo, hapa tuna-*defer* kwanza na tunaendelea kwingine. Ku-*defer* maana yake tunasubiri kwanza. Haya sasa tunaendelea.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu haikupitishwa ikisubiri kuandikwa upya)*

Ibara ya 66

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mapendekezo ya marekebisho niliyoyapendekeza ni kwamba, Ibara hii ifutwe kabisa, ambayo inahusu ununuzi wa vifaa *used*, lakini ime-*qualify* vifaa hivyo ni ndege, meli na vifaa vya treni kwa maana ya mabehewa na *engine* zake. Sasa wakati napendekeza Ibara hii ifutwe kabisa kulikuwa kuna kasoro mbili kubwa kwenye Muswada. Kasoro ya kwanza ni kwamba hakuna mahali popote kwenye tafsiri ya neno *used* ili sasa tujue kifaa kilichotumika ni kifaa cha aina gani, je, ni kifaa kilichotumika kidogo, miaka mingapi, kina ubora gani na kadhalika, ni chakavu au ni nini, hakuna hiyo tafsiri ya neno *used*. La pili, hakukuwa na *mechanism* ya *procedures* za ununuzi wa hiki kitu cha dharura yaani kuwa na *provision* ya ku-*provide regulation* za kueleza sasa *procedure* ndefu kama kutafanyika *due diligence*, tathmini ya kitaalam na nini hizo *process* zote hazikuwepo, sasa maelezo ambayo Waziri ameyatoa kwenye kuhitimisha hoja yamesema kwamba haya mambo mawili yatazingatiwa kwenye sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri sana pamoja na kuwa binafsi siungi mkono kabisa ununuzi wa vifaa vilivyotumika, tuijadili *text* ya *schedule* ambayo imeletwa na Serikali ya Ibara hii ya kujaribu ku-*provide* mazingira ya *provision* ya *regulation*, kuweka *regulation* na mazingira ya *definition* ya neno *used* ambalo mpaka sasa halijawa *defined*. Kwa hiyo, *unless* neno *used* liwe *defined*, lakini msimamo wangu katika hili au maoni yangu, *schedule* yangu ibaki pale pale kwamba Ibara hii ifutwe mpaka pale itakapokuwa imekidhi haja ya hivyo vigezo nilivyovizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mnyika kwamba Ibara hiyo ya 66 ifutwe kabisa na isionekane kwenye Muswada huu.

**MWENYEKITI**: Mnyika ame-*qualify* mwenzako anasema yeye kama *definition* ya *used* haijawekwa ndipo hapo anaendelea, ikiwekwa ataisoma hiyo. Sasa hivyo ndivyo Mheshimiwa Mnyika alivyo-*qualify* maelezo yake.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono katika kuifuta kabisa, lakini katika kuki-*qualify* hata pale ambapo hicho Ibara inazungumzia masuala ya jeshi pamoja na *civilian*, vile vile maeneo ambayo hayaleti umuhimu sawa katika masuala ya *emergency*. Kwa hiyo, wanatakiwa pia watenge kabisa masuala ambayo ni ya jeshi katika u-*emergency* wake, hayawezi kuoana na masuala ya *emergency* katika *civilian* kwenye mambo ya meli na ndege pamoja na treni. Kwa hiyo, nam-*support* Mheshimiwa Mnyika katika hizo *specifications* za kuainisha walizingatie pia na hilo.

**MWENYEKITI:** Unajadili hoja yake sio unaleta mengine. *AG!*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na mawazo ya kuifuta Ibara hii kwanza, ninayapa nafasi kubwa sana mawazo ya ku-*qualify* au ku-*define* neno *used*, lakini katika utendaji ni rahisi zaidi ku-*define used* kuliko ku-*define used* kwenye sheria. Kwa mfano, katika hoja humu Bungeni nimepata elimu kwamba ndege ambayo ina miaka 30 bado inaweza kufanya kazi ya ndege yenye miaka mitano. Sasa katika ku-*define* na zote zimekuwa *used,* kwa hiyo ukiweka *limit* uka-*define* kwamba ni mtambo au ndege ambayo ina miaka kadhaa, inakuwa ni ngumu kidogo, lakini nafikiri na naomba Mheshimiwa Mnyika alione hili anisaidie mawazo, nafikiri kwamba njia nzuri ya kufanya hiki ni kule jikoni kwenye *regulations* kwamba wakati Waziri atakapokuwa anatunga zile *regulations* na wakiwa sasa wana nafasi ya kitaalam zaidi waweze kuja na *description* ya hivi vitu ambavyo ni *used*, lakini kwa sasa hivi itakuwa vigumu sana kwa Bunge lako kutoa *definition* ya neno *used* kwa sababu inategemea kutoka *item* moja kwenda kwenye *item* nyingine. Kwa hiyo, nashauri Ibara ilivyo sasa na kama nilivyosema mawazo ya ku-*define* neno *used* ni mawazo mazuri, lakini yafanywe kwenye *regulations* kule siyo kwenye sheria hii. Nashukuru sana.

**MHE. JOHN J.MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo kadhaa. La kwanza, ni hatari sana kuacha mambo mazito yawe *defined* kwenye *regulations* zinazotengezwa na Waziri, kwa sababu *experience* yetu ya utengenezaji wa Kanuni hizi zinazotungwa na Mawaziri, inaonesha kwamba Bunge huwa linaziona hizo Kanuni baadaye sana wakati zimekwishaanza, pamoja na kuwekwa *provision* hapa inayosema kwamba sheria hii haitafanya kazi mpaka kanuni zitakapotungwa, lakini bado Mamlaka ya utungaji wa kanuni yako kule kwa Mawaziri na watatunga zile kanuni. Sasa kwa kuwa hii sheria ni mahsusi kwa bidhaa tatu tu, ndege, meli na treni yaani kwa maana ya mabehewa na vichwa, tumeshindwaje, kama Serikali bado haijajiandaa kuweka *mechanism* ya ku-*define standardisation* ya hizi bidhaa tatu, basi ni vizuri Ibara ikafutwa kwa sasa ili Serikali ikajiandae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa ufupi, hatari ninayoiona, marekebisho yaliyoletwa na Serikali yameondoa Ibara ya mwanzo iliyokuwa inasema kwamba Baraza la Mawaziri ndilo litakaloidhinisha, badala yake sasa itaidhinishwa na Waziri kwa kushauriwa na chombo anachokiunda mwenyewe na limetumika neno *advisory*, ningeweza kuelewa kama hapa kungekuwa na neno *Special Technical Committee*, lakini kwenye Muswada hapa kuna maneno *Special Technical Advisory Committee,* kwa hiyo, maana yake kuna Kamati ataiunda yeye mwenyewe Waziri itamshauri, halafu yeye ndio ataamua Baraza la Mawaziri halitaidhinisha, manunuzi yataendelea, hakuna *standardisation* kwenye sheria tunaacha mwanya mpana na nadhani kama Serikali hai-*redraft* hii, iwekwe vizuri na hayo maneno *advisory* yaondolewe kabisa.

**MWENYEKITI:** Utungaji wa kanuni za kutekeleza Miswada ni *standard application,* sasa hamwezi kusema mkafute Ibara kwa sababu ya kanuni zinazoweza kutungwa na ninyi kudai kanuni mnaweza. *AG*!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtu na kila Mheshimiwa Mbunge anachotaka hapa ni *system* ambayo ni *transparent*, *system* ambayo haiwaneemeshi watu wengine, lakini sisi kama binadam tunachoanza nacho ni *trust*, imani kwa mtu. Kwa hiyo, mimi nafikiri kwa mawazo yangu yaani kutoka moyoni, tusidhanie kwamba, Waziri atafanya mambo haya kwa maslahi yake au peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kwamba Waziri ni taasisi na nashauri kwamba labda *oversight* yetu sisi na mimi ni Mbunge, *oversight* yetu sisi twende kwenye zile kanuni.

Nafahamu kwamba, kweli haya mambo yaliyoko hapa ni mambo machache, lakini uchache wake hautuzuii sisi kumkamata Waziri kwenye kanuni na Mheshimiwa Mnyika ameonesha ni mtu anayefanya *research* nzuri na ana mawazo mazuri, tutashirikiana naye kusudi tuangalie kwamba zile kanuni zinafanya kazi vizuri. Pia hii sheria ni ya kizazi chetu na kizazi chetu kinayo Mamlaka ya kubadilisha, kwa hiyo, naomba sana kwa Mheshimiwa Mnyika, haya mambo ya umma hayana urafiki, nayafahamu hivyo, haya mambo hayana urafiki, huyu ni rafiki yangu, tutafanya vizuri, hapana, najua hilo. Lakini pamoja na haya kwamba ukubali, halafu *hands off, eyes on.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba tukubali Ibara hii ipite kama kilivyo.

**MWENYEKITI:** Kuna Kamati ya Sheria Ndogo, mkitaka kuagiza kitu kama hicho kipite huku, kwa sababu mambo yenyewe ni mazito, lakini tunayo Kamati yetu ndogo na ina Mamlaka kamili kabisa, kwa hiyo, kabla sija-*move* nakwenda kwa Zambi.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, sikuwa nimetofautiana sana na Mheshimiwa Mnyika kwamba Ibara hiyo ifutwe, lakini *on the second thought* nafikiri kwamba maelezo ambayo yalikuwa yametolewa na Serikali kwa sehemu kubwa yanaridhisha. Kwa nini na niseme tu kama alivyosema Mheshimiwa Mnyika, pamoja na kwamba kuna *provision* kwenye *regulations*, lakini bahati mbaya sana Bunge lako Tukufu halitungi Kanuni, kwa hiyo Waziri atakavyo-*define* neno *used*, itakuwa ni *discretion* yake pamoja na kwamba ana wataalam wanaomshauri, huo ndiyo wasiwasi mkubwa tunaouonesha hapa. Kwa hiyo, kama Mwanasheria ameagiza wataalam wake wamletee *version* ya kifungu fulani hapa kwa nini asitake wanasheria wake walete *version* ya neno *used* hapa ili turidhike kwamba unaposema *used* unamaanisha kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nikawa na wasiwasi kwenye *version* ambayo imekuja, kuna maneno yanayosema *public interest*, unasema *where public interest demands.* Sasa hii *how do you define* hii *public interest and who define this* public *interest,* ni mtu mmoja, watu wawili au namna gani? Maana yake haya ndiyo mazingira pia ambayo ninavyoona yanakuwa na wasiwasi. Mngetueleza vizuri ili liwe neno linaloeleweka, samahani.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Zambi kuhusiana na maneno *public interest.* Moja ya *marks* zangu nilizopata shuleni ni kuandika juu ya *public interest. Public interest* ni kama farasi mwenye kichaa. Kwa wale wanaopanda farasi, kwamba farasi mwenye kichaa akikasirika huwezi kujua atakupeleka wapi. Lakini katika *Public Law,* katika Sheria ya Umma unaposikia neno hili *public interest* ina maana kwamba kuna watu mmewaamini, mmewapa madaraka, hao watu kwa kuangalia mazingira ya nchi yetu ndiyo watakaosema hii ni *public interest.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndiyo maana nafikiri kwamba Ibara hii ukisoma *amendment* vizuri ile ya nne, inasema: "*The operation of this section shall not come into force until such time the regulations under section 105(1)(d) have been made and come into force".* Kwa hiyo, hii Ibara imesimamishwa mpaka hapo yale masharti yaliyoko kwenye Ibara ya 105, Ibara ya 105 iko kwenye ukurasa wa 84, hatujafika huko, (d) inasema:-

(1) *"The Minister may make regulations and rules for better carrying out of the provisions of this Act.*

(2) *Without prejudice to the generality of subsection (1), the Minister may make regulations prescribing,* angalia:-

> (d) Pamoja na *amendment, procurement procedures for used railways machines, ships and aircraft".*

Kwa hiyo Ibara ya 66 haitatekelezeka mpaka Waziri atakapotengeneza *regulation* na Kamati yetu ya Sheria Ndogo, itakuwa inazipitia hizo. Kwa hiyo, kwa maoni yangu sioni athari kama macho yetu yako wazi na mikono yetu iko nyuma, sioni athari ya Ibara ya 66. Lakini

naelewa hofu ya Wabunge na naelewa kwamba Waheshimiwa Mawaziri na watumishi wengine wa umma wameapa viapo vyao na ni wakati sasa Wabunge kusimamia viapo hivyo. Kwa hiyo nafikiri kwamba jinsi sheria ilivyo inatosheleza. Lakini hiyo hofu si hofu ambayo haina msingi, ni hofu ya kweli lakini kuna njia ya kuisimamia hiyo hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tunachokisema, *regulation* zitakazohusika na hii zitapitia kwenye Kamati yetu inayoshughulika na Sheria Ndogo. Ndiyo uamuzi huo. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni hizi Ibara ya 28(2) nitaongeza muda wa dakika 30 baada ya saa saba ili tumalize Muswada huu.

Ibara ya 67
Ibara ya 68
Ibara ya 69
Ibara ya 70
Ibara ya 71
Ibara ya 72
Ibara ya 73
Ibara ya 74
Ibara ya 75

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 76

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 77

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 78

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 79
Ibara ya 80

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 81

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 82

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 83
Ibara ya 84

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Ibara ya 85

Ibara ya 86
Ibara ya 87

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 88

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakubaliana na marekebisho ya Serikali kwenye Ibara hii.

**MWENYEKITI:** Asante. Aah! Unauliza nini sasa siyo *amendment*, wewe huna. Unataka ufafanuzi.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na marekebisho ambayo Serikali imeleta. Ukiona pale 2(b)(i)...

**MWENYEKITI:** Katika marekebisho ya Serikali.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Katika marekebisho. Wanaposema *a Senior Lawyer to be appointed by the Minister,* nadhani neno zuri ilikuwa ni *nominated.* Moja, mbili, katika hiyo (b) anasema *six members to be appointed by the Minister* ile ya tatu ya *Roman (iii) the Executive Secretary, the Executive Secretary is not appointed by the Minister*. Kwa hiyo, ingekuwa ni (c) ndiyo iseme *the Executive Secretary.* Nadhani nimeeleweka?

**MWENYEKITI:** Hebu rudia.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Nimesema la kwanza ile *subsection 2(b)(i), a Senior Lawyer to be appointed by the Attorney General.* Nasema *the Senior to be nominated by the Attorney General.* Halafu ile *Roman (iii))* inaanzia pale kwenye (b) ambapo inasema six *other members to be appointed by the Minister as follows*, ndiyo *Roman (i), (ii)* sasa *(iii)* inasema, *the Executive Secretary who shall be the Secretary of the Appeals Authority.* Sasa hii isiwe *Roman (iii)* iwe ni (c) kwa sababu huyu anakuwa *appointed by the President.*

**MWENYEKITI:** Mmeelewa? Mheshimiwa *AG*!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge. Tuli-*arrange* kwamba tubadilishe kusudi *Attorney General* a-nominate na ku-*appoint, but I think these are* ***asthmatics***. Lakini tuta-*take into account* hiyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tunatakiwa tuseme nini? Kwa sababu ndiyo tunatakiwa kuandika. Sasa wakuandalie, sisi tuendelee.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *88(b) six members to be appointed by the Minister as follows:- A Senior Lawyer to be nominated by the Attonery General,* ndiyo mapendekezo ambayo nayakubali kwamba badala ya *appointed* iwe *nominated.* Kwa sababu anaye-*appoint* kwanza ni Minister siyo *Attorney General.*

**MWENYEKITI:** Halafu umemsikia hiyo *Roman (iii)(b)* pendekezo Mheshimiwa anasema iwe (c) ijitegemee.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Ibara ya 89

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Inahusu Ibara ya 89 kinachohusiana na uteuzi wa *Executive Secretary* kwa maana ya Afisa Mtendaji Mkuu vile vile wa

chombo kinachoitwa Mamlaka ya Rufaa ya masuala ya Manunuzi, na-*recommend* Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba, kabla ya maneno katika sentensi hiyo ya *particulars one, there shall be an Executive Secretary of Appeals Authority who shall be appointed by the President on such terms and condition as the President may determine,* kuongeza maneno *who shall be appointed by the President,* baada ya neno *President* kuongeza maneno *upon recommendation by the Authority*, kwa mapendekezo ya Mamlaka.

Mwenyekiti, maneno ambayo yametolewa na Serikali kwamba kuhusiana na tafsiri ya mashirika ya umma na mipaka ya matumizi ya Sheria ya Matumizi ya Umma siyakubali sana. Kwa sababu kwa mujibu wa sheria hii ambayo tunaitunga, hili Baraza tutakaloliunda linakuwa *Board Corporate,* kama tukirudi kwenye Sheria huku mwanzoni kwenye uundaji wa hili Baraza na vifungu tulivyopitisha. Hii ni *Board Corporate* ambayo ina uwezo wa kushtaki, ina uwezo wa kushtakiwa, ina uwezo wa kukusanya pesa na ina uwezo wa kujiendesha.

Sasa kama ni *Board Corporate* maana yake ni kwamba ina-*fall* kwa tafsiri yangu, kwenye *category* ya mashirika ya umma. Kama ni kwenye c*ategor*y ya mashirika ya umma, naomba nisome *the Public Regulation Act, Cap. 257* kama ilivyofanyiwa marekebisho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliisoma saa zile. Nakumbuka ulitusomea kabla ya hapo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Naam.

**MWENYEKITI:** Nakumbuka ulitusomea kabla ya hapo?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** *Yah*! Kwa hiyo, nataka kusema tu kwamba, kwa mujibu wa hiyo Sheria ya Mashirika ya Umma, watendaji hawa wa mashirika ya umma, wanapaswa kuteuliwa na Bodi. Rais anateua Mwenyekiti na mamlaka ya Urais yanakuwa makubwa tu ya kuteua Mwenyekiti. Anaiunda ile Bodi, Bodi ikishaundwa kama Wajumbe wanateuliwa na Waziri au Rais, Bodi ikishakuwepo, ili iweze kufanya kazi yake vizuri Bodi ikae, iamue inamteua nani kufanya kazi za kiutendaji. Sasa kwa sababu *practice* hiyo hatuifuati sana, basi angalau tuje *middle point,* kwenye sheria kwamba Rais ateue baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwenye Bodi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti. Nataka kutoa ufafanuzi tu kidogo. Haya Mashirika yote ya Umma yameundwa chini ya *Public Corporation Act.* Lakini si mashirika yote ya umma yako chini ya Sheria hiyo. Mashirika mengi ya umma yameundwa na sheria zake zenyewe. Mashirika machache sana yameundwa na *Public Corporation Act,* hayazidi hata manne au matano. Kwa hiyo, si sheria hiyo ina-*apply* kwa mashirika yote, hapana. Nilitaka kutoa tu ufafanuzi huo.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa hili hapa!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Waziri wa Utawala Bora, amesema vizuri. Lakini zipo tabia ambazo inabidi tuzibadilishe kama anavyosema Mheshimiwa Mnyika. Isipokuwa suala linakuja je, ni hapa? Nakubaliana kwamba kwa mujibu wa Sheria hii ni *Corporate Board* na ukirudi sasa kwa Waziri kwamba *not all Corporate Boards* za *Public Corporation* zina-*fall under Public Corporation Act* ikiwa ni pamoja na *TANESCO*. Kwa hiyo, kama nilivyosema mwanzoni Ndugu yangu, Mheshimiwa Mnyika, hii hapa pia ina-apply hivyo hivyo kwamba, *if we think about changing this for the future* tunaweza. *This is the reading document,* tunaweza kurudi tukafanya masahihisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la Mheshimiwa Mnyika siyo la kupuuzwa. Maoni yangu ni kwamba, siyo mahali hapa kwa mujibu wa sheria hii, kwa sababu kama una-*base* kwenye *Public Corporation Act,* nadhani ita-*apply.* Ndiyo maana yake. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo ya mtaala *corporate governance* ya *Public Procurement Authority* itakuwa kama ambavyo Sheria hii inasema. Lakini kwa sababu ya ku-*improve,* Bunge hili la Kumi, bado lina vikao vingi sana, tunaweza kurudi hapa tukazungumza, wewe ukaja na maoni yako pia, tukazungumza, tukabadilisha kama Wabunge watakubaliana na mawazo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maoni yangu kwenye hili, vile vile nataka niseme ni mawazo ambayo nayaheshimu sana, isipokuwa wakati wake siyo kwenye Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Maelezo ya Waziri wa Utawala Bora pamoja na maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yamethibitisha kwamba, hapa ndiyo mahali pake na hapa ndipo tunapoweza kufanya. *(Makofi)*

Kwa tafsiri ya maelezo aliyoyasema Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora ni kwamba, Sheria niliyoinukuu haihusiani na mamlaka hii tunayoiunda leo. Kwa hiyo, tuiweke pembeni, hii niliyoinukuu na maelezo ya Mwanasheria Mkuu yanasema kwamba, Mamlaka hii tunayoiunda, hii *Procurement Authority Regulatory* tumeshaipita, sasa hivi tunaunda *Appeals Authority*. Mamlaka yake yanaundwa kwa sheria yake na hayo maneno vile vile ameyatumia Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora.

Sasa kwa kuwa Sheria yake ndiyo hii tunaitunga sasa hivi. Sasa tuingize hayo maneno, ili sheria yake hii bila kujali kinachosemwa na *Public Corporation Act* ambayo mna-*argue* kwamba haihusiki. Tuache pembeni, basi tuihusishe hii sheria tunayoitunga sasa tuongeze tu maneno pale kabla ya neno *President.* Mimi sijamvua mamlaka Rais ya kuteua. Kwa sababu ni msimamo ambao nauunga mkono ingawa ni msimamo mkali, nimekuja kwenye msimamo wa katikati, simvui Rais mamlaka ya kuteua. Ninachokisema ni kwamba kabla ya Rais kuteua, apokee mapendekezo ya Bodi na iingie ndani ya Sheria hii. Tuingize maneno *upon recommendation by the Board. (Makofi)*

Kwa kufanya hivyo tutakuwa tume-*reflect spirit ya* sheria hiyo ya *Corporation* pamoja inatakiwa itumike hapa, lakini tuna-*reflect spirit* ya Mwanasheria Mkuu pamoja na *spirit* ya Waziri wa Utawala Bora ambaye anasimamia *Corporate Governance*, hapa tunasimamia *Corporate Governance at the President's Office,* tufanye hivyo, tuboreshe utendaji huu wa uwajibikaji. Vyombo vifanye kwa uhuru wake. Rais ateue Mwenyekiti, vyombo viteue watu wake, wakatende kazi huko. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, pale nyuma tulikataa pendekezo hilo *for the time being,* haliwezi likaingia kinyemela. Ni mfumo ule ule na tulishaikataa, ilikuwa *by* mapendekezo ya Bodi. Kwa hiyo, hapa *floor* iwe hivyo hivyo. Waheshimiwa Wabunge kuna mambo mengi mnayotaka kuyafanya na mengine myalete kwa utaratibu ambao unatusaidia sisi kubadilika mifumo. Lakini siyo kusukuma kaneno kadogo pembeni. Kwa hiyo, ibara hii napendekeza tukikubali kama kilivyo halafu tuendelee.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 90

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 91

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 92
Ibara ya 93

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 94
Ibara ya 95

Ibara ya 96

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 97

*(Ibara iliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 98

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 99

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 100
Ibara ya 101

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 102
Ibara ya 103

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko)*

Ibara ya 104

**MWENYEKITI:** Napenda kumkumbusha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tuliruka ibara ya 65. Wameleta marekebisho? Kwa sababu muda ukifika tunataka tuyafanye marekebisho, *otherwise* hatuwezi kwenda.

Ibara ya 104 ina marekebisho, Mheshimiwa Zambi!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 104 (2) (a) inasomeka:-

*"Without reasonable excuse fails or refuses to give information..."*

Sasa baada ya neno *information,* pawe na neno '*or produce'.* Sijui kama *AG* ameliona, naona kuna neno lina *miss* hapo na ndio mapendekezo niliyoyaleta pia kwenye *Schedule of Amendments* niliyoiwasilisha.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yangu ni kwamba, hatuna haja ya kufanya hivyo na ile koma ndio hasa kwa sababu tunaanza, *"Without reasonable excuse, fails or refuses to give information, produce any document, records or reports required under subsection (2)."* Sasa katika *flow* ya kawaida ya Kiingereza, huhitaji kuweka *or* pale. Nafikiri wako wataalamu wengi waliosoma *Oxford* wataniunga mkono kwenye hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zambi, nadhani msibishane.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wala hatubishani, nakubaliana na yeye kwa sababu, pale palikuwa pame-*miss* neno lolote, mimi nilifikiri '*or'* yeye amefikiri koma, nakubaliana na yeye.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Baada tu ya Ibara ya 104 (1) (e), yale maneno yanayofuata kwenye ukurasa wa 83, *"commits an offence and on conviction shall be liable"* baada ya neno *liable,* yafutwe yale maneno mengine yote na yawekwe haya ya

kwangu; *"liable to both imprisonment for a term not exceeding thirty years and to payment of the full amount of the loss incurred or to confiscation of personal properties to cover the loss." (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, makosa yote makubwa ya manunuzi na yanayohusu ufujaji mkubwa wa fedha, ndio yale yaliyoainishwa katika Ibara ya 104 (1), ambayo ni (a), (b), (c), (d), (e). Sasa nashauri na kulishawishi Bunge lako likubaliane na mapendekezo yangu haya kwa kuweka adhabu hii kubwa kwa hawa watu ambao wanafuja mali za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu, wameonekana wakilalamika mara kwa mara na wakasema kuwa haiwezekani mali za Serikali zikageuzwa kuwa shamba la bibi. Sasa na sisi Bunge hili, tumsapoti Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuweka Sheria ya mfano, hakuna mantiki ya mtu, tuseme sisi tunachotaka fedha alizosababisha hasara zirudishwe. Ndio faida ya Watanzania kuliko sasa hivi, Sheria hapo inasema kwamba, atapewa adhabu ya kulipa sio chini ya shilingi milioni kumi lakini tusiwaachie Mahakimu kuamua, tuamue hapa kwamba, sisi tunachotaka ni fedha iwe *recovered* kwa sababu hakuna mantiki ya mtu analisababishia Taifa hili hasara ya shilingi bilioni 200 halafu wewe ukamuachia Hakimu aamue kati ya milioni 10 na kuendelea, kwa nini, asizifidie fedha zote alizosababisha hasara? Baada ya hapo, iende sambamba, analipa fidia ya fedha zetu na anaenda jela miaka 30 ili iwe fundisho. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii. Moja kwa moja napenda kuungana mkono na Mheshimiwa Mpina, kutokana na *amendment* yake aliyoifanya hapa na hii ina maana inaleta *justification* ya Bunge hili kwamba, hatupendelei suala zima la ubadhirifu. Kama watu watalisababishia Taifa hili pengine hasara ya shilingi bilioni 20, shilingi bilioni 50, halafu mtu unampiga faini ya shilingi milioni 10, hailingani, kitu kama hicho. Kwa hiyo, naomba Bunge lako Tukufu na nawashawishi Wabunge wenzangu kwamba, lazima tuweke kigezo kiasi kwamba hata manunuzi yote yatakayofanyika, basi mtu huyo ni lazima mwisho wa siku awajibike kwa *loss* itakayopatikana katika Taifa hili, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hata Mungu alipoona Sodoma na Gomora matatizo yamekuwa makubwa sana, adhabu aliyoamua kutoa ni ya kugharikisha Sodoma na Gomora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha Watanzania sasa hivi ni kwenye eneo la manunuzi. Fedha tunazokusanya inaonekana kwamba, kwenye manunuzi kule ndiko zinakopotelea na mpaka sasa tunasema kwamba, hatutanunua vifaa vipya katika mazingira fulani kwa sababu hatuna fedha. Naungana na Mheshimiwa Mpina, adhabu kali inatakiwa kwenye eneo hili kama alivyopendekeza. Lakini pale ambapo amesema kwamba, isiyozidi miaka thelathini, Hakimu anaweza akamfunga mwaka mmoja au mwezi mmoja! Hapo ndipo sasa tunatofautiana, angeboresha kwamba na isipungue miaka ishirini. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Actually, point* aliyoisema Mheshimiwa Lugola, ndiyo nilikuwanayo; *not exceeding 30 years,* maana yake kwa kweli tunaruhusu hata mwezi mmoja au miezi miwili. Kwa hivyo, *amendment* anayoipendekeza Mheshimiwa Lugola, ndiyo niliyokuwanayo, *not less than 20 years. (Makofi)*

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono mabadiliko haya ya Mheshimiwa Mpina, lakini natia msisitizo kwamba, watu watakaosababisha hasara katika manunuzi, wafilisiwe mali zao ili kufidia hasara zilizosababishwa. Pia kuweka *fine* ya shilingi milioni 10, naona hili jambo sio sahihi kwa sababu Sheria haitungwi kila siku, shilingi milioni 10 ya leo haitakuwa sawa na shilingi milioni 10 ya miaka 10 ijayo tutakapokuwa tunatekeleza Sheria hii. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata bahati ya kulishauri Bunge, bahati ya kipekee. Katika kutunga sheria tusiwe na hasira. Hasira ni pango la shetani. Mimi sio Mhubiri lakini siko mbali na hao, kwa sababu angalia makosa yanayotajwa; nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba, hili tatizo linahitaji adhabu kali, nakubaliana na ninyi kabisa.

Lakini angalia makosa yanayotajwa katika Ibara ya 104 kwenye *philosophy* ya kutoa adhabu, adhabu unayotoa ni lazima iwe *propotional* na kosa, yaani ilingane na kosa lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa angalia (a); mtu ambaye kwa kufahamu anatoa taarifa ya uwongo. Angalia (b); mtu ambaye ana-*interfere* au ile *exerts* ya ku-*interfere.* Angalia (c), mtu ambaye anafungua ile *sealed tender* au anatoa taarifa ya *information* zilizoko mle ndani. Angalia (d), mtu ambaye ana-*connives,* yaani anashirikiana kwa nia mbaya na (e); mtu ambaye anasababisha hasara, sawa! Sasa tunasemaje, huyo mtu anafanya kosa na kama akipatikana na hatia, tunachotoa pale ni *minimum sentence.* Yaani katika kutoa adhabu, Hakimu hana *option* isipokuwa kutoa hiyo adhabu ambayo tunaisema; *"shall be liable to a fine not less than ten million." So* tuzungumze kwamba, *10 million is not adequate.* Hizo ni busara, lakini mnapofanya busara hizo msiwe na hasira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kwenye kifungo, kifungo ambacho hakipungui miaka mitano, Hakimu hana mamlaka ya kutoa kifungo ambacho hakifikii miaka mitano na makosa tunayozungumza ni yale yaliyotajwa pale.

Waheshimiwa Wabunge, iliwahi kutungwa Sheria hapa mwaka 1983, Sheria ya Wahujumu Uchumi; Sheria ile ilitungwa kwa hasira na matokeo yake mnayafahamu. Kwa hiyo, ninyi ndio mnatunga Sheria, kazi yangu na nimesema nina bahati kwamba nimepata nafasi ya kulishauri Bunge kwenye hili na silazimishi, mimi maoni yangu ni kwamba, adhabu hizo kwa makosa yaliyotajwa pale zinatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mnaweza kusema na nimesikia mmoja anasema huyu mtu ambaye ana-*cause* hasara, afilisiwe au alipe thamani ya ile hasara aliyosababisha, lakini msisahau kwamba, kuna Sheria nyingine inayoitwa *Public Officers Recovery of Debts,* ambayo pia inaweza kutumika katika mazingira haya. Kwa sababu na wengine hawa ni *Public Officers,* wengine sio *Public Officers.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa maoni yangu nilikuwa nashauri kwamba, yale maoni ya Mheshimiwa Mpina, pamoja na uzuri wake, lakini tusiyakubali, tuchukue haya ambayo yapo hapa, kifungo kisichopungua miaka mitano sio kifungo kidogo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho nimejifunza ni kwamba, Mwanasheria wetu hana uzoefu na manunuzi. Inawezekana hajui mfumo wa manunuzi unavyokwenda. Makosa yaliyotajwa katika Ibara ya 104 (a)… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, zungumzia hoja yako. Kusema mtu fulani hana uzoefu, wote tutakuwa hatuna uzoefu wa kitu fulanifulani, kila mmoja wetu atakuwa hana uzoefu wa kitu fulani.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa Mwongozo wako. Makosa yaliyozungumzwa katika Ibara ya 104 (a), (b), (c), (d) na (e) ndio mahali pekee ambapo manunuzi huwa yanachakachuliwa; ndio sehemu pekee ambapo watu wakitaka kufanya wizi katika manunuzi wanafanyia katika vifungu hivyo. Kwa *fair* sasa, kama alivyozungumza Mwanasheria hapa kwamba, tunatoa adhabu kubwa sana na yeye amesema kwamba, haya makosa ni madogo na sisi tumesema ile shilingi milioni 10 sasa aliipataje? Amesema kwamba, malipo yatafanyika kulingana na kosa lililotendwa. Sasa kama wewe umeingilia mfumo wa manunuzi, Taifa likapoteza shilingi bilioni 200; ni kwa nini sisi tuzungumzie ku-*recover* shilingi milioni 10? Tumuachie Hakimu ku-*recover* shilingi milioni 10! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa maana nyingine, kama anavyozungumza yeye kwamba haya makosa ni madogo sana, maana yake ni kwamba hata hiyo adhabu ya shilingi milioni 10 itakuwa ni kubwa basi kama makosa haya ni madogo. Ndivyo…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Taarifa Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Amalize kwanza. Naomba amalize. Hebu maliza, endelea Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria alisema tusiwe na hasira na yeye asiwe na hasira. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Hebu endelea, mimi ndio naongoza Kikao, kwa hiyo tunataka tuelewe vizuri.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema kwamba, tusitunge Sheria ambazo zinapendelea upande mwingine. Tulitunga Sheria hapa ya Maliasili, mwananchi akiingia tu kwenye *Game Reserve,* hata kama hana silaha, akijaribu kukimbia anapigwa risasi na Wabunge tuliridhia Serikali ilivyosema. Leo tuna Sheria ya kuteketeza mali za wananchi, kwamba mtu akileta mali bandia hapa nchini zinateketezwa. Leo mtu aliyefuja fedha za umma, tunaendelea kumbembeleza! Tusitunge sheria za upendeleo! Mara nyingi hili limekuwa likitokea, Sheria ambazo zinawahusu wananchi zinakuwa kali zaidi, sheria ambazo zinawahusu watumishi wa umma ni za kubembeleza, *very soft!* Kwa nini? *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walisimama)*

**MWENYEKITI:** Haya, nyie wote mkae, naamua kama ifuatavyo. Hapa *amendment* imeletwa na Mheshimiwa Mpina, lakini ukiwasikiliza waliochangia, kila mtu alikuwa na ya kwake, ingawa *spirit* ni hiyohiyo. Sasa hii Ibara itarudi kwenye Kamati, mtajadiliana kwenye Kamati vizuri na kila mtu akiwa *sober,* sio kila mtu unamfikiria uliyemuona mwizi sijui wapi huko, basi hapa ni lazima afungwe tu. Tukae tumfikirie mtu ambaye hayupo lakini pia tunataka kuganga yajayo. Kwa hiyo, hii Ibara inarudi kwenye Kamati. Tukiahirisha hapa, Kamati itakwenda kukaa na *interested parties* waende kushiriki kule. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilirudishwa kwenye Kamati husika ili ijadiliwe zaidi)*

Ibara ya 105

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 105, nimekubaliana na masahihisho ya Serikali.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Msingi wa mapendekezo ya marekebisho ninayoyapendekeza kwenye Ibara ya 105, ni kuongeza maneno kwenye kipengele cha (1), baada ya neno *The Minister,* kuweka maneno "*in consultation with responsible Parliamentary Standing Committee",* halafu maneno yanaendelea, *may make regulations and rules for the better carrying out of the provision of this Act.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa pendekezo hili ni kwamba, kwenye Sheria hii tunayoitunga na hata Sheria nyingine, mara nyingi yanapokuwepo masuala tete sana ambayo yanaonekana ni vigumu sana kupita Bungeni, kunawekwa *General Clause* kwenye Sheria, halafu inasema kwa kadri ya Kanuni zitakavyotungwa. Halafu baadaye, Waziri anakwenda kutunga Kanuni kwenye Gazeti la Serikali, Kanuni zinakuja kuletwa Bungeni baadaye, Kanuni zinaanza kufanya kazi na mkono ule wa Bunge wa ku-*scrutinise* Kanuni kabla hazijatoka kwenye Gazeti la Serikali kwa kiwango kikubwa unakuwa haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa *spirit* ya maelekezo ya mdomo ambayo uliyatoa kuhusiana na Ibara ile kuhusiana na masuala ya manunuzi ya vitu chakavu; ulielekeza kwamba, wa-*consult* na Kamati husika, nakubaliana kabisa na yale maelekezo lakini ingekuwa ni vyema kwa unyeti wa Muswada huu na kwa kuwa kuna vipengele vingi sana ambavyo bado kama Bunge hatujaviingia kwa undani wake, kuwe na maneno hayo kwenye Sheria ili Waziri kabla ya kutoa Kanuni kwenye Gazeti la Serikali, a-*consult* Kamati husika ya Bunge kabla Kanuni hazijatolewa. Hii itawezesha Bunge kutimiza vizuri sana ule wajibu wa Kikatiba wa Ibara ya 63(2), wa kuisimamia Serikali kupitia kutunga Sheria lakini *extension* yake vilevile ni kusimamia utungwaji wa Sheria ndogondogo na *regulations* sehemu ya Sheria ndogondogo, ahsante.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo mengine yanataka pia tuangalie *concept* ya *Public Law.* Tunachozungumza hapa ni utendaji wa Mihimili na Waziri kwa mujibu wa Ibara hiyo ni *delegate.* Wale waliosoma Sheria, ni kwamba *delegatus non protest delegare* kwamba, Bunge linamtuma Waziri akafanye kazi ya kuandika Kanuni. Sasa huyu mtumaji, huwezi kusema ukifanya niletee, hapana! Sio *principle* ya *Public Law* na kwa sababu kuna Kamati ya Bunge inayoshughulikia hizi Sheria ndogondogo, hii ndio itakuwa kazi yake. Lakini kusema *Minister in consultation* na hiyo Kamati ya Bunge, kwanza utakuwa unavunja msingi wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo inalipa kazi Bunge kuisimamia Serikali na inaisimamia kwa sababu, *Minister is a delegate and a delegate can not delegate.* Kwa hiyo, Waziri kwa msingi wa Kanuni hiyo, anawajibika Bungeni na kama juzi ulikuwa kwenye semina ya Profesa Kabudi, ni vizuri kufahamu hizi *principles* za *Public Law.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna mtu ambaye atakuwa amechukizwa kwa kazi ya Waziri, kuna Mhimili wa Dola ambao utasema Waziri, umekwenda kinyume na madaraka ambayo ulipewa na Bunge. Itakuwa vibaya sana kama na Wanakamati wa Bunge watakuwa pia ni washtakiwa katika huo msukumo. Utakuwa sasa unairuhusu Mahakama kuja jikoni huku Bungeni kwa msingi ule wa *judicial review of administrative action* kwa sababu, maamuzi haya ya Mawaziri, yanakuwa *questioned* Mahakamani! Sasa ukisema *in consultation with* Kamati ya Bunge na yenyewe itakuwa *questioned;* na itakuwa bado ile unasema *supremacy of, not supremacy but* ile kazi ya Bunge, sasa Mhimili mwingine unaukaribisha bila wewe mwenyewe kufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo, nimepata bahati sana na bahati yangu kama alivyosema Profesa Kabudi, ninao utabahari wa jambo hili. Kwa hiyo, nashauri Bunge lisikubali kuwa sehemu ya kutunga hizi Kanuni, isipokuwa lisimamie hizi Kanuni zitakapokuwa zinaletwa kwenye Kamati inayohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndio mawazo yangu.

**MWENYEKITI:** *The spirit* aliyokuwanayo Mheshimiwa Mnyika, inafanana hivyo. Sasa kusema kwamba, *in consultation,* maana yake tuingie katika kutunga, hiyo hapana lakini *spirit* yake ilikuwa kwamba, hizo Kanuni ziwe zimefika Bungeni na kuangaliwa, sio *in consultation* kama alivyoweka. Kwa sababu, *in consultation* maana yake ndio tunatunga kama tunavyotunga hii Sheria. *(Makofi)*

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kidogo tu. Ibara ya 65, imeongelea *Emergency Procurement* na fasili ya (5) ya Ibara hiyo inasema, Waziri atatunga Kanuni za *Emergency Procurement.* Tukija kwenye Ibara ya 105 (2), kinaongelea Kanuni na kimesema, *Without prejudice to the generality of subsection (1) the Minister may make regulations prescribing;* sasa siioni *procedures for emergency procurement,* haiko hapa, katika zote hizo mpaka (x) kule; kwa hiyo, kama *AG* anakubali, napendekeza pale baada ya (d), iwepo (e) mpya, iseme *procedures for emergency procurement.* Baada ya kuiweka (e) hiyo, sasa zinazofuata zote ziwe *re-numbered,* (e) iwe *procedures for emergency procurement.* Baada ya kuiweka (e) hiyo mpya, (e) ya zamani na nyingine zote za chini ziwe *re-numbered.*

**MWENYEKITI:** Kwanza twende kwa Mnyika. Kama navyosema, *the spirit* mimi ninavyoiona, Mnyika alichokitaka ni kwamba, wakishatunga Kanuni sio ziendelee tu hivi, lakini Kamati yetu ile iweze kushughulika sio *in consultation, the word consultation* kwa kweli sio. Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nilikuwepo kwenye Semina ya Profesa Kabudi ambaye ni Mwanasheria anam-*refer...*

**MWENYEKITI:** Bwana jibu achana na habari ya kwenye semina huko.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye hoja kwa sababu, tafsiri ya kukiukwa kwa Katiba, inategemea *context* na mimi niseme tu kwamba, ndio maana sikuweka Bunge, sikuweka *in consultation with Bunge;* nimeweka *in consultation with responsible Parliamentary Committee,* nilikuwa *cautious.* Kwa sababu, nilikuwa naelewa kuna Sheria nyingine ambayo *AG* ndio alipaswa ku-*refer* na sio maamuzi ya Mahakama ama baadaye maamuzi ya kuamuliwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria nyingine, *the Interpretation of Laws Act, Cap (1)* kama ilivyofanyiwa *revision* mwaka 2002, *Part VI* ya hiyo Sheria ambayo imetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inasema na ninanukuu mstari mmoja tu; *provisions relating to subsidiary legislations* ambapo hizi *rules, laws and regulations* hizi zina-*fall* kwenye *category* hiyo. *Section 38* ya Sheria hiyo inasema kwamba, Serikali inawajibika, nitatafsiri tu, kuweka kwa Bunge Kanuni ambazo Serikali imezitunga ili Bunge liridhie au lizikatae na kama Serikali haikuzileta, Bunge linaweza likazileta ikaziridhia au ikazikataa kwa mujibu wa Sheria, lakini huu msingi wa kisheria ni wa baadaye, tendo limeshafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya *AG,* ndio kauli ambayo inatoa viburi kwa Mawaziri wengi sana wanaotunga Kanuni. Wanatunga Kanuni mbovu sana! Mkimwambia tuletee kwenye Kamati tutoe maoni, anasema sio kazi yenu kutunga Kanuni kwa hiyo hatuwaletei, tutawaletea tukishazitunga! Kwenye tafsiri hiyohiyo ya Kikatiba ya Ibara ya 63 na kwenye misingi ya utawala bora, *consultation* ni jambo la kawaida, inategemea *level* ipi ya *consultation. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *consultation* na Kamati ya Bunge, haiondoi Mamlaka ya Bunge kuisimamia Serikali! Sasa kwa unyeti wa hizi Kanuni, mambo mengi tumeyaacha hapa tunasema yatakuwepo kwenye Kanuni, yatakuwepo kwenye Kanuni, halafu tunamwachia Waziri akatunge Kanuni, tunaletewa baadaye, tunajua Kamati ya Sheria Ndogo huwa inaletewa baadaye baada ya Kanuni kutungwa sio kabla! Sasa ili tupate mwanya wa kisheria wa kuilazimisha Serikali ku-*consult* na Kamati, tuingize hii *provision* hapa! Haiondoi Mamlaka ya Bunge kwa mujibu wa hizi Sheria nyingine nilizozi-*cite,* yataendelea kuwa pale na Mahakamani litahojiwa Bunge, sio Kamati ya Bunge kwa sababu, maamuzi ya Bunge ni ya Bunge, sio Kamati ya Bunge. *Consultation* sio maamuzi, ni mashauriano tu. Kwa hiyo, huwezi kuhojiwa Mahakamani kwamba, alikuja huyu akanitaka maoni, nikatoa maoni yangu! Huwezi kuhojiwa Mahakamani! Kwa hiyo, Mheshimiwa *AG,* anapotosha tu tafsiri ya Kisheria na tafsiri ya Katiba. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hapana sasa! Kamati ya Sheria Ndogo itakuwa na jukumu la kuchambua Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi, ndio inavyosema.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda niliotoa umekwisha na Bunge linarudia.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2), nilikuwa nimeongeza dakika 30, zimekwisha lakini hatujamaliza. Kwa hiyo, tukirudi saa 11.00 jioni, tutapata marekebisho ya Ibara ya 65, tutakuwa tumepata *consultation* ya Ibara ya 104, tutaendelea na Ibara zilizobakia kwa dakika chache zitakazokuwa zimebakia.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge, mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.30 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipoondoka tulikuwa katika hatua ya Kamati ya Bunge Zima, kwa hiyo, tutaendelea na Kamati ya Bunge Zima.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Tulikuwa na mambo ambayo niliagiza yafanyiwe kazi, kwanza ni Ibara ya 65, Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ibara ya 65, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Mnyika ambayo ilikuwa inapendekeza kwamba tuweke Ibara inayohusu mbadala wa Ibara ya 4 iliyofutwa. Tumefanya marekebisho na tuna jedwali la mabadiliko *(further schedule of amendment)* kwenye (a) tunasema, *in paragraph (Z) of the schedule of amendment*

*are amended by deleting subparagraph (b) and substituting for it the following (b) by deleting subclause (3), renaming subclauses (4) to (9) as subclauses (3) to (8) and deleting the word "Cabinet" appearing in subclause (3) as renamed and substituting for it the words "Government Procurement Services Agency".* Hivyo ndivyo tulivyofanya kwenye hoja ya Mheshimiwa Mnyika ili kuwa na hiyo *Government Procurement Service Agency* ili ifanye hiyo kazi ambayo tulikuwa tunazungumza asubuhi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG*, unaweza kueleza maana ya hiyo *amendments* kwa lugha rahisi kwa sababu hizi *amendment* zitaletwa sasa hivi, wanachapa nyingi ndiyo maana tulitaka ueleze kwa sababu bado hazijagawiwa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kama tunayo *schedule of amendment* ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha inayozungumzia *paragraph* (Z)...

**MWENYEKITI:** Ile *amendment* ya mwanzo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Nafikiri *amendment* ya pili, sasa tunachofanya ni kwamba katika ile (Z) ya *schedule of amendment* tunafuta *subparagraph* (b) na badala yake tunaweka (b) mpya ambayo inafuta kifungu kidogo cha (3). Pili, vifungu vidogo vya (4) - (9) tunavitaja kama ni (3) -(8), kwa maana kwamba kifungu cha 4 kinakuwa cha 3, cha 5kinakuwa cha 4 hivyo hivyo mpaka 8, cha 9 kile kinakuwa cha 8. Tukishafanya hivyo, tunafuta maneno *"Cabinet"*, Baraza la Mawaziri ambayo yanayoonekana katika kifungu kidogo cha 3 kama kilivyorekebishwa na badala yake tunaweka maneno *Government Procurement Services Agency*, Mamlaka ya Manunuzi ambayo ni ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishafanya hayo katika (b), tunafuta *paragraph* (c) iliyopo na tunaweka (c) mpya kwa maana kwamba katika kifungu kidogo cha 6 kama kilivyorekebishwa zamani kilikuwa kifungu cha 7, tunafuta maneno '*may'* na '*shall'* na tunaweka maneno mengine ambayo ni "*may" and "shall" respectively*. Kwa hiyo, tunasema *may and shall* na tunaongeza neno la mwisho *respectively* katika fungu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, tunaridhika kwamba tumefanya yale ambayo Mheshimiwa Mnyika alikuwa anatushauri tufanye. Ahsante.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo niliyoyasikia maana nyaraka sina, nakubaliana na marekebisho yaliyofanyika.

*(Ibara ya 65 ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 104

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ibara ya 104 ilikuwa ni mapendekezo ya Mheshimiwa Luhaga Johnson Mpina na nichukue nafasi hii kutambua ustaarabu mkubwa sana wa Mheshimiwa. Tulichofanya ili kuzingatia maoni au mapendekezo ya Mheshimiwa Mpina ni kwamba tumefuta *paragraph* (O) kwenye ile *Further Schedule of Amendments*. Katika Ibara ya 104(1) tunafuta maneno yale ya mwisho, baada ya Ibara ya 104(1)(a)(b)(c)(d) na (e) kuna maneno yanafuata, yanasema '*commit an offence'* hayo maneno yanaandikwa upya kama ifuatavyo. Nitayasoma kwa Kiingereza halafu nitatafsiri kwa Kiswahili. Baada ya kusoma, ukiteremka chini yanasema: "*Commits an offence and on conviction shall be liable to a fine of not less than ten million shillings or to imprisonment for a term of not exceeding seven year or to both, and in addition to the penalty imposed in this section, the court shall order that the amount of loss incurred by complainant be compensated, failure of which the court shall issue an order of confiscation of personal property of the person convicted in order to recover the loss". (Applause)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana kwamba badala ya kusema kama ilivyosemwa kwamba huyu akipatikana na kosa atalipa faini ya shilingi milioni kumi au kifungo cha jela cha miaka isiyopungua mitano sasa tunabadilisha hiyo, tunasema kwamba atalipa faini kwa kiwango kisichopungua shilingi milioni kumi au kifungo gerezani kisichozidi miaka saba au adhabu zote

mbili, pamoja na adhabu hizo Mahakama itatoa amri kwamba kiwango kile cha hasara alichosababisha kifidiwe naye. Kama ikishindikana, Mahakama itatoa amri ya kutaifisha mali zake binafsi ili kufidia hasara iliyosababishwa. *(Makofi)*

Tumefanya hivyo Waheshimiwa baada ya kutafakari Sheria ya Rushwa ambayo ina makosa kama haya na Mheshimiwa akatuelewa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina!

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi lakini pia niishukuru Serikali kwa kukubaliana sasa kwamba hawa wanaofanya ubadhirifu wa mali za umma wafidie hasara hiyo waliyoisababisha na kama sivyo basi wafilisiwe ili kufidia hasara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna kitu kimoja tu ambacho hatukuelewana sawasawa, ni kwamba baada ya ushauri ule wa Sheria Mama ya Rushwa ikakubalika kwamba miaka mingi iliyopo katika sheria ile ni miaka saba. Kwa hiyo, tukasema kama ndivyo hivyo Sheria hii ya Rushwa pia kutokana na ubadhirifu ulivyokisiri katika nchi yetu, Sheria ya Rushwa nayo italetwa hapa Bungeni tuweze kuipitia upya ili tuweze kurekebisha baadhi ya maeneo yanayohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kosa moja tu ambalo limefanyika ni hapa kwenye *commits an offence and on conviction shall be liable to a fine not less than ten million shillings or to imprisonment for a term of not less than seven years.* Sasa kama hiyo inakubalika *not less than seven year*, kama marekebisho hayo yatafanyika mimi sina matatizo kwa sababu nilikubali hivyo kwamba iwe miaka saba na kuendelea kwa sababu adhabu kwenye Sheria Mama ya Rushwa ilikuwa na hiyo miaka saba, ndiyo tukakubaliana kwamba sasa iwe miaka saba na kuendelea siyo chini ya miaka saba. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria hapa unaandikaje?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya msingi katika mambo ya rushwa ni Sheria inayoitwa *Prevention and Combating of Corruption.* Nakubaliana na Mheshimiwa Mpina kwamba maoni yake yalikuwa hivyo lakini Sheria hii Mama, ukiona *corrupt transactions in procurement,* adhabu inayotolewa hapo ni kama ifuatavyo, *a person convicted of an offence under this section shall be liable to a fine not exceeding fifteen million shillings or to imprisonment for a term not exceeding seven year or to both.* Sasa *wording* mimi sina tatizo, kusema kubadilisha na kusema *not less than seven years* kwa sababu kwanza makosa haya kama tulivyoona kwenye Kamati yanahitaji kushughulikiwa labda kwa njia tofauti, nafikiri nikubaliane naye kwamba tubadilishe pale badala ya kusomeka, nafanya hivyo nikijua kabisa kwamba vijana wangu watanikalisha kwenye masomo ya utungaji wa sheria, lakini kwa sababu ya *negotiation* hizi tunazofanya hapa Waheshimiwa Wabunge yale maneno '*for a term not exceeding'* tuseme '*for a term of not less than seven years'. (Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 106

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unisamehe sana, Ibara ya 105 haikuafikiwa, tulikuwa katikati ya Ibara ya 105 ndiyo ukaahirisha kikao.

**MWENYEKITI:** Sawa!

Ibara ya 105

**MWENYEKITI:** Nilikuwa na watu waliokuwa wanaijadili, ambao walikuwa na *amendments* walikuwa Mheshimiwa Zambi na Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Nilikuwa na *issue* hapa na mimi.

**SPIKA:** Mmh! Eleza *issue* yako.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii ya 105 inaongelea kanuni kwamba Mheshimiwa Waziri atatunga kanuni katika maeneo haya. Sasa eneo la madawa na vifaa vyake halipo. Kwa hiyo, napendekeza hapo kwenye (e), tui-*insert* (e) mpya ambayo inasema: *procedure and processes for procurement of medical equipment and supplies,* baada ya ku-*insert* (e) tunazi-*renumber* zile zote zinazofuata, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *amendment* huna lakini Waziri akitaka kuongeza atasema, Mheshimiwa AG.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maeneo ambayo Waziri amepewa mamlaka ya kuyawekea kanuni siyo *exhaustive*. Kwa hiyo, Waziri anaweza pia kuyawekea *regulations* maeneo mengine ambayo hayapo hapa, ndiyo maana yake hiyo, sina tatizo na *medical whatever,* lakini kama akitaka kufanya hivyo na kuna sababu hakuna kinachomzuia.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 106
Ibara ya 107
Ibara ya 108

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali la 2

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zambi!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Nimeridhika!

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali la 3

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

## T A A R I F A

### Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2011
### *(The Public Procurement Act, 2011)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima imepitia Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 yaani *The Public Procurement Act, 2011* kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa**

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono kwa hiyo Muswada wa Ununuzi wa Umma umepita kwa kibali cha Bunge lakini bado unasubiri saini ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, nawapongeza wote waliofanya kazi kwa bidii na Waheshimiwa Wabunge wamefanya kazi kwa bidii nzuri sana kwani ndiyo kazi yenu ya kutunga Sheria. Basi nawapongeza wote pamoja na wataalamu waliohusika na Muswada huu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hatua zote zimekamilika, nilisema kwamba nawapongeza wote waliofanya kazi nzuri pamoja na Waheshimiwa Wabunge. Kazi yetu ni kutunga Sheria na hakuna mtu mwingine atakayetunga Sheria isipokuwa sisi. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa namna ambavyo mmeendesha shughuli zetu, lakini pia tuwashukuru Wataalamu mbalimbali walioshiriki katika zoezi hili pamoja na wadau, kwa hiyo nawapongeza sana. Tunaendelea Katibu!

**(Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011**
***(The Constitutional Review Act, 2011)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeona nitoe maelezo haya ili kufafanua ni nini kinafanyika kwa sasa baada ya wananchi wengi kupotoshwa na baadhi ya watu wanaojaribu kuwashawishi waandamane kuhusu upitishwaji wa Muswada huu. *(Makofi)*

Muswada huu ni Muswada wa Kawaida kama Miswada mingine yoyote ambayo tumeipitisha hapa Bungeni kwa mujibu wa Sehemu ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, masharti ya jumla ya kutunga Sheria. Huu siyo Muswada wa Marekebisho ya Katiba bali ni Muswada wenye lengo la kuwezesha kuundwa kwa Tume ya kukusanya maoni kuhusu Katiba na Kuunda Bunge la Katiba kwa madhumuni ya kuwa na Katiba mpya. Kwa hiyo, huu ni Muswada wa kuwezesha hatua nyingine ziweze kuendelea. Lengo la kuwepo kwa Tume hiyo kutawezesha wananchi kutoa maoni yao kuhusu jinsi wanavyotaka Katiba iwe na baadaye kufikia kupiga kura ya maoni yaani *referendum* kwa wananchi wanaotaka.

Kwa hiyo, kwa kupitisha Muswada huu tutawapa fursa wananchi kujadili yale wanayotaka yaingie katika Katiba yao, bila kupitisha Muswada huu hakuna namna wananchi wanaweza kuanza kutoa maoni yao kuhusu Katiba mpya. Kwa kutokutunga Sheria hii sasa kutachelewesha zoezi la kukusanya maoni ya utunzi wa Katiba mpya kinyume na matarajio ya kuanza mchakato huu mapema.

Muswada huu uliwasilishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na Kusomwa kwa Mara ya Kwanza tarehe 5 Aprili, 2011 chini ya ombi maalumu la kujadili mfululizo katika mkutano mmoja yaani ulitetwa kwa *Certificate of Urgency* baada ya kuona kwamba haukukidhi, tukaamua kwamba uahirishwe Kusomwa Mara ya Pili ukawa katika mfumo mzima wa Kusomwa Mara ya Kwanza. Kwa hiyo, kwa miezi yote hii Muswada huu ulikuwa chini ya Kusomwa Mara ya Kwanza. Kwa hiyo, Kanuni ya 86 inaruhusu Muswada huu sasa usomwe kwa Mara ya Pili.

Zipo sababu za kutosha zifuatazo kuwezesha Muswada kuendelea kwa hatua zilizobaki. Muswada ulikwishasomwa kwa Mara ya Kwanza na nikaupeleka kwenye Kamati ya Katiba ya Sheria na Utawala kwa ajili ya uchambuzi. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilikusanya maoni kutoka kwa wadau ambapo vilikuwepo vituo vitatu yaani Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar na wananchi waliokuwa karibu walijitokeza kwa wingi na kutoa maoni yao ambayo yalikuwa mengi

na yenye mwelekeo wa kukosoa kilicholetwa kwa lugha ya kuutaka Muswada huo ufanyiwe marekebisho kwenye maeneo ambayo waliona yana kasoro. Zoezi la kuendelea na kuujadili Muswada huu mfululizo liliahirishwa ili kutoa nafasi ya muda mrefu kama kuendelea na uchambuzi na kuipa nafasi Serikali kufanya marekebisho ya awali ambayo yalipatikana na kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili ili uweze kueleweka vizuri kwa wananchi na wadau wengine.

Muswada huu ulipokelewa tena na Bunge baada ya kuchapishwa upya kwa mujibu wa Kanuni ya 86(2) na Kamati na Wabunge mbalimbali kupata nafasi ya kuupitia upya. Bunge liliuchapisha kwenye magazeti yote ili kutoa nafasi kwa wadau na wananchi kuusoma ili kuwasilisha maoni yao kwenye Kamati kwa uchambuzi zaidi. Kamati ilipata nafasi ya kukutana na wadau kadhaa ambao waliwasilisha maoni yao, wengine wamewasilisha kwa maandishi ambayo mengi yamezingatiwa na Serikali. Wabunge kama wawakilishi na wananchi, nao walipata nafasi ya kuwasilisha maoni ya wananchi wao wakati wa uchambuzi katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Hivyo basi, Muswada huu umekidhi matakwa yote yaliyoainishwa katika Kanuni ya 80, 86 na 88 na hivyo unapaswa kuingia katika hatua zilizobaki ili kuwezesha mchakato wa kupata maoni ya wananchi uanze. Ni wakati huo ndiyo wananchi mmojammoja watapewa fursa ya kuuliza maswali, kutoa maoni yao na siyo katika Muswada huu kwa sababu wananchi wamewakilishwa na wadau wengi na Wabunge wao.

Waheshimiwa Wabunge, kumekuwepo na maneno kwamba sijui Muswada ukasomwe Mara ya Kwanza, hauwezi kusomwa Mara ya Kwanza kwani upo katika *stage* ya Mara ya Kwanza na tuwe wakweli kwa sababu hakuna kitu cha ajabu kuhusu Muswada huu na hao wote ambao nimewasikiliza jana, mimi mwenyewe nimekutana nao, wameleta na michango yao, ipo hapa. Kwa hiyo, tusiwapeleke wananchi wakaelewa kwamba kuna kitu kibaya kinachofanyika, hakuna kitu chochote kibaya. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tukifika katika ngazi hii ya pili mtajadili, tukifika ngazi ya Bunge Zima mtafanya *amendments* mnazozitaka kwani hiyo ndiyo haki yenu, vinginevyo hakuna sababu nyingine yoyote.

Kwa hiyo, namwita mtoa hoja asome Muswada wake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 86(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007 kwamba Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2001, yaani *"The Constitutional Review Act, 2011"* kama ulivyochapishwa upya na kama ulivyorekebishwa katika majedwali ya marekebisho yaliyo katika lugha ya Kingereza na Kiswahili, sasa usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kueleza maudhui ya Muswada ulio mbele ya Bunge lako Tukufu, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa umahiri wako katika kusimamia mchakato wa Wananchi wa kujadili Muswada huu na Kamati ya Bunge kuchambua na kujadili Muswada huu tangu ulipowasilishwa Bungeni na Kusomwa Mara ya Kwanza mwezi Aprili, 2011.

Aidha, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Mheshimiwa Angellah J. Kairuki, Makamu Mwenyekiti na wanakamati wote kwa ujumla, kwa ushirikiano wao walionipa katika kuuchambua Muswada huu kwa kina na kutoa mapendekezo na ushauri ambao umenisaidia sana katika kuboresha maudhui ya Muswada huu. Mapendekezo na ushauri wa Kamati umewezesha maandalizi ya maboresho kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho lililotolewa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo mkunjufu kabisa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Aboubakar Khamis Bakary, Waziri wa Katiba na Sheria wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa ushauri wake na ushirikiano alionipatia katika kipindi chote cha uandaaji wa Mudwada huu. Kipekee kabisa, nawashukuru wananchi wote na Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao muhimu iliyoboresha maudhui ya Muswada huu. Niwashukuru pia wataalamu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufanya kazi bila kuchoka wakati wa uandaaji wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuwepo kwa mapendekezo kwamba Muswada huu uwasilishwe na Kusomwa Mara ya Kwanza tena badala ya Kusomwa Mara ya Pili, naomba kutoa ufafanuzi kuhusu Kusomwa Mara ya Kwanza Muswada huu Bungeni. Pia naomba wale ambao wana Kanuni za Bunge wawe wananifuatilia kwa karibu ili vile vipengele ambavyo nitavitaja wavisome na kuviainisha vizuri. Pia wale wenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni vema wakawa nayo ili ninapotoa ufafanuzi wafuatilie kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa faida ya Watanzania wote wanaonisikiliza, kabla sijaenda mbali, napenda kueleza taratibu za kuwasilisha Muswada Bungeni na kwa kawaida Muswada unaletwa na Serikali Bungeni pale inaporidhika kwamba Muswada umekamilika tayari kwa kusomwa kwa mara ya kwanza Bungeni. Muswada ukishasomwa kwa Mara ya Kwanza Bungeni, Wabunge hupewa nakala za Muswada ili waweze kuyasoma maudhui na kuyaelewa yaliyomo katika Muswada huo. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 82(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, ukiangalia ukurasa wa 55, Muswada ukisomwa kwa mara ya kwanza haujadiliwi katika kikao hicho cha Bunge isipokuwa tu kama Muswada husika umetolewa kwa hati ya dharura iliyowekwa saini na Rais kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 80(4) ambayo tunaiona katika ukurasa wa 54 wa Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, sababu ya kutojadili Muswada katika mkutano ambao Muswada umesomwa kwa mara ya kwanza, ni kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge mmojammoja kurudi Jimboni na kutafuta maoni kutoka kwa wananchi ambao anawawakilisha. Kwa kufanya hivyo, Wabunge huweza kupata maoni ya wananchi wa Jimboni kuhusu Muswada uliowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya Muswada Kusomwa Mara ya Kwanza, Spika kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ambayo tunaiona katika ukurasa wa 56 wa Kanuni za Kudumu za Bunge, atapeleka Muswada kwenye Kamati yenye jukumu katika sekta inayotokana na Muswada husika. Muswada hupelekwa kwenye Kamati ili ujadiliwe, kuchambuliwa na kisha kutolewa ushauri na maoni. Pia katika kutekeleza jukumu hili, Kamati husika kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2), ambayo ipo kwenye ukurasa wa 56, inatakiwa kuwaalika wadau mbalimbali wenye utaalamu au wanaoshughulika na mambo yaliyomo ndani ya Muswada husika ili kusikia ushauri na maoni yao kwa lengo la kuisaidia katika uchambuzi wa Muswada huo. Aidha, Kamati ya Bunge husikiliza maelezo kutoka Wizara husika inayowasilisha Muswada na kutoa fafanuzi mbalimbali kutokana na ushauri, maoni ya wadau na pia maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ni katika hatua hii ya uchambuzi wa Muswada yanaweza yakatokea marekebisho ambayo, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(2) ambayo tunaiona ukurasa wa 56 na 57 yanaweza yakatokea mambo yafuatayo:-

Moja, mtoa hoja anaweza kuleta Jedwali la Marekebisho ili nalo lijadiliwe pamoja na Muswada au mbili, Kamati inaweza kumshauri mtoa hoja kufanya marekebisho na hivyo kumtaka alete jedwali la marekebisho kutokana na maoni ya wadau au wananchi kwa ujumla. Katika ngazi hii ya majadiliano kwa kuzingatia maoni ya wadau, wananchi na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Kamati aghalabu marekebisho ya Muswada hufanyika. Hivyo basi, wakati mwingine wakati marekebisho ni mengi mtoa hoja huweza kuuchapa upya Muswada kwa kuzingatia ushauri wa Kamati na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 86(10)(a) ambayo tunaipata katika ukurasa wa 58 wa Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kuchapisha upya kwa Muswada hakumzuii Mbunge yeyote au Kamati kuleta tena marekebisho kwa njia ya jedwali la marekebisho. Kwa hiyo, Muswada uliowakilishwa Kusomwa Mara ya Kwanza na kuchambuliwa na Kamati na wadau kutoa maoni yao, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali anaweza kuuchapa tena Muswada huo katika Gazeti la Serikali ili kuingiza ushauri na maoni ya wadau na Wajumbe wa Kamati kisha kuurudisha Muswada huo kwenye Kamati kwa ajili ya kuandaa maoni ya Kamati juu ya Muswada ulio mbele yao. Katika hatua hii bado mapendekezo na ushauri wa ziada unaweza kutolewa na Kamati, utaratibu huu niliousema ni wa Kikanuni na ni wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza taratibu hizi, naomba sasa nirudi kwenye Muswada ambao ninauwasilisha.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2011, uliwasilishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na Kusomwa kwa Mara ya Kwanza tarehe 5 Aprili, 2011.

Muswada huu uliwasilishwa kwenye vikao vya wadau vilivyoandaliwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ambavyo viliendeshwa Mjini Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar kati ya tarehe 7 Aprili, 2011 mpaka tarehe 9 Aprili, 2011. Baada ya kupata maoni ya Wadau, Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala ilitoa taarifa kwako na kuomba utoe muda zaidi ili wananchi waweze kuelimishwa kuhusu Muswada na vilevile Kamati iweze kuupitia Muswada kwa kina zaidi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Aprili, 2011 ulitoa maelekezo kwa Kamati kama ifuatavyo:-

(a) Muda zaidi utolewe kwa Kamati na wananchi kuufikiria Muswada huu;

(b) Muswada uchapishwe kwenye magazeti na kutangazwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari ili kutoa fursa ya kutosha kwa wananchi wengi kuuelewa na kuutolea maoni;

(c) Utangulizi wa Muswada huu uwekwe vizuri zaidi ili wananchi waelewe madhumuni ya Muswada huu kwani inaonekana wazi kwamba wananchi wengi wanadhani tayari tumeanza kuandika Katiba, kumbe lengo la Muswada huu ni kutunga Sheria ya Kuunda Tume ya Kukusanya Maoni tu; na

(d) Muswada utafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, mambo ambayo Serikali imefanya kwa maelekezo yako na kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

(a) kutoa elimu kwa wananchi kuhusu Muswada huo;

(b) kutafsiri Muswada kwa lugha ya Kiswahili; na

(c) kufanya mashauriano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, yote haya tumeyafanya na tulitoa taarifa kwako. Muswada wa Sheria ukipata mapendekezo na ushauri mwingi haubadiliki hadhi yake. Hata kama mapendekezo na ushauri huo ungesababisha Muswada kuchapishwa hata mara tano hauhitaji Kusomwa kwa Mara ya Kwanza tena. Wanaodai hivyo ama hawajui maudhui ya Kusoma kwa Mara ya Kwanza au ni upotoshwaji wa makusudi wa taratibu za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vyema watu wanapotoa hoja zao wawe wanasoma Kanuni za Kudumu za Bunge kwa sababu sisi tunaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Hata hivyo inaashiria tu mwanzo wa taratibu za Kibunge za kutunga sheria. Kuwaalika wadau kumekusudiwa kuwa upo uwezekano mkubwa Muswada kubadilika ili mradi usipoteze sababu na maudhui ya awali. Katika Muswada huu maboresho yaliyofanyika hayakubadilisha lengo la awali la Muswada huu.

Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni mashahidi na mmeuona huo Muswada, maudhui hayajabadilika hata kidogo. Katika Muswada huu, tuliwapelekea Kamati rasimu ya marekebisho mwezi Juni, 2011 kabla haujachapishwa katika Gazeti la Serikali. Kamati iliridhia Muswada uchapishwe tena na kuingiza marekebisho kabla haujawasilishwa kwa ajili kusomwa kwa mara ya pili na mara ya tatu kwa mujibu wa Kanuni ya 86(10). Kwa hiyo, wale ambao wamesema kwamba tumechakachua, Muswada huo umepitia *procedure* zile ambazo zipo katika Kanuni za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mashauriano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kati ya mwezi Aprili hadi Juni, 2011, Wizara yangu ilifanya vikao na Wizara ya Katiba na Sheria ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa lengo la kujadiliana, kushauriana na kukubaliana katika maeneo mbalimbali ya Muswada huo. Katika vikao hivyo, tulipata fursa ya kubadilishana mawazo, kupata maoni, ushauri na mapendekezo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu namna bora ya kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, masuala ya msingi yaliyojitokeza katika mashauriano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kama yafuatayo:-

(a) kwamba Sheria inayopendekezwa kutungwa isiwe ya kudumu na badala yake ikome baada ya Katiba Mpya kutungwa na kuanza kutumika; baada ya tukio hilo itungwe Sheria ya Kudumu kuhusu Tume ya Katiba na utaratibu wa kura za maoni. Ushauri huo tumeuzingatia na kuuwekea masharti katika Ibara ya 34(3) ya Muswada huu;

(b) kwamba kuwepo na masharti yanayoainisha utaratibu wa makubaliano baina ya Rais wa Jamhuri ya Muungano na Rais wa Zanzibar kuhusu uteuzi wa Wajumbe wa Tume na Katibu wa Tume. Suala hili limezingatiwa kwa mapana yake;

(c) kwamba Muswada uainishe suala la mashauriano baina ya Wanasheria Wakuu wa pande zote mbili za Muungano katika kumshauri Rais, suala hili linafanyiwa kazi na kuwekewa masharti katika Ibara ya 20(1) ya Muswada huu;

(d) kuwa Muswada uweke masharti ya kuwepo idadi sawa ya Wajumbe wa Bunge la Katiba kutoka kila upande wa Muungano. Kwa kuzingatia mapendekezo haya, suala hili limewekewa masharti kama inavyoonekana katika Ibara ya 20(2) ya Muswada huu;

(e) kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano lisigeuzwe kuwa Bunge la Katiba. Baada ya majadiliano na makubaliano ya pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano, suala hili limefanyiwa uamuzi kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 20(2) ya Muswada huu;

(f) kwamba suala la upigaji kura katika Bunge la Katiba kupitisha Muswada wa Katiba liwe ni theluthi mbili ya idadi ya Wajumbe wote kutoka pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano. Suala hili limewekewa masharti katika Ibara ya 24(3) ya Muswada huu;

(g) kuwepo utaratibu wa kupiga kura ya maoni na kupata matukio kwa kuzingatia asilimia isiyozidi 50 ya idadi ya watu waliopiga kura ya maoni kwa kila upande wa Jamhuri ya Muungano ili kuepuka kucheleweshwa kwa upatikanaji wa Katiba Mpya. Suala hili limewekewa utaratibu katika Ibara ya 32(2) ya Muswada huu;

(h) kwamba kumekuwepo masharti yanayoruhusu mashauriano ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na matumizi ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa Tanzania Bara na Daftari la Wakazi kwa Zanzibar. Suala hili limewekewa masharti katika Ibara ya 27(1) ya Muswada huu; na

(i) kwamba Sheria inayopendekezwa iainishe masharti kuhusu uwepo wa Spika, Naibu Spika na Katibu wa Bunge la Katiba. Ushauri huu umewekewa masharti katika Ibara ya 21, 22 za Muswada huu. Aidha, kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati sasa badala ya kuongozwa na Spika na Naibu Spika, Bunge Maalum litaongozwa na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, hayo ndiyo masuala ambayo tuliyojadiliana na kushauriana na wenzetu wa upande wa pili wa Muungano. Nafikiri Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kwamba hoja na masuala mengi yaliyojiliwa katika vikao vya mashauriano katika pande mbili hizi za Muungano yamezingatiwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo mahsusi ya wadau yaani wadau wote kwa ujumla. Tumetenganisha maoni mahsusi na maoni ya ujumla. Maoni mahsusi ni kama yafuatayo:-

(a) Muswada kuandikiwa kwa lugha ya Kiswahili;

(b) Jina fupi la Muswada kuitwa Sheria ya Katiba Mpya ya Mwaka 2011 au Sheria ya Kuunda Tume ya Katiba ya Mwaka 2011;

(c) Rais kutokuwa na madaraka ya kuteua Wajumbe wa Tume na kutoa hadidu za rejea;

(d) Ibara ya 9(2) kuzuia wananchi kujadili na kuyatolea maoni mambo yaliyooanishwa katika Ibara hiyo; na

(e) Vyama vya Siasa kutoshiriki katika Kampeni za Kura za Maoni.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu moja moja kama ifuatavyo:-

Kuhusu maelekezo ya Muswada kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili, suala hili limetekelezwa. Hata hivyo Kanuni ya 144 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2007 inaelekezwa kwamba lugha rasmi ya Bunge ni Kiswahili au Kiingereza. Kwa kawaida japo si sheria, Miswada mingi inayowasilishwa Bungeni isipokuwa Katiba ya Nchi imekuwa ikiandikwa kwa lugha ya Kiingereza na kujadiliwa kwa lugha ya Kiswahili au zote kwa pamoja.

Aidha, kifungu cha 84 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya Kwanza, inaeleza kwamba lugha rasmi ya sheria ni Kiswahili na Kiingereza lakini panapotokea mgongano, toleo la lugha ya Kiingereza litakuwa ndio mwongozo katika tafsiri Mahakamani na mahali pengine popote. Hadi sasa, hakuna istilahi na msamiati maalum wa maneno ya Kiswahili yaliyojaribiwa katika Mahakama yaani *"Judiciary Tested".* Hata kwa wenzetu upande wa Zanzibar, tafsiri ya Muswada kwa lugha ya Kiswahili huandikwa kwa madhumuni ya majadiliano kwenye Baraza la Wawakilishi. Baada ya hapo nakala inayopelekwa kwa Mheshimiwa Rais kuwekewa saini inapelekwa kwa lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jina fupi la Muswada, Serikali inaendelea kupendekeza ibaki kama ilivyoandikwa hapo awali kwa sababu ni kwamba jina hilo linatoa maana pana inayoonyesha kwamba Sheria inayopendekezwa inakusudia kuunda Tume, kuainisha hadidu za rejea, kuweka utaratibu wa kuwepo Mabaraza ya Katiba, kuunda Bunge Maalum la kujadili na kupitisha Katiba inayopendekezwa ili wananchi wapigie Kura ya Maoni. Vilevile Muswada unapendekeza utaratibu wa Kura ya Maoni na uzinduzi wa Katiba Mpya. Hivyo basi, kwa maoni ya Serikali, mapendekezo yaliyotolewa na wadau hayatoi taswira ya madhumuni mapana ya sheria inayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mamlaka ya Rais. Kwa mujibu wa Ibara ya 33(1), Rais ndiye Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amri Jeshi Mkuu. Kwa kuzingatia Ibara hiyo, suala la kutungwa Katiba ya Nchi ni vyema likasimamiwa na mwenye mamlaka yeye binafsi na si kukasimu kwa namna yoyote ile, kwa chombo au mamlaka nyingine yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzoefu wa nchi nyingine, tumefanya utafiti katika nchi nyingine. Kwa mfano nchi ya Kenya, Tume iliundwa na Rais, nchi ya Zambia, Tume iliundwa na Rais na nchi ya Uganda, Tume iliundwa na Waziri wa Katiba na Sheria. Wenzetu Ghana Tume ya Kukusanya Maoni ya Wananchi imeundwa na Rais. Kama Waheshimiwa Wabunge tulivyoelekezwa na watoa mada wakuu katika semina kuhusu Muswada wa Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011, ni vizuri tukabadili mitazamo yetu kuhusu Rais. Hapa Rais haangaliwi kama Mkuu wa Mhimili wa Utawala bali ni Mkuu wa Nchi yaani *Head of State. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ibara ya 9(2) ya Muswada. Serikali imeboresha kwa kuondoa maneno yaliyokuwa yanaleta ukakasi ambao ulisababisha baadhi ya wananchi kudhani kuwa masuala yaliyoorodheshwa katika Ibara ya 9(2) wamezuia kuyajadili. Aidha, Ibara ndogo ya (3) imeongezwa ili kutoa ufafanuzi wa kile kinachokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, suala la Vyama vya Siasa kufanya kampeni ya kura ya maoni. Kilichofanyika katika Muswada huu ni kuondoa suala la kufanya kampeni na badala yake Vyama vya Siasa na Taasisi zisizo za kiserikali zilizosajiliwa Tanzania na kuendeshwa na raia wa Tanzania zishirikiane na Tume na Serikali kuhamasisha wananchi kuipigia Kura ya Maoni ya ama kukubali au kuikataa Katiba inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie kipengele hiki. Badala yake tumeweka hivi, Vyama vya Siasa, Taasisi Zisizo za Kiserikali zilizosajiliwa Tanzania na kuendeshwa na raia wa Tanzania zishirikiane na Tume na Serikali kuhamasisha wananchi kupiga kura ya maoni ya ama kuikubali au kukataa Katiba inayopendekezwa. Hapo tuna-*avoid* Taasisi za Nje zisije zikatuingilia katika kujadili Katiba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni na michango ya ujumla ya wadau yalikuwa ni *specific issues* au maoni ya ujumla ambayo wananchi wengi waliyatoa. Sasa maoni mengine yamegusa katika sehemu mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) kwamba jina la Muswada libadilishwe hiyo nimeshaizungumzia;

(b) kuna maneno muhimu ya kuongezewa tafsiri, hilo tumesema Serikali imelizingatia lakini baadhi ya tafsiri na istilai na misamiati imeingizwa lakini mengine tafsiri zake ziko kwa mujibu wa Jamhuri ya Muungano;

(c) kuwa madhumuni yote ya Muswada yaainishwe kwa kuweka masharti rasmi ili kwenda sambamba na Muswada, masuala ya muafaka wa Kitaifa liwe ni moja ya madhumuni ya Muswada. Mapendekezo haya na ushauri huo umefanyiwa kazi na kuainishwa katika masharti na maeneo husika na suala la muafaka wa Kitaifa limeongezwa kama ilivyoanishwa kwenye madhumuni Ibara ya 4 (j);

(d) kwamba Tume isiundwe na Rais na Wajumbe wa Tume wateuliwe na kuthibitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano; Ushauri huo kama nilivyosema hapo juu kwamba Mkuu wa nchi ndiye mwenye mamlaka ya kufanya hivyo;

(e) kuwa hadidu za rejea zitolewe na Rais, lakini zijadiliwe na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Ushauri huu umepokelewa na Serikali na kwa hiyo hadidu za rejea zimewekwa kwenye Muswada katika Ibara ya 8 ya Muswada huu;

(f) kwamba idadi ya Wajumbe wa Tume ni kubwa sana itasababisha gharama kubwa. Sisi kama Serikali tumeliangalia hilo, tumesema kulingana na majukumu ya Tume na ukubwa wa Jamhuri ya Muungano, idadi ya Wajumbe si kubwa kama ilivyoonekana. Hivyo basi ushauri huu sisi kama Serikali hatukuk;ubaliana nao, tumesema tubaki na Wajumbe wa Tume walewale;

(g) kwamba suala la kukiuka Kanuni za Maadili liwe ni moja ya vigezo vya kutengua ujumbe wa Mjumbe wa Tume. Suala hili limefanyiwa kazi kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 12;

(h) kwamba sifa za Katibu wa Tume na zianishwe kwenye Muswada. Ushauri huu umefanyiwa kazi kama ilivyoanishwa kwenye Ibara ya 13(3) ya Muswada huu;

(i) kwamba gharama za Tume zisimamiwe na Serikali na si Waziri na kwamba Wajumbe wa Tume washirikishwe katika kuamua viwango vya maslahi na posho zao. Kwa utaratibu na sheria, kazi hiyo ya kuangalia maslahi ya Tume na Watumishi ni mamlaka ya Waziri husika;

(j) kwamba Wajumbe wa Tume wasiwe na kinga, ila katika eneo hili, wananchi walitofautiana, kuna wanaosema kwamba kuwepo na kinga na kuna ambao wanashauri kwamba kinga hiyo iboreshwe. Hivyo basi, kwa kuwa huu ni utaratibu wa kawaida katika

utekelezaji wa majukumu ya umma, kinga ya Wajumbe imeboreshwa zaidi kama ilivyoainishwa kwenye Ibara ya 15;

(k) kwamba mpangalio wa Ibara ya 16, 17 na 18 uangaliwe upya. Suala hilo limefanyiwa kazi kwa kuhamisha masharti ya Ibara ya 16 kuwa masharti ya Ibara ya 18. Aidha, Ibara ya 17 na 18 sasa zimeunganishwa na kuwa Ibara ya 16 ya Muswada huu ambayo kwa sasa hivi ni mojawapo ya hadidu za rejea;

(l) kwamba ripoti iwasilishwe kwa wananchi na si kwa Rais na Rais asiwe na mamlaka ya kubadili ripoti ya Tume. Serikali imelitafakari suala hili na kuona kwamba kwa kuwa Rais ni Mkuu wa Nchi na ndiye atakayeunda Tume, ni dhahiri kwamba ripoti ya Tume inapaswa kuwasilishwa kwake ili yeye kwa kutumia Waziri mwenye dhamana ya Katiba aweze kuwasilisha kwenye Bunge Maalum;

(m) kuwa kiundwe chombo kitakachounda Bunge Maalum la Katiba kwa kushirikiana na Bunge la Jamhuri ya Muungano na vyama vya kiraia. Pia Rais asiteue Wajumbe Wabunge Maalum wa Bunge la Katiba, ushauri huu sisi kama Serikali tumezingatia na utaona mabadiliko katika aya ya 20 ya Muswada huu;

(n) kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano lisiwe na uwezo wa kujigeuza kuwa Bunge la Katiba na badala yake liundwe Bunge mahususi la Katiba. Serikali imekubaliana na maoni hayo na yamezingatiwa katika aya ya 20 ya Muswada huu;

(o) kwamba Muswada uainishe utaratibu wa kujadili majina ya wanaopendekezwa kuwa Wajumbe wa Bunge la Katiba yapitishwe na Bunge la Jamhuri ya Muungano. Suala hili tumeliainisha katika Ibara ya 20 kwa hiyo hakuna tatizo tena;

(p) kwamba Mamlaka ya Bunge ya Katiba yasikome mara tu baada ya kutungwa kwa Katiba mpya na kwamba yawepo masharti ya kumwezesha Rais kuitisha tena Bunge la Katiba. Ushauri huu umefanyiwa kazi kama ulivyoainishwa katika Ibara ya 32(3) na Ibara ya 32(4) ya Muswada huu;

(q) kwamba Muswada uweke masharti yatakayoainishwa hatma ya Katiba mpya endapo wananchi watapiga kura ya hapana kwa asilimia kubwa zinazohitajika kisheria. Ushauri huu tumeuzingatia sisi kama Serikali na kuweka masharti kwenye Ibara ya 32 na mwisho; na

(r) kwamba vyama vya siasa viruhusiwe kushiriki katika kampeni za kura za maoni. Ushauri huu umefanyiwa kazi na kuainishwa katika Ibara ya 29(2).

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu sita. Sehemu ya Kwanza ina Ibara ya kwanza, ya pili na ya tatu zenye masharti ya utangulizi yanayohusu Jina la Sheria inayopendekezwa, tarehe ya kuanza kutumika na matumizi ya Sheria inayopendekezwa. Sehemu hii inaendelea kutoa tafsiri ya baadhi ya misamiati, maneno yalitotumika na mamlaka zilizotajwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili ni Ibara ya nne. Ibara ya nne inaweka masharti yanayohusu madhumuni ya Muswada. Sehemu hii inaainisha kwa undani madhumuni ya chimbuko la mchakato wa mabadiliko ya Katiba ikijumuisha viapo na yamini za Wajumbe wa Tume na Sekretarieti na utaratibu wa kuendesha mchakato wa mabadiliko ya Katiba utakavyofanywa. Katika sehemu hii inadhihirisha kwamba madhumuni ya Muswada huu si kutungwa kwa Katiba mpya kama ilivyopotoshwa na baadhi ya watu. Ni dhahiri kwamba lengo la Sheria inavyopendekezwa ni kuweka utaratibu wa kuratibu mchakato wa kukusanya maoni kwa ajili ya kuunda Tume itakayokusanya maoni ya wananchi na taratibu nyingine ambazo zitawezesha nchi yetu kupata Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu ni Ibara ya tano mpaka ya 19. Sehemu hii ndiyo inayochukua nafasi kubwa ya Muswada huu ambayo ina masharti ya kuanzishwa kwa Tume,

utaratibu wa kukusanya maoni na Ibara ya 5, 6 na 7 zinahusu uundwaji wa Tume, uteuzi wa Wajumbe wa Tume na Muundo wa Tume. *(Makofi)*

Tume itaundwa na Rais baada ya kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar na kwa ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar. Wajumbe wa Tume watatoka katika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano kwa idadi sawa na majina yao kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. *(Makofi)*

Ibara ya 8 inaainisha masharti kuhusu hadidu za rejea, kuwa ni zile zilizoanishwa katika Ibara ya 9 na Ibara ya 16 ya Muswada huu. Aidha, kazi na majukumu ya Tume, uhuru wa Tume katika utekelezaji wa kazi na majukumu yake, viapo na yamini za Wajumbe na ukomo wa Wajumbe wa Tume ni masuala ambayo pia yameainishwa kwa kina katika sehemu hii. Sanjari na hilo sehemu hii pia inaainisha mambo ambayo yanapaswa kuzingatiwa na kulindwa katika mchakato wa ukusanywaji wa maoni kutokana na umuhimu wa uzito wake katika Taifa letu. Kwa hiyo, Ibara ya 9, 13, 14 na Ibara ya 15 zinaweka masharti yanayohusu uwepo wa Sekretarieti ya Tume, gharama za Tume na Kinga kwa Wajumbe wa Tume na Sekretarieti.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne yenye Ibara ya 16, 17, 18 na 19 inahusu utaratibu wa utendaji kazi wa Tume pamoja na kuanisha kazi, wajibu na mamlaka ya Tume. Sehemu hii inataka Tume kutayarisha ripoti ambayo itaambatishwa na rasimu ya Muswada wa Katiba na kuwasilisha kwa Rais na Rais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Sehemu ya Tano ina Ibara ya 20, 21, 22, 23, 24, 25 na 26 zenye masharti yanayohusu uundwaji wa Bunge Maalum la Katiba na Ibara ya 20 mpaka ya 22 zinahusu tamko la kuundwa kwa Bunge Maalum, Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum, Katibu na watumishi wengine wa Bunge Maalum. Bunge Maalum la Katiba litaundwa na Rais baada ya kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar baada ya kupata ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar. Mamlaka ya Bunge Maalum, masharti kuhusu Bunge hilo, Kanuni zake na ukomo wa mamlaka wake yameainishwa katika Ibara ya 23, 24, 25, na 26. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita yenye Ibara ya 27, 28, 29, 30 na 31, 32, 33 na 34 inahusu uhalalishaji wa Katiba kupitia kura ya maoni ambapo haki ya wananchi kupiga kura ya maoni kwa kuzingatia Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 1984 imeanishwa. Katika kutekelezwa masharti hayo, wananchi watahamasishwa kupitia vipindi maalum vitakavyoendeshwa na vyama vya kiraia, vyama vya siasa na Tume yenyewe. *(Makofi)*

Kwa mujibu wa Ibara ya 27, Kura ya Maoni itaendeshwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushirikiana na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ambapo Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa upande wa Tanzania Bara na Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa upande wa Tanzania Zanzibar yatatumika. Kwa mujibu wa Ibara ya 32, matokeo ya Kura ya Maoni yataamuliwa kwa asilimia isiyopungua 50 ya jumla ya kura zote zilizopigwa kutoka Tanzania Bara na asilimia 50 ya jumla ya kura zote zilizopigwa kutoka Tanzania Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masharti ya kuvunjwa kwa Tume yameanishwa katika Ibara ya 33 ambapo Rais atatoa amri kupitia Gazeti la Serikali la kuvunja Tume. Katiba Mpya itabainisha tarehe ya kuanza kutumika na namna Rais atakavyozindua na kuanza kutumika. Masharti hayo yameainishwa katika Ibara ya 34 ya Muswada huu. Sheria hii inayopendekezwa itakoma kutumika na masharti yake yatapoteza nguvu ya kisheria mara tu baada ya kuzinduliwa kwa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kutungwa kwa Katiba Mpya ni muhimu kwa kila mwananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sisi Wabunge ni viongozi na wawakilishi wa wananchi na kwa sababu hiyo tunao wajibu wa kuielewa Sheria hii inayopendekezwa na kuelewa mchakato wote wa kukusanya na kuratibu maoni ya wananchi kuhusu Katiba Mpya. Hadi sasa wananchi wameshirikishwa kwa mapana kupitia makongamano, mikutano, vikao vya kukusanya maoni, vyombo vya habari na hadhara zinazofanana na hivyo na kwa kiasi kikubwa

mapendekezo mengi kama nilivyosoma kwenye hotuba yangu yamezingatiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya Muswada huu kupitishwa na kuwa Sheria wananchi wote watapewa muda mrefu wa kujadili, kutoa maoni na jinsi gani Katiba yao wanataka iwe. Niwahakikishie Watanzania wote kwamba kila mwananchi atafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kuchukua fursa hii kuwasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu na kutoa fursa kwa Bunge lako Tukufu kuujadili na kutoa mapendekezo yake ili hatimaye Muswada huu uweze kuwa Sheria itakayoanzisha safari ya kuelekea katika upatikanaji wa Katiba Mpya. *(Makofi)*

Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa mara nyingine kwa kuusimamia kwa kikamilifu mchakato wa kutungwa kwa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2011 na sina shaka kwa uongozi wako Waheshimiwa Wabunge watajadili na hatimaye kuupitisha Muswada huu utakaowezesha kuwepo kwa Sheria hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia kwako napenda kuwashukuru Wabunge wote kwa kunisikiliza na naomba waujadili na kuupitisha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ambayo imejadili Muswada huu atoe maoni ya Kamati. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Tunaendelea na kazi hakuna mwongozo sasa hivi. Tunaenda na ratiba. *(Makofi)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo baadaye.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, unatunyima haki.

**SPIKA:** Ninakunyima haki, ninayo Kanuni inayosema Mwongozo ni baada ya jambo fulani kutokea. Kwa sasa hivi naomba nimalize hatua hizi. Nimalize hatua hizi na ninyi mtakapomaliza basi. *(Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa hii kama ilivyosambazwa Bungeni iingie kama ilivyo kwenye *Hansard,* na mimi nitatoa *executive summary,* kwa kifupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza kazi hii muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu hadi kukamilika kwa taarifa ninayoiwasilisha leo mbele ya Bunge lako Tukufu. Kamati yangu imeuchambua Muswada huu kwa kina na kwa kuzingatia amali na maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la mwaka 2007 niweze kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kuuleta Muswada huu kwenye Kamati yangu. Muswada huu unalenga kuweka utaratibu utakaowezesha Taifa letu kupata Katiba Mpya. *(Makofi)*

Madhumuni makuu ya Muswada huu ni kuunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba itakayoratibu na kukusanya maoni ya wananchi juu ya Katiba Mpya. Aidha, Muswada huu unaainisha utaratibu wa namna ya kuchambua maoni ya wananchi na masharti kuhusu Mabaraza ya kutoa ushauri juu ya rasimu ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu pia unaweka masharti juu ya utayarishaji na uwasilishaji wa ripoti kuhusu maoni ya wananchi; utaratibu wa kuunda Bunge Maalum; uendeshaji wa kura ya maoni na masharti yanayohusiana na masuala hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu uliwasilishwa katika Bunge hili na kusomwa kwa mara ya kwanza mnamo tarehe 5 Aprili, 2011 na kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007 uliuleta kwenye Kamati yangu kwa ajili ya utekelezaji wa hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa Kamati ilitekeleza jukumu hilo kwa kuzingatia umuhimu na upekee wa Muswada huu toka nchi yetu ilipopata Uhuru wake mwaka 1961. Kamati yangu iligawanyika katika makundi matatu yaliyokwenda Dar es Salaam, Zanzibar na Dodoma kwa lengo la kutoa fursa kwa wananchi kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu kati ya tarehe 7 mpaka 9 Aprili, 2011. Kutokana na vikao hivyo, Kamati ilipokea maoni na mapendekezo ya wananchi kuhusu Muswada huu ambayo kwa kiasi kikubwa yamesaidia kuuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa fursa kwa wananchi kwa kuzingatia misingi mikuu ifuatayo; Katiba ni mali ya wananchi na si ya kundi lolote katika jamii, na kwa mantiki hiyo ni vyema kuwashirikisha kuanzia hatua za awali. Vilevile kwa kuzingatia kuwa Katiba ni ya wananchi, ilibidi wapewe nafasi ya kutosha ya kutoa maoni juu ya Muswada wa Sheria itayakayounda vyombo vitakavyoendesha mchakato wa kupata Katiba Mpya. Hii ni fursa nzuri na ya kipekee ya kuimarisha umoja na mshikamano wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa dhamira ya dhati ya kuruhusu mchakato wa mabadiliko ya Katiba uanze kupitia tamko alilolitoa katika hotuba yake ya mwisho wa mwaka aliyoitoa Desemba 31, 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inamshukuru pia Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Jaji Frederick Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalamu wa Ofisi yake na wale wa Wizara ya Katiba na Sheria, kwa ushirikiano wao kwa Kamati. *(Makofi)*

Aidha, Kamati yangu inapenda kuliarifu Bunge lako na Watanzania kwa ujumla kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati na wadau mbalimbali kwa kuuboresha Muswada na kwa kuutangaza tena kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza na pia kuuchapisha katika magazeti mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu mwezi Aprili mwaka huu, Kamati imepokea maoni mengi na mazuri kutoka kwa wadau ikiwa ni pamoja na Taasisi za Kiraia, Vyuo vya Elimu ya Juu, Vyama vya Siasa na wataalam waliobobea katika masuala ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa taasisi za kiraia ambazo Kamati ilipokea maoni yake ni pamoja na *TUCTA, NOLA, LHRC, WLAC, TAWLA, TGNP, TLS,* Mfuko wa Mwalimu Nyerere na Jukwaa la Katiba na Chama cha Majaji Wastaafu Tanzania. *(Makofi)*

Kwa upande wa Vyuo vya Elimu ya Juu, ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Zanzibar, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo cha Mipango na Chuo cha Elimu ya Biashara Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu viliwasilisha maoni yao kwa Kamati, tunawashukuru sana. Kamati pia inawashukuru watalaam wa masuala ya Sheria na Katiba waliofika mbele ya Kamati na kutoa ushauri na mapendekezo ya kitaalam. Miongoni mwao ni Profesa Issa Shivji, Profesa Paramagamba Kabudi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Romwald Haule kutoka Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini Ruaha, Jaji Joseph Warioba na Msajili wa Vyama Vya Siasa, Mheshimiwa John Tendwa. *(Makofi)*

Aidha, kwa upekee kabisa, Kamati yangu inapenda kuwashukuru wananchi ambao walifika mmoja mmoja mbele ya Kamati na wale waliotoa maoni yao kwa njia ya maandishi na kwa njia ya mtandao kwa lengo la kuboresha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni ambayo Kamati iliyapata kutoka kwa makundi hayo yaliisaidia kuuboresha Muswada huu na hivyo kujiridhisha kwamba, ni sahihi kwa kuletwa Bungeni kwa ajili ya Kusomwa Mara ya Pili na Mara ya Tatu kwa mujibu wa Kanuni ya 84 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2011, kwa kuzingatia maoni ya kitaalam kuhusiana na utungaji wa Sheria, Kamati imejiridhisha kwamba ni lazima kuzingatia masharti ya Katiba iliyopo. Kamati yangu ilijiridhisha kuhusu masuala ya msingi yakiwemo kasoro za kisheria zinazokusudiwa kuboreshwa na kurekebishwa kwa kuzingatia masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwa mantiki hiyo sasa ninayo heshima kuwasilisha maoni yafuatayo kuhusiana na sehemu mbalimbali za Muswada:-

Mheshimiwa Spika, jina refu la Muswada; kwa kutambua kwamba jina refu ndilo linabeba maudhui yote ya Muswada, Kamati ilifanya uchambuzi na kupendekeza matumizi sahihi ya maneno kwa kufuta baadhi ya maneno na kuingiza maneno mengine mapya.

Kamati inapendekeza maneno “kuainisha masharti” yafutwe na badala yake yawekwe maneno “kuweka utaratibu.” Pia maneno “kuhalalisha masharti yaliyomo kwenye” yafutwe na badala yake yawekwe maneno “kutoa ushauri juu ya.”

Kamati pia inapendekeza “Bunge la Katiba” lililopo kwenye jina refu sasa liitwe “Bunge Maalum.” Sababu za mapendekezo hayo ni kwamba nchi yetu haijawahi kuwa na Bunge la Katiba bali Bunge Maalum kama inavyosomeka kwenye aya ya tatu ya sehemu ya utangulizi wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo inatamkwa kwamba “Kwa hiyo basi Katiba hii imetungwa na Bunge Maalum…”

Kutokana na mapendekezo haya, Kamati inapendekeza jina refu la Muswada lisomeke; “Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kuunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa madhumuni ya kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi juu ya Katiba; kuainisha na kuchambua maoni ya wananchi; kuainisha masharti kuhusu Mabaraza ya kutoa ushauri juu ya rasimu ya Katiba; kuweka masharti juu ya utayarishaji na uwasilishaji wa ripoti kuhusu maoni ya wananchi; kuweka utaratibu wa kuunda Bunge Maalum, uendeshaji wa kura ya maoni na kuweka masharti yanayohusiana na mambo hayo. “

Mheshimiwa Spika, jina fupi la Muswada; kwa kuzingatia kwamba jina fupi hutoholewa kutoka katika jina refu, Kamati imeridhika jina fupi la Muswada huu liendelee kuwa “Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011.”

Mheshimiwa Spika, tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii; Kamati inaafiki tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii ibakie Desemba 1, 2011 kwani itaharakisha kuanza kwa mchakato wa kupata Katiba Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Sheria; Kamati inaafiki mapendekezo ya sheria hii kwamba itumike Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, tafsiri; Kamati kwa kutambua umuhimu wa tafsiri sahihi ya maneno yaliyotumika katika Muswada huu, inapendekeza maneno yafuatayo yawekewe tafsiri ili kuondoa mkanganyiko. Katika tafsiri ya neno "Mabaraza" maneno "Muswada wa" ambayo yako mstari wa mwisho yafutwe na sehemu hiyo isomeke "Rasimu ya Katiba" badala ya "Muswada wa rasimu ya Katiba." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu ya mapendekezo hayo ni kwamba, maoni ya wananchi yatakayokusanywa na Tume ni kwa ajili ya kuandaa "Rasimu ya Katiba" na siyo "Muswada wa Rasimu ya Katiba."

Kamati inashauri maneno Bunge Maalum, Gazeti la Serikali, Mwenyekiti wa Tume na Mwenyekiti wa Bunge Maalum yawekewe tafsiri ili yaweze kueleweka vizuri kwa sababu hayapo kwenye sehemu ya tafsiri. Kwa mujibu wa aya ya tatu ya sehemu ya utangulizi kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inatamkwa kwamba "Kwa hiyo basi Katiba hii imetungwa na Bunge Maalum."

Mheshimiwa Spika, madhumuni; kuhusu Ibara ya 4(a) Kamati inapendekeza kufuta maneno "itakayokusanya na kuratibu" na badala yake kuweka maneno "itakayoratibu na kukusanya" na hivyo kuifanya ibara hiyo isomeke "Kuweka utaratibu wa kuunda Tume itakayoratibu na kukusanya maoni ya wananchi."

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 4(h), Kamati inapendekeza yaongezwe maneno "Vyama vya Siasa na makundi mengine kama ambavyo Tume itaona inafaa" baada ya maneno "Mashirika ya Kidini" ili kuifanya ibara hiyo isomeke "Kuweka utaratibu kuhusu namna ambavyo Tume itakusanya maoni kutoka kwa Taasisi za Umma na Binafsi, Vyama vya Hiari, Mashirika ya Kidini na Vyama vya Siasa na makundi mengine kama ambavyo Tume itaona inafaa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu ya mapendekezo haya ni kwamba, Ibara hiyo kwa sasa hairuhusu Vyama vya Siasa kutoa maoni mbele ya Tume.

Mheshimiwa Spika, vilevile Ibara ya 4(l) neno "kuunda" lifutwe badala yake liwekwe neno "kuitisha." Sababu ya mapendekezo haya ni kwamba, kwa mujibu wa Ibara ya 20 ya Muswada huu tayari muundo wa Bunge Maalum unajulikana na hivyo Rais atakachofanya ni kuliitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 4(m) ya Muswada unazungumzia uwepo wa "Spika" na "Naibu Spika" kama viongozi wa Bunge Maalum. Badala ya maneno hayo Kamati inashauri matumizi ya maneno "Mwenyekiti" na "Makamu Mwenyekiti," kwa sababu Bunge Maalum kwa kawaida huendeshwa na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mabadiliko hayo sasa yataifanya Ibara hiyo isomeke, "kuweka mfumo utakaowezesha uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum…"

Mheshimiwa Spika, uundaji wa Tume; Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Muswada kwamba Rais kwa mamlaka yake kama Mkuu wa Nchi aachiwe madaraka ya kuunda Tume anayopewa na Ibara ya 36 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Aidha, Kamati inapendekeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wasitajwe katika Ibara hii kwa sababu wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Katiba za pande zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yameainishwa katika Ibara ya 59(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, yameanishwa katika Ibara ya 56 ya Katiba ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uteuzi wa Wajumbe wa Tume; Kamati inapendekeza kwamba Ibara ya 6(3)(c) ambayo inatamka kwamba kigezo kimojawapo cha uteuzi ni "maslahi ya umma" kifutwe kwa sababu hata isipotajwa Rais atazingatia suala hilo wakati wa uteuzi. Aidha, Ibara ya 6(3)(e) ambayo inaelekeza kwamba katika kufanya uteuzi wa Wajumbe wa Tume, Rais atazingatia "vigezo vingine ambavyo ataona vinafaa" ifutwe ili kuondoa utata wa uhalali wa uteuzi nje ya vigezo vilivyotajwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Ibara ya 6(4)(a) Kamati inashauri neno "zote" liongezwe baada ya neno "ngazi" na maneno "ya Taifa, Mkoa au Wilaya," yaondolewe.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya yataifanya Ibara hiyo kusomeka "mtu hatakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume endapo mtu huyo ni kiongozi wa chama cha siasa katika ngazi zote." Sababu za mapendekezo ni kwamba Ibara hii inazuia viongozi wa Vyama vya Siasa katika ngazi za Taifa, Mkoa na Wilaya tu kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume. Aidha, Kamati inapendekeza Ibara ya 6(4)(c) iboreshwe ili kuondoa dhana ya kumhukumu mtu ambaye hajatiwa hatiani hasa kwa kuzingatia Ibara ya 13(6)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, muundo wa Tume: Katika Ibara ya 7(c) Kamati inakubaliana na idadi ya juu ya Wajumbe 30 iliyopendekezwa kwenye Muswada, hata hivyo inapendekeza idadi ya chini ya Wajumbe hao isipungue 20. Sababu ya mapendekezo hayo ni kwamba ni vyema kutoa mwongozo wa idadi ya chini na idadi ya juu ya Wajumbe ambao wanaweza kuteuliwa.

Mheshimiwa Spika, hadidu za rejea; kwa kuzingatia umuhimu wa Muswada huu, Kamati inapendekeza hadidu za rejea ziwe sehemu ya Muswada huu kupitia jedwali *"schedule"* ili kurahisisha mabadiliko pale itakapobidi.

Mheshimiwa Spika, sababu ya mapendekezo hayo ya Kamati ni kwamba hiyo itarahisisha mabadiliko kufanyika bila kuhitaji kwenda Bungeni na pia italeta uwazi wa hadidu hizo kufahamika kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inapendekeza iwekwe Ibara ndogo baada ya Ibara ya 8(3) ambayo itaipa Tume mamlaka na uhuru wa kufanya kazi iwapo itahitaji kwenda nje ya hadidu za rejea zilizoainishwa kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kazi za Tume; Kamati inapendekeza kwamba neno "watu" kama lilivyotumika katika Ibara ya 9(1)(b) lifutwe na badala yake liwekwe neno "Wananchi."

Mheshimiwa Spika, mabadiliko hayo yataifanya Ibara hii sasa isomeke "Kupitia na kutafiti usahihi na ulinganifu wa masharti ya Kikatiba yanayohusu mamlaka ya wananchi, mifumo ya kisiasa, demokrasia, utawala wa sheria na utawala bora."

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza iwepo Ibara ndogo baada ya Ibara 9(1)(d) inayotamka kwamba miongoni mwa majukumu ya Tume ni pamoja na "Kuandaa Rasimu ya Katiba." Sababu ya mapendekezo haya ni kwamba Tume ndiyo itakayokuwa na jukumu la kuandaa Rasimu ya Katiba, itakayopelekwa katika Bunge Maalum.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati inapendekeza kufutwa kwa neno "itazingatia" katika Ibara ya 9(2) na badala yake liwekwe neno "itaongozwa." Pia maneno "na kwa mantiki hiyo" yafutwe na hivyo kuifanya Ibara hiyo isomeke "katika kutekeleza masharti ya Ibara ndogo ya (1), Tume itaongozwa na misingi mikuu ya Kitaifa na maadili ya jamii ya kuhifadhi na kudumisha mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inapendekeza katika Ibara ya 9(2)(f) yaongezwe maneno “wenye sifa ya” katikati ya maneno “wote” na “kupiga kura,” na hivyo kuifanya Ibara hiyo isomeke “uchaguzi wa kidemokrasia wa mara kwa mara katika vipindi maalum kwa kuzingatia haki ya watu wote wenye sifa ya kupiga kura.” Sababu za mapendekezo haya ni kwamba si kila mtu anaweza kupiga kura isipokuwa yule mwenye sifa zilizowekwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza Ibara 9(2)(i) iandikwe upya, badala ya kusomeka “uhuru wa kuabudu na uvumilivu wa dini nyingine” sasa isomeke “uwepo wa Jamhuri ya Muungano isiyokuwa na dini na inayoheshimu uhuru wa kuabudu.” Sababu ni kwamba, dhana ya uvumilivu inayotajwa katika Muswada si rahisi kutekelezeka na inaweza kuwa chanzo cha migogoro ya kidini.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati inapendekeza Ibara ya 9(3) iboreshwe kwa kufuta maneno “vifungu vidogo vya (1)” katika mstari wa kwanza na badala yake yawekwe maneno “Ibara ndogo ya (2).” Pia neno “watu” katika mstari wa tatu lifutwe kabla ya maneno “kutoa maoni” na badala yake liwekwe neno “wananchi.” Mabadiliko hayo yataifanya ibara hiyo isomeke “kwa madhumuni ya Ibara ndogo ya (2) na kwa jambo lolote lingine muhimu kwa Taifa, Tume itatoa fursa kwa wananchi kutoa maoni yao kwa uhuru kwa lengo la kuendeleza na kuboresha masuala hayo.”

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya Tume; katika Ibara ya 10, Kamati inashauri maneno “kwa kadri itakavyokuwa muhimu” yafutwe Ibara hiyo isomeke “Tume itakuwa na mamlaka na uhuru chini ya Sheria hii na haitaingiliwa na mtu au mamlaka yoyote.” Sababu ya mapendekezo haya ni kwamba “kwa kadri itakavyokuwa muhimu” yataleta utata wa tafsiri kwani ni vigumu kupima vigezo vya “umuhimu.”

Mheshimiwa Spika, Kiapo cha Wajumbe na Katibu; Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Muswada kwamba, Wajumbe wa Tume wale kiapo au yamini mbele ya Rais kwa utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Spika, ukomo wa Ujumbe; Kamati inapendekeza katika Ibara ya 12(1)(d) yaongezwe maneno “kama zilivyoainishwa katika jedwali la pili la Sheria hii” ili kuifanya isomeke “kuondolewa kwa makosa ya kukiuka kanuni za maadili kama zilivyoanishwa katika jedwali la pili la Sheria hii.”

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Ibara ya 12(3) Kamati inapendekeza maneno “au sekretarieti” yafutwe baada ya neno “Tume” na hivyo Ibara hii isomeke “Mjumbe wa Tume ambaye atakiuka masharti ya Kanuni za Maadili atapoteza sifa za kuendelea kuwa mjumbe.”

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti; Kamati inashauri kwamba, baada ya Ibara ya 13(2) iongezwe Ibara ndogo inayopendekeza uwepo wa “Naibu Katibu wa Tume” na vilevile ianishwe jinsi atakavyopatikana. Sababu ya mapendekezo hayo ni kwamba katika Jedwali la kwanza sehemu ya pili ya Muswada huu inaonesha kiapo au yamini ya Katibu au Naibu Katibu.

Mheshimiwa Spika, gharama za Tume; Kamati inapendekeza katika Ibara cha 14(1) yaongezwe maneno “ya Serikali” baada ya neno “Hazina’ ili Ibara hiyo isomeke “Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.” Sababu za mapendekezo haya ni kuweka usahihi katika jina la mfuko huo, kama inavyosomeka katika Ibara ya 135 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Ibara ya 14(2) Kamati inapendekeza maneno “kadri ya Waziri atakavyoamua kulingana na” katika mstari wa pili yafutwe na badala yake maneno “mujibu wa” yaingizwe ili kuifanya ibara hiyo isomeke “Wajumbe wa Tume na Sekretarieti watalipwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za nchi.” Sababu ya mapendekezo hayo ni kwamba, Serikali hufanya malipo kwa mujibu wa sheria na taratibu za fedha.

Mheshimiwa Spika, kinga kwa Wajumbe wa Tume na Sekretariati; Kamati imeridhika na masharti yaliyomo katika Ibara ya 15 na hivyo kuridhia ibaki jinsi ilivyo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa utendaji; Kamati inashauri katika Ibara ya 16(4)(b) ziongezwe Nyaraka za Azimio la Arusha na Matamko ya Rais wa Zanzibar *(Presidential Decrees)* katika orodha ya nyaraka ambazo Tume itazipitia na kuzichambua. Sababu za mapendekezo haya ni kwamba, hizo ni miongoni mwa nyaraka muhimu ambazo zinaweza zikawa rejea nzuri kuhusiana na historia ya mabadiliko ya Katiba yetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Ibara ya 16(8) Serikali ifafanue namna Mabaraza ya Katiba yatakavyofanya kazi na muda mahsusi ambao Rasimu ya Katiba itaanza kuandikwa. Sababu za mapendekezo haya ni kuweka uwazi katika zoezi zima la utendaji kazi wa Mabaraza.

Mheshimiwa Spika, uwasilishaji wa ripoti; Kamati inashauri Ibara ya 18(2) iboreshwe kwa kufuta maneno "masuala ya kisera na" na kuweka maneno "Mwenyekiti wa Tume" badala ya neno "Waziri" hivyo kuifanya Ibara isomeke "Baada ya kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar na baada ya kukamilisha majadiliano kuhusu taratibu za kiutendaji, Rais atamuagiza Mwenyekiti wa Tume kuwasilisha Muswada wa Katiba katika Bunge Maalum."

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inashauri Muswada ueleze ni baada ya muda gani baada ya Rais kupokea Ripoti ya Tume, atapeleka Rasimu ya Katiba kwenye Bunge Maalum. Kutokana na mapendekezo hayo, Ibara hii sasa itasomeka "Rais atamuagiza Waziri kwa kushirikiana na Tume kuwasilisha Rasimu ya Katiba katika Bunge Maalum."

Mheshimiwa Spika, makosa na adhabu; katika Ibara ya 19(1) Kamati inashauri kuongezwa kwa maneno "au taasisi" baada ya neno "mtu"; neno "potosha" baada ya neno "atakayemkwamisha" na pia "kwa makusudi" baada ya neno "Sekretarieti" lililopo katika mstari wa tatu wa Ibara hii. Vilevile neno "kumkwaza" lifutwe ili kuondoa utata wa tafsiri yake ambayo inaweza kusababisha likatumika vibaya. Mapendekezo hayo yataifanya Ibara hiyo isomeke "Mtu au Taasisi itakayokwamisha, potosha au kumzuia Mjumbe wa Tume au Sekretarieti kutekeleza majukumu au kutekeleza mamlaka ya Tume au Sekretarieti kwa makusudi atakuwa ametenda kosa."

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inashauri Muswada huu uweke utaratibu wa namna ambavyo mashauri yatakayokuwa Mahakamani na ambayo yatakuwa hayajawasilishwa Mahakamani kutokana na kukiukwa kwa sheria hii, yatakavyoendelea baada ya Sheria hii kumaliza matumizi yake na hivyo kupoteza nguvu za kisheria.

Mheshimiwa Spika, tamko la Bunge la Katiba; Kamati inapendekeza Muswada uondokane na dhana ya uundwaji wa Bunge la Katiba na badala yake itumike dhana ya uitishwaji wa Bunge hilo kwani kwa kwa mujibu wa Ibara ya 20(2) ya Muswada huu muundo wa Bunge hilo tayari unajulikana.

Vilevile Kamati inapendekeza maneno Wanasheria Wakuu wa pande mbili za Muungano wasitajwe katika Ibara hii kwani majukumu yao yanajulikana. Kutokana na mapendekezo yaliyotolewa hapo juu, yanafanya Ibara hii ya 20(1) sasa kusomeka; "Rais, baada ya kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar, kwa kupitia Tangazo la Serikali ataitisha Bunge Maalum." Kamati pia inashauri Muswada huu ueleze muda ambao Bunge Maalum litaanza kazi tangu kuitishwa kwake na Rais kupitia Tangazo la Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Ibara 20(2) Kamati inashauri vifungu vya 20(2)(c) na 20(2)(d) vifutwe kwa minajili iliyoelezwa hapo juu, hivyo mabadiliko hayo yataifanya Ibara ndogo ya 20(2)(e) kuwa 20(2)(c). Aidha, katika Ibara ya 20(2)(e) Kamati inaishauri Serikali itoe ufafanuzi kuhusiana na namna idadi ya Wajumbe 116 ilivyofikiwa na pia jinsi watakavyopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Ibara ya 20(2)(e) Kamati inashauri makundi mengine katika jamii yaongezwe. Miongoni mwa makundi hayo ni vyama vya wafanyakazi, wakulima, wavuvi na wafanyabiashara. Hii itasaidia makundi hayo kushiriki katika Bunge Maalum kwa kuzingatia taswira ya kijiografia na uwiano wa makundi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Ibara ya 20(2)(v) Kamati inaishauri Serikali kutoa ufafanuzi wa dhana ya "makundi yenye mahitaji maalum katika jamii" ili kuondoa mgongano kwani haijawekwa wazi vigezo vinavyotumika kuainisha makundi yenye mahitaji maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika Ibara ya 20(3) Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Muswada kwamba, idadi ya Wajumbe wa Bunge Maalum kutoka Tanzania Zanzibar inayotajwa, haitapungua theluthi moja ya Wajumbe wote wa Bunge Maalum, iwe kwa makundi yote ya Wajumbe yanayotajwa katika aya za (a) hadi (e). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuongeza Ibara ndogo baada ya Ibada ya 20(4) ambayo itaainisha utaratibu wa kuitisha Bunge Maalum, ikieleza muda na mahali ambapo Bunge hilo litakutana.

Mheshimiwa Spika, Spika na Naibu Spika wa Bunge la Katiba; katika Ibara ya 21 kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa hapo awali, Kamati inaona ni vyema Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, wakaongoza Bunge Maalum badala ya Spika na Naibu Spika. Aidha, Kamati inashauri iandaliwe rasimu ya Kanuni za Bunge Maalum itakayokuwa na viapo kwa viongozi wa Bunge hilo kama inavyoelezwa katika Ibara ya 21(4).

Mheshimiwa Spika, Katibu na Watumishi wa Bunge Maalum; katika Ibara ya 22(3) Kamati inapendekeza Katibu na Naibu Katibu wa Bunge Maalum watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa Kanuni na sio kama inavyoelekezwa katika Ibara hii kuwa watatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa "maelekezo ya Spika au Naibu Spika kadri itakavyokuwa."

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Bunge la Katiba; Kamati inapendekeza Ibara ya 23(2) ifutwe kwa sababu dhana inayotajwa kuhusiana na "Mamlaka ya Bunge kutunga masharti ya Katiba" kutokana na mabadiliko hayo Ibara ya 23 itasimama yenyewe bila Ibara ndogo.

Mheshimiwa Spika, masharti kuhusu Bunge la Katiba; katika Ibara ya 24(1) Kamati inapendekeza kufutwa kwa maneno "linaweza kuandaa" na badala yake liwekwe neno "litaandaa" na hivyo kuifanya Ibara hiyo isomeke "Bunge Maalum litaandaa Kanuni kwa kwa ajili ya kuendesha shughuli za Bunge Maalum."

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inapendekeza Ibara 24(2) ifutwe na badala yake iwekwe Ibara ya 24(3) na ichukue nafasi ya Ibara hii. Kamati yangu pia inashauri kuwa Ibara hii itamke kuwa siyo kila kifungu cha Rasimu ya Katiba kitakuwa na umuhimu sawa. Hivyo basi, Kamati inashauri yawepo masharti ya kuhitaji kuungwa mkono kwa theluthi mbili kwa mambo ya msingi tu sawa na Nyongeza ya Pili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mmwaka 1977. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bunge la Katiba; Kamati inashauri Ibara ya 25(2) iandikwe upya na hivyo isomeke; "Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge Maalum, na kwa madhumuni hayo, Bunge la Jamhuri ya Muungano litatunga Sheria mahsusi itakayowapa kinga Wajumbe wa Bunge Maalum." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kukoma kwa mamlaka ya Bunge la Katiba; kuhusiana na Ibara ya 26(2) Kamati inakubaliana na madaraka ya Rais kuitisha tena Bunge Maalum katika siku zijazo kwa ajili ya kutunga masharti ya Katiba kabla ya kuzindua Katiba inayopendekezwa. Kamati pia inapendekeza madaraka hayo ya Rais yawekwe pia katika Ibara ya 32 kupitia Ibara ndogo ya (5). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa kura ya maoni; kuhusu Ibara ya 27 Kamati inashauri itungwe Sheria mahsusi itakayosimamia si tu kura ya maoni, bali hata kutumika kwa masuala mengine yatakayohitaji kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, swali la kura ya maoni; Kamati inashauri kuwa Ibara 28(1) inayosomeka "ndani ya siku saba baada ya kuchapishwa kwa Katiba, Tume ya Taifa ya Uchaguzi... "neno

“Katiba” litamkwe kuwa ni “Katiba inayopendekezwa,” kwa sababu neno “Katiba” limetafsiriwa kama Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. *(Makofi)*

Vilevile kwenye mstari wa mwisho yaongezwe maneno “litakalotolewa na” baada ya neno “swali.” Pia yaongezwe maneno; “na wananchi” ili Ibara hiyo isomeke; “swali litakalotolewa na kuamuliwa na wananchi kwa kura ya maoni.”

Mheshimiwa Spika, baada ya ushauri wa hapo awali kuridhiwa Ibara ya 28(2) ifutwe kwa sababu swali linalorejewa katika kura ya maoni litamtaka mpigakura kueleza endapo anaridhia Katiba au la, hivyo jambo hilo halihitaji mashauriano kati ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa ya uendeshaji wa kura ya maoni; katika Ibara ya 29(1) Kamati inashauri neno; “itaainisha” kama lilivyo kwenye mstari wa nne lifutwe na kuwekwa maneno; “itatangaza taarifa itakayoainisha” hivyo kuifanya Ibara hiyo isomeke; “Ndani ya siku kumi na nne baada ya kuchapishwa kwa swali katika Gazeti la Serikali, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushirikiana na Tume ya Uchaguzi Zanzibar itatangaza taarifa itakayoainisha.”

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati yangu inapendekeza Ibara ya 29(2) ya Muswada ifafanue kuwa elimu ya uraia inayotamkwa hapa ni “elimu ya uraia juu ya Katiba inayopendekezwa.”

Mheshimiwa Spika, aidha, maneno “atatoa taarifa” katika Ibara 29(3) yaondolewe na kuwekwa maneno “atawataarifu wananchi wa eneo analohusika nalo” na hivyo kifungu hicho kitasomeka; “ndani ya siku ishirini na moja baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutangaza taarifa, msimamizi wa uchaguzi wa kila jimbo la uchaguzi atawaarifu wananchi wa eneo analohusika nalo kuhusu utaratibu wa uendeshaji wa kura za maoni.”

Mheshimiwa Spika, haki ya kupiga kura ya maoni; Kamati ilipendekeza kuwa katika Ibara cha 30 mstari wa tatu maneno; “la wakazi” yaondolewe na kuwekwa “daftari la wapiga kura wa Zanzibar.” Hivyo Ibara hiyo itasomeka; “Mwananchi ambaye jina lake limeingizwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lililoanzishwa chini ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na Daftari la Wapiga Kura wa Zanzibar…”

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuendesha kura ya maoni; Kamati inashauri Serikali itoe ufafanuzi juu ya maneno “Marekebisho yatakayolazimu” kama inavyoonekana kwenye mstari wa nne wa Ibara ya 31. Sababu ya mapendekezo haya ni kuondoa utata wa tafsiri unaoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kura ya maoni; katika Ibara ya 32(2) Kamati inashauri liongezwe neno “halali” kila baada ya neno “kura zote” ili Ibara hiyo isomeke “Matokeo ya kura ya maoni yataamuliwa kwa msingi wa kuungwa mkono kwa asilimia inayozidi hamsini ya jumla ya kura zote halali zilizopigwa kutoka Tanzania Bara na asilimia inayozidi hamsini ya jumla ya kura zote halali zilizopigwa kutoka Tanzania Zanzibar.”

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Ibara ya 32(2), Kamati inaishauri Serikali kufanya utafiti ili kujua ni mchakato utakaofuatia ili kupata suluhisho *“exit clause”* iwapo upande mmoja wa Muungano utashindwa kupata zaidi ya nusu ya kura za kuunga mkono Katiba inayopendekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati inashauri busara iliyotumika katika Ibara 32(2) ya kuunga mkono kwa zaidi ya asilimia hamsini ya kura zote halali zilizopigwa itumike pia kwenye Ibara ya 24(3) ya Muswada huu kuhusiana na kupitishwa kwa Katiba Inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Ibara ndogo iongezwe baada ya Ibara ya 32(4) ya Muswada huu kuelezea iwapo wingi wa kura ya maoni utakuwa ni hapana, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 itatumika kwa muda gani kabla ya kuanza tena kwa mchakato wa kupata Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba, iongezwe Ibara ndogo ya 32(5) ambayo itaelezea busara iliyotumika katika Ibara ya 26(2) kuhusiana na kumpa Rais mamlaka ya kuliitisha tena Bunge Maalum, Ibara hiyo isomeke; "Kuvunjwa na kukoma kwa mamlaka ya Bunge la Katiba hakutachukuliwa kuwa kunaondoa mamlaka ya Rais kuliitisha tena Bunge Maalum lenye Wajumbe wale wale siku zijazo... kwa lengo la kurekebisha masharti yaliyomo kwenye Katiba iliyopendekezwa."

Mheshimiwa Spika, sababu za ushauri huu ni kwamba, hatua hii itasaidia kushughulikia masuala yaliyo na mgogoro katika Katiba inayopendekezwa kwa lengo la kuirekebisha ili Katiba hiyo ipate kuhalalishwa tena na wananchi kupitia kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, kuvunjwa kwa Tume; Kamati inashauri maneno "baada ya" katika Ibara 33(1) yaongezwe mwanzoni kabisa kabla ya neno "matokeo" ili kuleta maana sahihi, na hivyo isomeke; "baada ya matokeo ya kura ya maoni kutangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Rais kwa kupitia amri iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, ataivunja Tume."

Mheshimiwa Spika, kuanza kutumika kwa Katiba; Kamati inapendekeza katika Ibara 34(4) itamkwe wazi iwapo kutakuwa na mgongano kati ya Sheria iliyo katika Toleo la Kiswahili na ile iliyopo katika Toleo la Kiingereza, ni ipi itazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, sasa napenda kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati hii waliochambua Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi Chana, Mwenyekiti, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe ni Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mheshimiwa Rashidi Ali Abdallah, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Azza Hilall Hamad, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mheshimiwa Abas Mtemvu, Mheshimiwa Nimrod Mkono na Mheshimiwa Tundu Lissu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe binafsi kwa kutupatia ushauri na miongozo mbalimbali ambayo imetuwezesha kukamilisha kazi hii muhimu kwa uhai wa Taifa letu. Napenda pia kumshukuru Dokta Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge na timu yake yote iliyotusaidia katika jukumu hili. Hususani niwataje Makatibu wa Kamati, Ndugu Peter Magati, Ndugu Deogratias Egidio, Ndugu Chacha Nyakega na Ndugu Brown Mwangoka, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii inakamilika. *(Makofi)*

Pia tunatambua na kuthamini mchango mkubwa uliotolewa na Catherine Kitutu na Pauline Mavunde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Muswada huu. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika, Mungu libariki Bunge letu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu! *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, hoja ya kuahirisha mjadala!

**SPIKA:** Utaahirishaje? Mimi nimemwita Mheshimiwa Tundu Lissu. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. LISSU – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba maoni nitakayoyasema huku Bungeni na yale ambayo watapatiwa Waheshimiwa Wabunge, yaingizwe katika *Hansard* ili niweze ku-*summarize* kwa haya ambayo nimeyaandika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spiika, tarehe 11 Machi, 2011 Serikali ilichapisha Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011 katika Gazeti la Serikali la tarehe hiyo. Muswada huo ulipelekwa katika Mkutano wa Tatu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa Hati ya Dharura. Hata hivyo, baada ya upinzani mkubwa dhidi ya Muswada huo kujitokeza karibu nchi nzima, Bunge lililazimika kuondoa Hati ya Dharura na hivyo kufanya Muswada kushughulikiwa kwa mujibu wa utaratibu wa kawaida wa kutunga sheria uliowekwa na Kanuni za 80, 83 na 84 za Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano, Toleo la mwaka 2007. *(Makofi)*

Katika kufanya hivyo, Bunge kwa kupitia Spika liliiagiza Serikali kufanya mambo yafuatayo kwa mujibu wa Taarifa Rasmi ya Majadiliano Katika Bunge *(Hansard)* ya Kikao cha Nane cha Mkutano wa Tatu cha tarehe 15 Aprili 2011. *(Makofi)*

Kwanza muda zaidi utolewe kwa Kamati na wananchi kuufikiria Muswada huu. Katika kufanikisha hili, Serikali iandae Muswada huu kwa lugha ya Kiswahili ili wananchi wenyewe waweze kusoma yaliyomo kwenye Muswada huo badala ya kupewa tafsiri tu na watu wengine. *(Makofi)*

Pili, Muswada uchapishwe kwenye magazeti na kutangazwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari ili kutoa fursa ya kutosha kwa wananchi wengi kuuelewa na kuutolea maoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, utangulizi wa Muswada huu uwekwe vizuri zaidi ili wananchi waelewe madhumuni ya Muswada huu, kwani imeonekana wazi wananchi wengi wanadhani tayari tumeanza kuandika Katiba, kumbe lengo la Muswada huu ni kutunga Sheria ya Kuunda Tume ya Kukusanya maoni tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutoa maagizo haya, Bunge lilisitiza kwamba Muswada huu upo ndani ya Bunge, haupo Serikalini. Hii ni kwa sababu, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Bunge, Muswada ulikwishasomwa kwa mara ya kwanza na kupelekwa kwenye Kamati inayohusika kwa ajili ya kuanza kujadiliwa. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) Kamati ilikwishaanza kupokea maoni ya wadau kwa lengo la kuisaidia katika uchambuzi wa Muswada huo. Kazi iliyokuwa imebaki kwa Kamati ilikuwa ni kutumia mamlaka yake chini ya Kanuni ya 84(3) kufanya marekebisho katika Muswada wa Sheria kwa kumshauri Waziri anayehusika na Muswada huo kufanya mabadiliko. Ni baada tu ya kupata ushauri wa Kamati kuhusu mabadiliko ndio Serikali ingeweza kuleta Jedwali la Mabadiliko kwa lengo la kufanya mabadiliko katika hatua hii kabla Muswada haujaletwa Bungeni kwa ajili ya kusomwa mara ya pili na kwa mjadala wa Bunge zima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna hata moja ya maagizo haya ya Bunge ambalo limetekelezwa na Serikali. Hata tafsiri ya Kiswahili ya Muswada ambayo imeletwa Bungeni ililetwa kwenye Kamati wiki mbili zilizopita baada ya Muswada kufanyiwa mabadiliko na Serikali bila kujali Kanuni ya 84(3) ya Kanuni za Bunge inayotaka Serikali kupata ushauri wa Kamati kwanza. Pamoja na kuonyesha imesainiwa tarehe 8 Machi, 2011 sawa na Muswada wa zamani uliopigiwa kelele sana na wananchi ililetwa kwenye Kamati wiki mbili zilizopita, ikiwa ni wiki moja baada ya Kamati kukataa kuujadili Muswada Mpya kwa vile ulifanyiwa mabadiliko na Serikali bila kupata ushauri wa Kamati kama inavyotakiwa na Kanuni ya 83(4) ya Kanuni za Bunge. Badala ya kutekeleza maagizo ya Bunge, Serikali imeleta Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011 ambao ulichapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 14 Oktoba, 2011.

Aidha, Kamati imeingiliwa mno katika kazi zake na wewe Mheshimiwa Spika. Kwanza; kwa kuikatalia Kamati ruhusa ya kwenda Mikoani kukusanya maoni ya wananchi kama ilivyokuwa imeomba mara mbili;

Pili, kwa kuilazimisha Kamati kujadili Muswada huu mpya ambao Kamati ilikuwa imekataa kuufanyia kazi kwa sababu ya ukiukwaji wa Kanuni za Bunge; na tatu, kwa kuiongezea Kamati wajumbe wa ziada watano bila kujali masharti ya Kanuni ya 113(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. *(Makofi)*

Muswada huu mpya una tofauti kubwa na za kimsingi na Muswada wa zamani kama nitakavyoonyesha hapa. Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, mabadiliko makubwa

na ya kimsingi yaliyofanywa kwenye Muswada wa zamani yalihitaji na bado yanahitaji mjadala wa Kitaifa wa wananchi kama ambavyo wengi wamedai katika mijadala inayoendelea nchi nzima. Aidha, Bunge hili Tukufu lilihitaji, na bado linahitaji, muda zaidi wa kuyatafakari mabadiliko haya makubwa na ya kimsingi katika Muswada wa zamani. Katika mazingira haya, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini ni busara na ni *sound policy* kwa Muswada huu Mpya kusomwa mara ya kwanza ili kuruhusu mjadala unaohitajika kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mabadiliko ya Katiba; kama ilivyokuwa kwa Muswada wa zamani, Muswada huu unapendekeza kuundwa kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba ambayo kwa mujibu wa utangulizi wa Muswada, itawajibika kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi juu ya Katiba (na) kuainisha na kuchambua maoni ya wananchi. Kwa mujibu wa Ibara ya 5, Tume hii itaundwa na Rais kwa kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar, na kwa ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar. Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 6(1), Rais atateua Wajumbe wa Tume kwa kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Ibara ya 6(2) inapendekeza kwamba muundo wa Tume utazingatia msingi wa kuwepo kwa uwakilishi ulio sawa kwa kila upande wa Jamhuri ya Muungano. Pendekezo hili linarudia, kwa njia iliyojificha zaidi, msimamo wa Ibara ya 6(2) ya Muswada wa zamani iliyokuwa imeweka wazi kwamba idadi ya wajumbe wa Tume itakuwa sawa kwa sawa kwa pande zote za Jamhuri ya Muungano! Kama ilivyokuwa kwa Muswada wa zamani, Ibara ya 7(2) ya Muswada inapendekeza kwamba uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti utafanyika kwa msingi kwamba iwapo Mwenyekiti atatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, basi Makamu Mwenyekiti atakuwa mtu anayetoka upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Muundo wa Tume unakamilishwa na Sekretarieti ya Tume itakayoongozwa na Katibu. (Ibara ya 13(1) kwa mujibu wa Ibara ya 13(2), Katibu huyo atateuliwa na Rais baada ya kukubaliana na Rais wa Zanzibar. Watendaji wengine wa Sekretarieti watateuliwa na Waziri kwa makubaliano na Waziri mwenye dhamana ya mambo ya Katiba wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kumpa Rais baada ya makubaliano na Rais wa Zanzibar mamlaka ya kutoa hadidu za rejea za Tume na muda wa kukamilisha na kuwasilisha ripoti. (Ibara ya 8(1) na kama hali itahitaji kufanya hivyo, Rais “kwa makubaliano na Rais wa Zanzibar” anaweza kuongeza muda usiozidi miezi mitatu ili kuwezesha Tume kukamilisha na kuwasilisha ripoti. (Ibara ya 8(2) hadidu za rejea, kwa mujibu wa Ibara ya 8(3), “... zitakuwa ni hati ya kisheria ambayo Tume itaizingatia katika utekelezaji wa majukumu na utumiaji wa mamlaka yake kwa mujibu wa Sheria hii.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 9(1) ya Muswada inaelezea kazi za Tume kuwa ni pamoja na:-

(a) Kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi;

(b) Kupitia na kutafiti usahihi na ulinganifu wa masharti ya Kikatiba yanayohusu mamlaka ya watu, mifumo ya kisiasa, demokrasia, utawala wa sheria na utawala bora;

(c) Kutoa mapendekezo kwa kila hadidu ya rejea; na

(d) Kuandaa na kuwasilisha ripoti.

Mheshimiwa Spika, ijapokuwa haijaainishwa hivyo, ni wazi kwa mujibu wa wa Ibara ya 17(1)(d) na (2) ya Muswada kwamba moja ya kazi za Tume ni kuandaa Rasimu ya Muswada wa Katiba Mpya. Mapendekezo ya Muswada kuhusu Tume ya Mabadiliko ya Katiba ni muhimu na yanazua maswali mengi yanayohitaji mjadala wa Kitaifa na maamuzi ya wananchi. Maeneo haya muhimu ni pamoja na nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano katika mchakato mzima wa kutengeneza Katiba Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Rais; kama ambavyo tumepata kusema ndani ya Bunge hili, kwa muda wote wa uhai wetu kama Taifa huru, mfumo wetu wa Kikatiba na wa kisiasa umejengwa juu ya nguzo kuu ya Urais wa Kifalme *(Imperial Presidency).* Hii inatokana na ukweli kwamba katika mfumo huu, Rais ana madaraka makubwa sana ya kiutendaji na ya kiutungaji sheria. Vilevile Rais ana kivuli kirefu cha Kikatiba juu ya mahakama kwa kutumia mamlaka makubwa aliyonayo katika uteuzi wa viongozi wote wa ngazi za juu za Mahakama. Urais wa Kifalme ndio chanzo kikuu cha kukosekana kwa uwajibikaji katika ngazi zote za Serikali na ndio kichocheo kikubwa cha rushwa na ufisadi wa kutisha ambao umefanywa kuwa ni sehemu ya kawaida ya maamuzi ya Kiserikali ya nchi yetu. Sio vibaya, katika kuthibitisha jambo hili, kurudia maneno ya Ibara ya 37(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977: "... Rais atakuwa huru na hatalazimika kufuata ushauri atakaopewa na mtu yeyote...." Na kama alivyowahi kusema Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere kwenye mahojiano ya mwaka 1978 na Shirika la Habari la Uingereza *(BBC),* kama Rais wa Tanzania alikuwa na mamlaka kwa mujibu wa Katiba na sheria za nchi yetu ya kuwa dikteta! *(Makofi)*

Muswada mpya unaendeleza kivuli kirefu cha Urais wa Kifalme katika mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya. Mtu mwenye mamlaka ya kidikteta, kama Rais alivyo kwa mujibu wa Katiba ya sasa, hawezi kusimamia upatikanaji wa Katiba ya kidemokrasia. Kwa kutumia mamlaka makubwa ya uteuzi wa Tume yanayopendekezwa na Muswada huu, ni wazi Rais Kikwete, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama Tawala cha CCM, atateua wajumbe anaowataka yeye na Rais Dokta Ali Mohamed Shein, Makamu wake ambaye pia ni Rais wa Zanzibar! Ni wazi vilevile kwamba watu watakaoteuliwa na Marais hawa ni watu wasiokuwa tishio kwa *status quo* kwa maana ya kupendekeza mabadiliko makubwa katika mfumo wa Kikatiba na kiutawala na hivyo kuhatarisha maslahi ya CCM!

Mheshimiwa Spika, hali ni hiyo hiyo kwa Sekretarieti ya Tume ambayo ndio chombo cha kiutendaji na moyo wa Tume yenyewe. Kama Katibu ambaye ndiye Mtendaji Mkuu wa Tume ni mteuliwa wa Rais na ni mtumishi wa Serikali; kama watendaji wengine wa Tume ni watumishi wa Serikali walioteuliwa wa Waziri ambaye naye ni mteuliwa wa Rais baada ya kukubaliana na Waziri mwenzake wa Zanzibar; na kama watumishi wengine wa Tume nao ni watumishi wa Serikali kama inavyopendekezwa na Ibara ya 13 ya Muswada Mpya, ni wazi, kwa hiyo, kwamba mapendekezo haya yote ya uteuzi wa wajumbe, watendaji na watumishi wengine wa Tume yana lengo moja tu kuhakikisha kwamba matokeo ya kazi ya Tume hiyo ni yale tu yanayotakiwa na Rais na Serikali yake na chama chake cha CCM.

Mheshimiwa Spika, badala ya mapendekezo haya ya Muswada Mpya, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza utaratibu wa kidemokrasia zaidi katika uteuzi wa Tume. Kwanza, badala ya Tume hiyo kuwa "Tume ya Rais" kama inavyopendekezwa katika Muswada, tunapendekeza iwe "Tume ya Vyama" *(Multiparty Commission)* kwa maana moja kubwa, Wajumbe wa Tume wateuliwe kufuatana na mapendekezo na makubaliano ya vyama vya siasa vyenye uwakilishi Bungeni, vyama vingine vilivyosajiliwa pamoja na mashirika ya kijamii, taasisi za kitaaluma na za kidini. Hii haina maana kwamba Wajumbe wa Tume hiyo hawatatakiwa kuwa na sifa zilizoainishwa katika Ibara ya 6(3) ya Muswada Mpya. La hasha! Wajumbe wa Tume ya Vyama watatakiwa kuwa na sifa zozote za kitaaluma zinazotakiwa ili kuwawezesha kufanya kazi ya kitaalamu kama inavyopendekezwa na Muswada Mpya. *(Makofi)*

Pili, baada ya uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Vyama, inapendekezwa kwamba Wajumbe walioteuliwa kwa mashauriano na makubaliano kama tunavyopendekeza watatakiwa wathibitishwe na Bunge la Jamhuri ya Muungano. Pendekezo hili litahakikisha kwamba Wajumbe wa Tume wanakuwa *vetted* na chombo kikuu cha uwakilishi wa wananchi. Hili litajenga kuaminiana baina ya Serikali, vyama vya siasa, mashirika ya kijamii, taasisi za kitaaluma na za kidini na litaipa Tume ya Mabadiliko ya Katiba uhalali mkubwa wa kisiasa, kitu ambacho ni muhimu katika mazingira ya sasa ya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tofauti pekee na muhimu kati ya pendekezo la Muswada Mpya na pendekezo letu kuhusu mamlaka ya uteuzi wa Wajumbe wa Tume ni *locus* ya uwajibikaji wao. Wajumbe wanaoteuliwa na Rais wanakuwa na shinikizo la kutoa matokeo yatakayompendezesha Rais au chama chake. Wajumbe wanaotokana na mapendekezo na makubaliano ya wadau

wengi na wanaothibitishwa na chombo cha uwakilishi cha wananchi kama tunavyopendekeza hawawezi kuwa na shinikizo la kutoa matokeo yatakayompendezesha mmojawapo wa wadau hao. Faida kubwa na ya wazi ya Tume ya Vyama ni kwamba matokeo ya kazi yake yana nafasi kubwa zaidi ya kukubaliwa, kuheshimiwa na kutekelezwa na wadau mbalimbali kuliko matokeo ya kazi ya Tume ya Rais. Kwa lugha nyingine, kazi ya Tume ya Vyama itakuwa na uhalali wa kisiasa *(political legitimacy)* mkubwa zaidi kuliko Tume ya Rais.

Pendekezo hili linawahusu Katibu, watendaji na watumishi wengine wa Tume vilevile. Kutokana na uzoefu uliotokana na historia yetu na mfumo wetu wa kiutawala na Kikatiba, watumishi wa Serikali wamekuwa hawana uhuru wa kufanya maamuzi kwa kuzingatia utashi wao na uadilifu wa kitaaluma bali hufanya maamuzi kwa kuzingatia matakwa ya mabosi wao wa kisiasa. Hii ni kwa sababu, kisheria na hata kivitendo, watendaji na watumishi karibu wote wa umma hujiona wanawajibika kwa mamlaka zao za uteuzi yaani Rais na/au Waziri. *(Makofi)*

Aidha, watendaji na watumishi hawa wanawajibika kinidhamu kwa mamlaka zinazoongozwa na watendaji wa Serikali ambao nao ni wateuliwa wa Rais na kwa hiyo wanakuwa na woga wa kufanya maamuzi yanayoweza kuhatarisha maslahi ya kisiasa ya Rais na Chama Tawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hizo, ni muhimu kwa watendaji na watumishi wote wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba wawe huru dhidi ya mashinikizo yoyote ya kisiasa kutoka kwa Rais na Serikali yake na chama chake. Ili Tume iwe na mamlaka na uhuru unaohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake na ili isiingiliwe kweli na mtu au mamlaka yoyote kama inavyosema Ibara ya 10 ya Muswada, inabidi mamlaka ya uteuzi yaondolewe katika mikono ya Rais na/au Waziri ambaye ni mdau mmojawapo tu wa wadau wengi wa mchakato wa Katiba Mpya. Na namna ya pili ya kuhakikisha uhuru huu unakuwepo ni kuweka utaratibu wa kuwapata watendaji na watumishi hawa nje kabisa ya utumishi wa Serikali kwa kuweka masharti ya kuwataka waombe kazi, kufanyiwa usaili na kuteuliwa na jopo la wataalamu walio huru.

Mheshimiwa Spika, namna ya tatu ya kuhakikisha uhuru wa Tume katika kutekeleza majukumu yake ni kuhakikisha wajumbe wake wanapatiwa ulinzi wa ajira zao *(security of tenure)* sawa na wanaopatiwa majaji wa Mahakama ya Tanzania ili kuzuia uwezekano wa Wajumbe kuondolewa kwa sababu zisizotokana na utendaji wao wa kitaaluma au ukosefu wa maadili. Kwa maana hiyo, mapendekezo ya Ibara ya 10 Muswada Mpya juu ya uhuru wa Tume hayatoshelezi hata kidogo. Hii ni kwa sababu Ibara ya 12 ya Muswada Mpya ambayo inazungumzia ukomo wa ujumbe wa Tume, haijaweka utaratibu wowote wa namna ya kushughulikia nidhamu ya Wajumbe pale kunapokuwepo tuhuma za ukiukaji wa Kanuni za Maadili zinazopendekezwa katika Ibara ya 12(2) na Jedwali la Pili la Muswada. Kutokuweka utaratibu huu kuna hatari kubwa kwani kisheria mamlaka ya uteuzi huwa ndio mamlaka ya nidhamu pale ambapo sheria haijaweka utaratibu tofauti wa nidhamu. Hii ina maana kwamba bila kuweka utaratibu wa kisheria wa nidhamu ya Wajumbe wa Tume, Rais ndiye atakuwa na uwezo wa kuwaondoa madarakani kwa sababu yeye ndiye aliyewateua!

Mheshimiwa Spika, pendekezo letu la tatu linahusu hadidu za rejea. Hapa kuna hoja za aina mbili. Kwanza, sambamba na pendekezo la kutompa Rais madaraka ya uteuzi wa Wajumbe wa Tume, Rais asipewe mamlaka ya kutoa hadidu za rejea kwa Tume. Pili, kwa vile kama inavyopendekezwa katika Muswada Mpya hadidu za rejea ni hati ya kisheria inayotakiwa kuzingatiwa na Tume katika utekelezaji wa majukumu yake, ni muhimu hati hii iwekwe wazi katika sheria yenyewe badala ya kubakia kuwa siri ya Rais. Watanzania lazima wajue Tume inapewa majukumu gani ya kisheria. Aidha, Wajumbe wa Tume wenyewe lazima wafahamu wanapewa majukumu gani ya kisheria na wafahamu kwamba wanatakiwa kufuata matakwa ya sheria na sio maelekezo ya mtu mmoja hata kama ni Rais wa Kifalme. Hii itasaidia uwajibikaji wa Tume kwa wananchi kwani itakuwa rahisi kupima matokeo ya kazi ya Tume kwa hadidu za rejea zilizowekwa wazi katika sheria.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba badala ya kumsubiri Rais kutoa hadidu za rejea, tayari Ibara za 9 na 16 za Muswada Mpya zimeshafanya hivyo kwa kuainisha kazi za Tume, mipaka ya Tume katika utekelezaji wa kazi hizo na utaratibu wa namna ya kuzifanya. Kwa ajili hiyo, zaidi ya

kutaka kuonyesha kwamba Rais ana mamlaka makubwa katika mchakato mzima wa upatikanaji wa Katiba Mpya, mapendekezo ya Ibara ya 8 hayana maana wala sababu yoyote na yanaweza kuondolewa bila kuathiri maudhui ya Muswada.

Aidha, kwa kuzingatia mapendekezo ya Ibara ya 9, haijulikani Rais atatoa maelekezo gani ya ziada yanayohusu kazi za Tume na namna ya kuzitekeleza. Kwa upande mwingine, mapendekezo ya Ibara ya 8 yanaweza kuleta mkanganyiko na mgogoro wa kisiasa na kisheria usiokuwa wa lazima endapo Rais atatoa hadidu za rejea zinazotofautiana na matakwa ya kisheria kama yanavyopendekezwa na Ibara 9 ya Muswada Mpya. Pendekezo letu, kwa hiyo, ni kwamba Ibara ya 8 ifutwe yote na Ibara za 9 na 16 zifafanuliwe vizuri ili kuweka wazi zaidi hadidu za rejea za Tume na namna ya kuzitekeleza.

Mheshimiwa Spika, kuna mapendekezo mengine yaliyoko kwenye Muswada yanayoonyesha hatari za Urais wa Kifalme. Kama tulivyoona, Tume inatakiwa kuwasilisha ripoti yake kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano na kwa Rais wa Zanzibar. Baada ya hapo, kwa mujibu wa Ibara ya 18(2) ya Muswada, "baada ya mashauriano na makubaliano na Rais wa Zanzibar na baada ya kumalizika kwa taratibu za ndani zinazohusu utungaji wa sera, Rais atamwelekeza Waziri kuwasilisha Muswada wa Katiba katika Bunge la Katiba kwa ajili ya kupitishwa kwa vifungu vya Katiba."

Pendekezo hili ni la hatari kubwa. Kwanza, "kumalizika kwa taratibu za ndani zinazohusu utungaji wa sera" maana yake ni baada ya kukamilika kwa utaratibu wa kawaida wa Kiserikali unaohusu utungaji sera na sheria. Chini ya utaratibu huu, rasimu ya Muswada hupelekwa kwanza kwenye Kamati ya Watalaam ya Baraza la Mawaziri *(Inter Ministerial Technical Committee of the Cabinet)* kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho na Makatibu Wakuu kabla ya kupelekwa kwenye Baraza la Mawaziri kwa maamuzi ya mwisho. Baada ya maamuzi ya mwisho ya Baraza la Mawaziri, rasimu ya Muswada hurudishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuandikwa upya ndipo upelekwe katika Bunge la Katiba.

Katika hatua zote hizi, Muswada wa Sheria huweza kufanyiwa marekebisho makubwa. Kwa maana hiyo, pendekezo la kuuwasilisha Muswada wa Katiba Mpya katika Bunge la Katiba baada ya kuupitisha kwanza kwa Makatibu Wakuu ambao wote ni wateuliwa wa Rais, na kwenye Baraza la Mawaziri ambalo Wajumbe wake wote (ukiacha Makamu wa Rais na Rais wa Zanzibar) ni wateuliwa wa Rais ni kutengeneza mazingira ya kisheria yatakayoruhusu uchakachuaji wa Muswada huo kwa lengo la kuhakikisha matokeo yake ya mwisho yaani Katiba Mpya, yanakidhi maslahi ya Rais na chama chake cha CCM. Kwa vyovyote vile, pendekezo hili halikubaliki kwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, sifa za Wajumbe; Muswada Mpya unapendekeza sifa zifuatazo wanazotakiwa kuwa nazo wajumbe wa Tume:-

(a) Uzoefu katika kufanya mapitio ya Katiba na sifa za kitaaluma za Wajumbe kwenye mambo ya Katiba, sheria, utawala, uchumi, fedha na sayansi ya jamii;

(b) Jiografia na mtawanyiko wa watu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(c) Maslahi ya umma;

(d) Umri, jinsia na uwakilishi wa makundi mbali mbali ya kijamii; na

(e) Vigezo vingine ambavyo Rais ataona vinafaa. (Ibara ya 6(3).

Mheshimiwa Spika, zaidi ya sifa zilizotajwa, Ibara ya 6(4) inakataza watu wenye sifa zifuatazo kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume:-

(a) Wabunge, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Madiwani na viongozi wa vyama vya siasa wa ngazi zote kuanzia Wilaya hadi Taifa;

(b) Watumishi wa vyombo vya usalama;

(c) Watu waliowahi kuhukumiwa kwa kutenda kosa au wanaotuhumiwa mahakamani kwa mashtaka ya kukosa uaminifu au uadilifu;

(d) Watu wasiokuwa raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yana athari kubwa kwa mchakato mzima wa upatikanaji wa Katiba Mpya. Kwanza, kwa kukataza viongozi wa ngazi za juu na za kati wa vyama vya siasa kuteuliwa wajumbe wa Tume kunaondoa kwenye mchakato wa Katiba Mpya kundi kubwa la watu wenye utaalamu na uzoefu katika masuala mbalimbali ya kisiasa, Kikatiba, kisheria, kiuchumi, kiutawala, kifedha na kisayansi jamii. Vilevile, viongozi wa vyama vya siasa wanawakilisha makundi makubwa ya kijamii yenye mtawanyiko wa watu na wa kijiografia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wanawakilisha watu wa umri na jinsia zote kama inavyopendekezwa katika Muswada Mpya. *(Makofi)*

Aidha, kwa kuwa maneno "maslahi ya umma" hayajafafanuliwa katika Muswada, hakuna anayeweza kudai kwamba viongozi wa ngazi za juu na za kati wa vyama vya siasa vilivyosajiliwa kisheria baada ya kutimiza masharti yote husika ya kisheria na ambao wanaungwa mkono na mamilioni ya wananchi wa Tanzania kwa kupewa nafasi za uwakilishi katika taasisi za uwakilishi za umma kama Bunge, Baraza la Wawakilishi na Halmashauri za Serikali za Mitaa hawajui wala hawazingatii maslahi ya umma na kwa hiyo hawafai kuwakilishwa katika Tume ya Mabadiliko ya Katiba! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ingekuwa hivyo, Rais ambaye pia ni Mwenyekiti wa CCM na kwa hiyo kiongozi wa chama cha siasa naye pia atakuwa hana sifa za kuteua Tume! Na wakati haja ya kutoshirikisha watumishi wa taasisi za ulinzi na usalama katika mchakato wenye ubishani wa kisiasa kama utungaji wa Katiba Mpya inaeleweka, ni matusi kwa watu waliochaguliwa na wananchi kuwa Wabunge, Wawakilishi au Madiwani au viongozi wa vyama vya siasa vilivyowapendekeza watu hao, kuwekwa pamoja na wahalifu na kutamkwa kuwa hawana sifa za kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba! *(Makofi)*

Inaelekea lengo kuu la pendekezo hili ni kuhakikisha kwamba Vyama vya Upinzani, hasa CHADEMA, vyenye ushawishi mkubwa ndani na nje ya Bunge havipati fursa ya kuamua muundo na maudhui ya Katiba Mpya hasa katika hatua muhimu za uundaji wake. Pili, lengo kuu vilevile ni kuhakikisha kuwa Rais, na kwa hiyo chama chake cha CCM, wanadhibiti mchakato wa Katiba Mpya katika hatua muhimu ya uundaji wake. Endapo watafanikiwa katika hili, Rais na chama chake cha CCM watakuwa na nafasi kubwa ya kuamua aina ya Katiba Mpya itakayotokana na mchakato walioudhibiti kama inavyopendekezwa na Muswada Mpya. Hii ni kwa sababu, kwa kutumia uzoefu wa Tume nyingine zilizopata kuteuliwa miaka ya nyuma, wajumbe wengi huwa ni watumishi au waliopata kuwa watumishi wa Serikali na/au taasisi zake. Wajumbe wa aina hii wamekuwa hawana uthubutu wa kupendekeza mabadiliko makubwa yanayohitajika katika mfumo wa utawala wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, badala ya kukataza viongozi wa vyama vya siasa kama inavyopendekezwa na Muswada Mpya na kwa kuzingatia nafasi ya vyama vya siasa katika historia yetu na mfumo wetu wa utawala na kwa lengo la kuhakikisha Tume inakuwa na utaalamu, uzoefu na uhalali wa kisiasa unaohitajika, watu wanaostahili kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume wawe ni wale wenye sifa zinazopendekezwa na Ibara ya 6(3)(a), (b), (c) na (d) ya Muswada. Kwa sababu hiyo, hakutakiwi kuwa na vigezo vingine visivyojulikana wazi kwa wananchi. Kwa maneno mengine, pendekezo la kuwa na "vigezo vingine ambavyo Rais ataona inafaa" halikubaliki kwani linampa Rais mwanya wa kuteua marafiki zake au watu ambao hawana sifa zinazojulikana. Kwa maoni yetu vilevile, badala ya kuwa sababu ya *disqualification,* uongozi wa kuchaguliwa na wananchi katika taasisi za uwakilishi au katika vyama vya siasa unatakiwa kuwa *an added advantage* pale ambapo kiongozi husika ana sifa za kitaaluma zinazotakiwa!

Mheshimiwa Spika, misingi mikuu ya Kitaifa; Muswada unapendekeza kuwepo kwa "misingi mikuu ya Kitaifa" ambayo Tume inatakiwa kuizingatia kwa lengo la kuihifadhi na kuidumisha. Misingi mikuu inayopendekezwa ni:-

(a) Kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano;

(b) Uwepo wa Serikali, Bunge na Mahakama;

(c ) Mfumo wa kiutawala wa kijamhuri;

(d) Umoja wa Kitaifa, amani na utulivu;

(e) Uchaguzi wa kidemokrasia wa mara kwa mara katika vipindi maalum kwa kuzingatia haki ya watu wote kupiga kura;

(f) Ukuzaji na na uhifadhi wa haki za binadamu;

(g) Utu, usawa mbele ya Sheria na mwenendo wa sheria; na

(h) Uhuru wa kuabudu na uvumilivu wa dini nyingine. (Ibara ya 9(2).

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki kimefanyiwa mabadiliko kwa kufuta maneno "Tume itahakikisha... kutokugusika na utakatifu *(inviolability and sanctity)* wa mambo yafuatayo" yaliyokuwa katika Muswada wa zamani, na badala yake yamewekwa maneno mapya "... kuhifadhi na kudumisha mambo yafuatayo..." Mabadiliko haya yamefanywa ili kujaribu kuondoa hofu iliyojitokeza wakati wa mikutano ya kukusanya maoni ya wadau kwamba lengo la pendekezo hilo lilikuwa kuzuia mjadala juu ya masuala ya Kikatiba yenye utata mkubwa kama vile suala la Muungano. Hata hivyo, hatari ya kuzuiliwa kwa mjadala juu ya misingi mikuu ya Kitaifa bado haijaondolewa kwani, kwa mujibu wa Ibara mpya ya 9(3), "... Tume itatoa fursa kwa watu kutoa maoni yao kwa uhuru kwa lengo la kuendeleza na kuboresha masuala hayo." Tafsiri halisi ya maneno haya ni kwamba mjadala pekee utakaoruhusiwa juu ya "misingi mikuu ya Kitaifa" ni ule ambao lengo lake ni "kuendeleza na kuboresha masuala hayo."

Kwa maoni yetu, lengo kuu la pendekezo linalohusu kuendeleza na kuboresha "misingi mikuu ya Kitaifa" ni kuzuia mjadala wenye kuhoji "kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano" ili kuendeleza mfumo wa sasa wa Muungano wenye Serikali mbili. Hii ni kwa sababu katika mambo yote yanayopendekezwa kuwa misingi mikuu ya Kitaifa, ni "kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano" yenye Serikali mbili ndio ambayo imekuwa na mgogoro mkubwa kwa muda wote wa maisha ya Jamhuri ya Muungano. Ukiacha "ukuzaji na uhifadhi wa haki za binadamu" ambalo lilikataliwa na Serikali ya Mwalimu Nyerere kwa miaka yote ya utawala wake, mambo mengine yote yanayotajwa kuwa "misingi mikuu ya Kitaifa" hayajawahi kubishaniwa kwa miaka yote ya uhai wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la "misingi mikuu ya Kitaifa" linastaajabisha sana kwani kwa mujibu wa Ibara ya 98(1)(b) ya Katiba ya sasa, "kuwapo kwa Jamhuri ya Muungano, Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, madaraka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kuwapo kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano, madaraka ya Serikali ya Zanzibar, Orodha ya Mambo ya Muungano na idadi ya Wabunge kutoka Zanzibar" ni mambo yanayoweza kubadilishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ili mradi tu mabadiliko hayo yaungwe mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote wa kutoka Tanzania Bara na wa Tanzania Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, pendekezo la Ibara ya 9(3) ya Muswada kwamba "misingi mikuu ya Kitaifa" izungumzwe kwa lengo la kuiendeleza na kuidumisha tu, halikubaliki kwa sababu linazuia uhuru wa kuhoji na/au kupinga mambo ambayo kwa Katiba ya sasa ni ruhusa kuyahoji, kuyapinga na/au hata kuyabadilisha! Tunapendekeza Ibara ya 9(2) na (3) za Muswada zifutwe kabisa ili kuwepo na uhuru kamili wa kujadili, kwa kupinga au kuunga mkono, kila jambo linalohusika na Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, nafasi ya Zanzibar; pengine mabadiliko makubwa yaliyofanywa katika Muswada ni mapendekezo yanayohusu nafasi ya Zanzibar katika mchakato wa Katiba Mpya. Itakumbukwa kwamba moja ya masuala yaliyozua tafrani kubwa katika mchakato wa kukusanya maoni juu ya Muswada wa zamani hasa katika kituo cha Zanzibar ni kuwepo hisia kwamba nafasi ya Zanzibar ilikuwa imepuuzwa katika Muswada huo. Muswada sio tu kwamba umetekeleza matakwa yote ya ushirikishwaji wa Zanzibar, bali umekwenda mbali zaidi kwa kuifanya Zanzibar mwamuzi wa mustakbala wote wa Kikatiba wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii imefanyika kwa njia mbili, kwanza, kwa kumfanya Rais wa Zanzibar kuwa mshirika sawa wa Kikatiba wa Rais wa Jamhuri ya Muungano; na pili, kwa kuipa Zanzibar nafasi kubwa ya uwakilishi katika mchakato mzima wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, nafasi ya Rais wa Zanzibar; Muswada unapendekeza kwamba utekelezaji wa mamlaka yote ya Rais, Waziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano lazima ufanyike kwa "mashauriano na makubaliano" na Rais, Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar. Kwa mfano, Ibara ya 5 inayohusu kuundwa kwa Tume inamtaka Rais "kushauriana na kukubaliana" na Rais wa Zanzibar na kupata ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar. Vilevile, Ibara ya 6(1) inayohusu uteuzi wa Wajumbe wa Tume; Ibara ya 8(1) na (2) inayohusu hadidu za rejea na kuongeza muda wa Tume; na Ibara ya 13(2) inayohusu uteuzi wa Katibu wa Tume, zote zinataka kuwepo na makubaliano na Rais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Aidha, Ibara ya 13(5) inayohusu uteuzi wa watendaji wengine wa Tume inalazimu makubaliano kati ya Waziri na Waziri mwenzake wa Zanzibar ambao nao ni wateuliwa wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Rais wa Zanzibar.

Mamlaka ya Rais wa Zanzibar hayaishii tu kwenye uteuzi wa wajumbe na watendaji wa Tume, bali pia yanaingia hata katika uwasilishaji wa ripoti ya Tume. Kwa mujibu wa Ibara 18(1) ya Muswada, mara baada ya kumaliza kazi yake, Tume itawasilisha ripoti yake kwa Rais na kwa Rais wa Zanzibar. Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 18(2), mara baada ya kupokea ripoti hiyo, Rais, "baada ya kushauriana na kukubaliana" na Rais wa Zanzibar, "... atamuagiza Waziri kuwasilisha Muswada wa Katiba katika Bunge la Katiba." *(Makofi)*

Kwa mapendekezo haya pia, Rais wa Zanzibar sio tu kwamba ana mamlaka karibu sawa na Rais wa Jamhuri ya Muungano bali pia ana kura ya turufu katika mchakato wa Katiba Mpya. Maana yake ni kwamba Rais wa Zanzibar asipopatiwa nakala ya ripoti ya Tume au asipokubaliana na Rais wa Muungano, basi Muswada wa Katiba hautawasilishwa kwenye Bunge la Katiba! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yanaashiria kuwepo kwa mtazamo ambao chanzo chake ni makubaliano ya Muungano kati ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika ya tarehe 25 Aprili, 1964. Kwa mtazamo huo, Zanzibar ni nchi huru kama ilivyokuwa mwaka 1964 na kwa hiyo, ni lazima sio tu ishirikishwe kwa usawa, bali pia lazima ikubaliane na mabadiliko yoyote ya Kikatiba yanayopendekezwa na Muswada. Kama Profesa Palamagamba Kabudi wa Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alivyosema kwenye semina ya Wabunge juu ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Katiba iliyofanyika tarehe 12 Novemba 2011; "katika kuandika Katiba mpya, wabia wa Muungano wanarudi kwa usawa."

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mtazamo huu sio sahihi. Kwanza kabisa, Zanzibar sio nchi huru tena kama ilivyokuwa mwaka 1964, kama ambavyo hakuna tena nchi inayoitwa Tanganyika wala Serikali yake. Hii ni kwa sababu tangu kusainiwa kwa Hati za Muungano mwaka 1964, na kwa mujibu wa Ibara ya 4(3) ya Katiba ya sasa, masuala yote yanayohusu Muungano kama vile Katiba ya Tanzania yamekasimiwa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ambayo pia imekasimiwa mamlaka juu ya masuala ya iliyokuwa Tanganyika. Masuala haya ya Muungano hayawezi kujadiliwa upya na kwa usawa kati ya nchi hizi mbili kwa vile moja kati ya nchi hizo haipo tena na iliyobaki imepoteza sehemu ya uhuru wake kutokana na Muungano huo! Hii ndio kusema hakuwezi tena kuwa na wabia wa Muungano bila kwanza kuirudisha Tanganyika kama nchi na

bila kuirudisha Jamhuri ya Watu wa Zanzibar yenye uhuru na mamlaka kama iliyokuwa nayo kabla ya Muungano!

Pili, kuna dhana kwamba Rais wa Zanzibar hakushirikishwa katika mchakato wa maandalizi ya Muswada wa zamani. Dhana hii vilevile ni potofu. Kwanza, Rais Dokta Ali Mohamed Shein mwenyewe ametamka wazi kwa waandishi wa habari kwamba alishiriki katika hatua zote za maamuzi kwenye Baraza la Mapinduzi.

Kwa mujibu wa Ibara ya 54(1) ya Katiba ya sasa, Rais wa Zanzibar ni mmoja wa Wajumbe wa Baraza la Mawaziri la Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kwa hiyo ni mshiriki wa maamuzi yote ya Serikali hiyo. Kwa maana hiyo, maslahi ya Zanzibar yanawakilishwa ndani ya “chombo kikuu cha kumshauri Rais” katika Jamhuri ya Muungano. (Ibara ya 54(3) hii ni licha ya ukweli kwamba kwa mlolongo wa madaraka uliopo katika Ibara ya 54(2), Rais wa Zanzibar sio mmoja wa Wajumbe wanaoweza kuongoza mikutano ya Baraza hilo.

Aidha, ndani ya Baraza la Mawaziri, Zanzibar inawakilishwa pia na Makamu wa Rais ambaye kwa mujibu wa Ibara ya 47(1) ya Katiba ya sasa “... ndiye Msaidizi Mkuu wa Rais kuhusu mambo yote ya Jamhuri ya Muungano....” Kwa maana hiyo, mapendekezo ya Muswada yanayomfanya Rais wa Zanzibar kuwa sio tu mshiriki sawa lakini pia mwamuzi wa mustakbala wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano yanaenda kinyume sio tu na Katiba ya sasa bali pia na Hati za Muungano wenyewe. Kwa mapendekezo haya, endapo Rais wa Zanzibar hatakubaliana na uteuzi wowote wa Wajumbe wa Tume au Katibu wake au watendaji wake wengine, anaweza kusimamisha mchakato mzima wa Kikatiba hata kama unahusu masuala ya Tanzania Bara yasiyo ya Muungano! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwakilishi wa Zanzibar; ushawishi mkubwa wa Zanzibar hauishii katika kura ya turufu aliyo nayo Rais wa Zanzibar pekee yake. Zanzibar ina ushawishi mkubwa vilevile kutokana na nafasi kubwa iliyonayo katika vyombo vya maamuzi vinavyopendekezwa na Muswada. Kwa mfano, kwa mujibu wa Ibara ya 6(2), “... muundo wa Tume utazingatia msingi wa kuwepo kwa uwakilishi ulio sawa kwa kila upande wa Jamhuri ya Muungano.” Hii ina maana kwamba Wajumbe wa Tume na Sekretarieti yake wanatakiwa wawe sawa kwa sawa kati ya Tanzania Bara na Zanzibar. Ikumbukwe kwamba Tume hii inatengeneza Katiba inayohusu masuala ya Muungano, ambayo ni haki kwa Zanzibar kushirikishwa kwa usawa kabisa na vilevile masuala yasiyokuwa ya Muungano ya Tanzania Bara ambayo Zanzibar haina haki ya kushiriki.

Mheshimiwa Spika, Bunge la Katiba; eneo la pili ambalo Zanzibar ina ushawishi mkubwa kutokana na uwakilishi wake ni katika Bunge la Katiba linalopendekezwa katika Sehemu ya Tano ya Muswada. Kwa mujibu wa Ibara ya 20(2), Wajumbe wa Bunge la Katiba watakuwa ni Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano; Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar; Mawaziri wa Katiba na Sheria wa Jamhuri ya Muungano na wa Zanzibar; Wanasheria Wakuu wa Jamhuri ya Muungano na wa Zanzibar; na Wajumbe 116 watakaoteuliwa kutoka asasi zisizokuwa za Kiserikali, asasi za kidini, vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu, taasisi za elimu ya juu na makundi yenye mahitaji maalum katika jamii. Inaelekea kwamba, kwa mujibu wa Ibara ya 20(4), Wajumbe wasiokuwa Wabunge ama wawakilishi nao pia watateuliwa na Rais licha ya kutoka nje ya mfumo wa Kiserikali!

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 66(1)(a) ya Katiba ya sasa ya Muungano, Wajumbe wa Bunge la Jamhuri ya Muungano ni pamoja na Wabunge wa Majimbo ya Uchaguzi. Kwa *composition* ya sasa ya Bunge, kuna jumla ya Majimbo ya Uchaguzi 239 ambayo kati yao majimbo ya Zanzibar ni 50. Vilevile, kwa mujibu wa Ibara ya 66(1)(c) ya Katiba, Baraza la Wawakilishi Zanzibar linawakilishwa na Wabunge watano katika Bunge la Jamhuri ya Muungano. Aidha, kama inavyotakiwa na Ibara ya 66(1)(b), kuna Wabunge wanawake 102 wanaojulikana kama “Wabunge wa Viti Maalum.” Kwa mgawanyo wa sasa wa Wabunge hawa, idadi ya wanaotoka Zanzibar ni 25 kwa vyama vyote vyenye uwakilishi Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mwisho, kuna Wabunge wasiozidi 10 wanaoteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa Ibara ya 66(1)(e). Hadi sasa, Rais ameshateua Wabunge watatu ambao wote ni wa kutoka Zanzibar. Kwa hiyo, katika Bunge la sasa lenye Wabunge 353,

Wabunge wanaowakilisha Zanzibar ni 83 au karibu 23.5% ya Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sehemu ya Kwanza ya Sura ya Tano ya Katiba ya Zanzibar, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ni pamoja na Wawakilishi wa Majimbo 50 ya Uchaguzi, wawakilishi 10 wa kuteuliwa na Rais wa Zanzibar na Wawakilishi 20 wa Viti Maalum na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hiyo, jumla ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa sasa ni 81. Kwa maana nyingine ni kwamba endapo mapendekezo ya Ibara ya 20(1)(b), (c) na (d) ya Muswada yatakubaliwa, idadi ya wajumbe wa Bunge la Katiba wanaotoka Zanzibar itaongezeka hadi kufikia 164 kati ya Wajumbe 545 wa Baraza hilo kwa mujibu wa Ibara ya 20(2). Idadi hii ni sawa na 30% ya Wajumbe wote wa Bunge la Katiba.

Idadi hiyo ya uwakilishi wa Zanzibar bado haitakidhi matakwa ya Muswada kwani Ibara ya 20(3) inapendekeza kwamba "...idadi ya Wajumbe wa Baraza la Katiba kutoka Tanzania Zanzibar ... haitapungua theluthi moja ya wajumbe wote wa Bunge la Katiba!" Theluthi moja ya Wajumbe wa Bunge la Katiba ni Wajumbe 182. Kwa hiyo, ili kukidhi matakwa ya Muswada kuhusu uwakilishi wa Zanzibar, itabidi Wajumbe 18 kati ya 116 waliotajwa na Ibara ya 20(2)(e) watoke Zanzibar ili kufikisha idadi ya Wajumbe 182 ambayo ndio theluthi moja ya Wajumbe wote wa Bunge la Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengine ya Muswada ambayo pia yanazua maswali mengi juu ya nafasi ya Zanzibar katika mchakato wa Katiba Mpya. Kwa mfano, wakati Ibara ya 21(1) inapendekeza kwamba Spika na Naibu Spika wa Bunge la Katiba wachaguliwe kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Bunge hilo, Ibara ya 21(2) inapendekeza kwamba endapo Spika atatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano basi Naibu wake lazima atoke upande mwingine. Sambamba na pendekezo hili, Ibara ya 22(1) inapendekeza Makatibu wa sasa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar watakuwa ndio Katibu na Naibu Katibu wa Bunge la Katiba. Aidha, sawa na Ibara ya 21(2), Ibara ya 22(2) inapendekeza kwamba endapo Spika atatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, basi Katibu wa Bunge la Katiba lazima atoke upande mwingine.

Mapendekezo haya yanaonyesha sio tu nafasi na ushawishi mkubwa wa Zanzibar katika mchakato wa Katiba Mpya, bali pia ni mwendelezo wa dhana potofu kwamba Zanzibar ni mshirika sawa wa Jamhuri ya Muungano. Hii inathibitishwa pia na pendekezo la Ibara ya 24(3) ya Muswada inayotaka Katiba Mpya ikubaliwe na theluthi mbili ya Wajumbe wa Bunge la Katiba wanaotoka Tanzania Bara na vilevile theluthi mbili ya Wajumbe wanaotoka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba iwe ni kwa masuala ya Muungano yanayoihusu Zanzibar pia au kwa masuala yasiyokuwa ya Muungano ya Tanzania Bara ambayo hayaihusu, Zanzibar itakuwa na kura ya turufu kwa mujibu wa mapendekezo ya Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwakilishi mkubwa wa Zanzibar katika Bunge la Jamhuri ya Muungano umetumika kihistoria kwa lengo la kuwatuliza Wazanzibari wakati Serikali ya Mwalimu Nyerere ilipokuwa inamomonyoa uhuru wa Zanzibar kwa kuongeza orodha ya Mambo ya Muungano kwenye Katiba ya Muungano. Katika kitabu chake *Pan Africanism or Pragmatism? Lessons of Tanganyika – Zanzibar Union,* Profesa Issa Shivji, mwanazuoni mashuhuri wa Kikatiba na mwanafunzi wa historia ya Muungano huu amemnukuu aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar wakati wa utawala wa Hayati Sheikh Abedi Amani Karume, Bwana Wolfgang Dourado akimnukuu Sheikh Karume juu ya nafasi ya Zanzibar katika Bunge la Jamhuri ya Muungano; "Msiwe na wasi wasi, sisi tuna haki ya kuwakilishwa katika Bunge lao lakini wao hawana haki ya kuwakilishwa katika Baraza letu la Mapinduzi!"

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine inatokana na kuongezeka kwa ushawishi na nafasi ya Zanzibar katika siasa za ndani ya CCM, hasa hasa katika zama hizi za vyama vingi na vita za makundi mbalimbali ndani ya chama hicho. Katika mazingira haya, mtu yeyote anayetaka kupitishwa kuwa Mgombea Urais kwa kupitia CCM anakuwa anahitaji kura za CCM Zanzibar ili kushinda katika kinyang'anyiro hicho. Kwa kauli ya Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere mwenyewe katika kitabu chake Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania; "sababu moja kubwa iliyofanya

viongozi wetu wasitake kuwaudhi "Wazanzibari"... ni umuhimu wa kura za Zanzibar katika kumteua mwanachama wa CCM kuwa Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano. Kwa kiongozi yeyote anayeliona jambo hilo kuwa ni muhimu kupita mengine yote, kuwaudhi "Wazanzibari" ni dhambi ambayo haina budi iepukwe kwa kila njia."

Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, hofu hii ya kuwaudhi "Wazanzibari" ndio imepelekea kimya kikuu ndani ya CCM na ndani ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya ukiukwaji mkubwa wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano uliofanywa na Sheria ya Mabadiliko ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar, 2010.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba upendeleo wa Zanzibar unaopendekezwa katika Muswada huu kuhusiana na uwakilishi katika Bunge la Katiba na katika vyombo vingine vya maamuzi juu ya mchakato wa Katiba Mpya sio wa haki na haukubaliki tena. Kwanza, Ibara ya 64(2) ya Katiba ya sasa inaweka wazi kwamba Baraza la Wawakilishi Zanzibar lina mamlaka ya kutunga sheria katika Zanzibar "... juu ya mambo yote yasiyo mambo ya Muungano...." Hii pia ndio lugha ya Ibara ya 78(1) ya Katiba ya Zanzibar kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka jana. "Katiba ya Tanzania" ni jambo la kwanza katika orodha ya mambo ya Muungano iliyopo kwenye Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Muswada Mpya kupendekeza kwamba Baraza la Wawakilishi Zanzibar liwe sehemu ya Bunge la Katiba ni kukiuka wazi wazi matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na ya Katiba ya Zanzibar. Ni ajabu iliyoje kwamba wale wanaojifanya ni machampioni wa Muungano wanaweza kunyamazia ukiukaji huu wa Katiba!

Mheshimiwa Spika, Thomas Paine, mwandishi maarufu wa Marekani ya wakati wa Mapinduzi ya mwaka 1776, aliwahi kuandika kijitabu alichokiita *Common Sense* juu ya uhalali wa Uingereza kutawala Bara la Amerika ya Kaskazini ambako alisema: *"... [T]here is something very absurd in supposing a continent to be perpetually governed by an island [for] in no instance hath nature made the satellite larger than its primary planet...!"* Yaani ni ujinga kudhani kwamba Bara linaweza kutawaliwa milele na kisiwa kwa sababu utaratibu wa asili haujawahi kufanya kitegemezi kuwa kikubwa kuliko sayari yake ya msingi. Hata kama ni kweli kwamba Tanganyika sio Bara kama ilivyokuwa Marekani ya Kaskazini, bado tunakubaliana na Tom Paine kwamba "ni ujinga kudhani kwamba Visiwa vya Zanzibar vitaendelea kuwa na maamuzi na ushawishi mkubwa katika masuala yasiyokuwa ya Muungano, ya Tanganyika kwa sababu utaratibu wa asili haujawahi kufanya maslahi ya Visiwa hivyo kuwa bora zaidi ya maslahi ya Tanganyika!"

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yetu, wakati umefika kwa Muungano kuwekwa kwenye msingi wa usawa na imara zaidi. Msingi huo unahitaji kurudishwa tena kwa Serikali ya Tanganyika ambayo ndio ilikuwa pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mbia mkuu wa Muungano wa mwaka 1964. Kurudishwa huko kwa Tanganyika kutaiwezesha Zanzibar kujadiliana nayo kwa usawa juu ya masuala yote yanayohusu Muungano. Haya yote yanawezekana tu endapo Muungano huu utawekwa mbele ya wananchi ili waamue kwa kura ya maoni kama wanataka kuendelea nao au la; na kama wanataka kuendelea nao ni muundo gani wa Muungano wanaoutaka.

Mapendekezo ya kurudishwa kwa Tanganyika na Serikali yake sio mapya. Miaka ishirini iliyopita, Tume ya Rais ya Mfumo wa Chama Kimoja au Vyama Vingi vya Siasa (Tume ya Nyalali) ilipendekeza hivyo hivyo. Miaka saba baadae, Tume ya kukusanya maoni juu ya Katiba, *White Paper* Na. 1 ya 1998 (Tume ya Kisanga) nayo ilipendekeza hivyo hivyo. Kuendelea kupuuza mapendekezo haya wakati Zanzibar inavunja Katiba ya sasa ya Muungano; kuendelea kukaa kimya kwa hofu ya kuwaudhi Wazanzibari wakati wao wanajitwalia uhuru wa kujiamulia mambo yao wenyewe huku wakiendelea kushiriki katika maamuzi ya mambo ya Tanganyika yasiyokuwa ya Muungano; kuendeleza kile alichokiita Mwalimu Nyerere falsafa ya "changu ni changu, chako ni chetu" katika mahusiano ya Zanzibar na Tanzania Bara, ni kutulazimisha tuipinge dhana nzima ya Muungano kati ya nchi zetu mbili kitu kinachoweza kupelekea kuvunjika kwa Muungano wenyewe. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni isingependa tufike huko lakini ndoa hii ya kulazimishana haiwezi ikadumu muda mrefu kwa taratibu za aina hii.

Mheshimiwa Spika, udhoofishaji wa upinzani, mapendekezo ya Muswada juu ya uwakilishi katika Bunge la Katiba yana athari nyingine kubwa katika majadiliano na maamuzi ndani ya Bunge la Katiba. Kwa mujibu wa uchambuzi uliofanywa na Profesa Issa G. Shivji kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, endapo mapendekezo ya Ibara ya 20(2) ya Muswada yatapitishwa, CCM itakuwa na kati ya Wajumbe 350 hadi 400 katika Bunge la Katiba ambalo lina Wajumbe 545. Kwa upande mwingine Chama cha Wananchi *(CUF)* ambacho kina Wawakilishi 29 katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar kitakuwa na Wajumbe 65 katika Bunge la Katiba. Kwa maana ya uwakilishi katika Bunge la Katiba, *CUF* itakuwa ndio chama cha pili kwa nguvu za kisiasa ndani ya Bunge hilo, licha ya kuwa na Wabunge wawili tu wa kuchaguliwa kwa upande wa Tanzania Bara na licha ya kupata kura chache sana katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana.

Na kama inavyojulikana, tangu muafaka wa kisiasa Zanzibar kati ya CCM na *CUF* wa mwaka 2010 na kuzaliwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, upinzani wa kisiasa Zanzibar umekufa na kwa upande wa Tanzania Bara na hasa Bungeni na kwenye chaguzi ndogo kama ule wa Igunga, *CUF* imekuwa ikishirikiana na CCM kuipinga CHADEMA. *(Makofi)*

Kwa mapendekezo haya, Kambi ya CCM na *CUF* katika Bunge la Katiba inaweza kufika hata zaidi ya Wajumbe 465 katika ya Wajumbe 545 wa Bunge hilo! CHADEMA ambayo kwa sasa ndio chama kinachoongoza Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kutokana na matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, itabakia na Wabunge wake 48 na vyama vya Kibunge vilivyobaki yaani *NCCR-Mageuzi, TLP* na *UDP* vitabaki na jumla ya Wabunge sita. Kwa hiyo, CHADEMA itakuwa chama cha tatu kwa nguvu za kisiasa ndani ya Bunge la Katiba licha ya kuwa ni chama kikuu cha upinzani chenye nguvu na ushawishi mkubwa wa kisiasa nchini! *(Makofi)*

Kwa maana nyingine, iwe ni kwa makusudi au bila ya kujua au kwa kunuia, athari mojawapo kubwa ya mapendekezo ya Muswada kuhusu uwakilishi katika Bunge la Katiba itakuwa ni kuiongezea nguvu zaidi kambi ya CCM/*CUF* na kupunguza nguvu na ushawishi wa CHADEMA ambayo ndio chama pekee kinachobeba matarajio na matamanio ya Watanzania wengi wanaotaka mabadiliko ya kimsingi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haihitaji kuwa na Shahada ya Uzamivu kujua kwamba Bunge la Katiba lenye uwakilishi wa aina hii litapitisha Katiba Mpya ambayo pengine itatofautiana na Katiba ya sasa kwa jina tu! Na wala haihitaji kisomo kikubwa kujua kwamba Bunge la Katiba la aina hii halitagusa “msingi mkuu” uliobaki wa Jamhuri ya Muungano yaani Serikali mbili. Hapa pia ni wazi kuwa lengo halisi la mapendekezo haya ni kuhakikisha kwamba mchakato wa Katiba Mpya utazaa matunda yasiyokuwa tofauti sana na ya Katiba ya sasa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwakilishi wa Bunge la Katiba, sio Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wala Baraza la Wawakilishi Zanzibar lenye mamlaka Kikatiba na kisiasa ya kutunga Katiba Mpya ya Tanzania. Hii ni kwa sababu sisi wote tuliopo humu ndani tulichaguliwa kwa mujibu wa Katiba ya sasa na mamlaka yetu yote yapo ndani ya kona nne za Katiba hiyo. Kama ni kweli, kama anavyodai Profesa Kabudi kwamba kitendo cha kutunga Katiba Mpya vilevile ni kitendo cha kuua Katiba ya zamani, basi sisi Wabunge na Wawakilishi wa Zanzibar hatuna mamlaka ya kuiua Katiba ya sasa kwa sababu sisi wote tulikula kiapo cha kuilinda, kuihifadhi na kuitetea. *(Makofi)*

Pili, sisi sote ni Wabunge na Wawakilishi wa vyama vya siasa kwa sababu kwa mujibu wa Katiba ya sasa sheria zote husika, tumechaguliwa kwa sifa kuu ya kuwa wanachama wa, na tuliopendekezwa na, vyama vya siasa. Kuligeuza Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuwa Bunge la Katiba ni sawa na kusema kwamba wasiokuwa wanachama wa vyama vya siasa hawana haki ya kushiriki katika kutunga Katiba Mpya kwa sababu ya kuwa na kilema cha kisheria kinachowakataza kuchaguliwa kuwa Wabunge na Wawakilishi! *(Makofi)*

Ibara ya 20(4) ya Katiba ya sasa inatamka wazi kwamba “... ni marufuku kwa mtu yeyote kulazimishwa kujiunga na chama chochote....” Sio kosa, kwa hiyo, kwa mamilioni ya Watanzania ambao wameamua kwa hiari zao kutokuwa wanachama wa vyama vya siasa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haikubaliani, na haiwezi kukubali ubaguzi wa aina hii dhidi ya Watanzania walioamua kutumia haki zao za Kikatiba ya kutokujiunga na chama chochote cha siasa. Aidha,

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haitakubali Watanzania hao waadhibiwe kwa kunyimwa kushiriki katika Bunge la Katiba kwa sababu tu ya kutokuwa wanachama wa vyama vya siasa. *(Makofi)*

Tatu, Wajumbe 116 wanaopendekezwa kuteuliwa kwenye Bunge la Katiba kwa mujibu wa Ibara ya 20(2)(e) na (4) ya Muswada Mpya sio, na hawawezi kuwa wawakilishi wa wananchi. Kwanza, hawajachaguliwa na mtu yeyote na wala taasisi zao kuwawakilisha katika Bunge la Katiba kwa sababu Muswada Mpya unapendekeza wateuliwe na Rais. Pili, Bunge la Katiba ni chombo cha uwakilishi wa moja kwa moja wa wananchi na kwa mila na desturi zinazokubalika na kutumika Kimataifa, Wajumbe wa Bunge la Katiba huchaguliwa moja kwa moja na wananchi bila ya kujali vyama vya siasa na huwa na kazi moja tu; kutunga Katiba Mpya. Kwa sababu zote hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza Wajumbe wa Bunge la Katiba wachaguliwe moja kwa moja na wananchi na kusiwe na masharti yoyote kuhusu uanachama wa vyama vya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhalalishaji wa Katiba mpya, Muswada una mapendekezo ambayo yanaashiria kuachana na utaratibu wa kihistoria wa utungaji wa Katiba ambao umewaweka wananchi kando katika michakato wa Kikatiba tangu miaka ya mwanzo ya Uhuru. Kwa mujibu wa Ibara ya 27(1), kutakuwa na kura ya maoni kwa lengo la kuihalalisha Katiba Mpya. Kwa mujibu wa Ibara ya 30, watu wote walioandikishwa kuwa wapiga kura kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya Taifa na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar, watakuwa na haki ya kupiga kura katika kura hiyo ya maoni. Aidha, kufuatana na Ibara ya 32(2), matokeo ya kura ya maoni yataamuliwa kwa msingi wa kuungwa mkono kwa zaidi ya 50% ya kura zote zilizopigwa Tanzania Bara na kiasi hicho hicho kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya ushirikishwaji wa wananchi katika kuipa Katiba uhai wa kisheria ni jambo la maana sana na linaonyesha kuwa tumeanza kuachana na urithi wa Kikatiba wa kikoloni ulioanza na Katiba ya Uhuru ya mwaka 1961. Hata hivyo, mapendekezo haya yamejaa mitego na vichaka vingi vya hatari. *(Makofi)*

Kwanza, Ibara ya 27 inapendekeza kwamba kura ya maoni itaratibiwa na kusimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushirikiana na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Tume hizi mbili kwa mashauriano na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar ndizo zitakazotengeneza swali litakaloulizwa kwenye kura ya maoni. (Ibara ya 28(1) na (2) Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 31, utaratibu utakaotumika katika kura ya maoni ni ule unaotumika katika chaguzi za kawaida katika nchi yetu yaani Sheria ya Uchaguzi wa Taifa, Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292 na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarudia kauli yake ndani ya Bunge hili wakati wa kujadili Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria tarehe 24 Agosti, 2011; "Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina imani, sio tu na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, bali pia na mfumo mzima wa kisheria na kitaasisi unaoendesha chaguzi za nchi yetu. Mfumo huu na watendaji wake wameonyesha wazi kutokuwa huru na kutumiwa na Chama cha Mapinduzi kuchakachua matokeo ya chaguzi mbalimbali hapa nchini. Kwa maana hiyo, Tume ya Uchaguzi ya Taifa na ile ya Zanzibar, haiwezi kuachiwa jukumu kubwa la kuendesha kura ya maoni kwa ajili ya kupata Katiba Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba Serikali ilete Bungeni Muswada wa mapendekezo ya mabadiliko ya Katiba na ya Sheria husika za uchaguzi kwa lengo la kuiunda upya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa lengo la kuhakikisha inasimamia zoezi la kura ya maoni kwa uhuru na bila upendeleo kwa Chama Tawala."

Kuna maeneo mengine ambayo nayo yanaonyesha kwamba lengo halisi la Muswada huu ni kupata Katiba ambayo haitabadilisha mambo ya msingi ila itakuwa mpya kwa jina tu. Kwanza, Ibara ya 26(2) inapendekeza kumpa Rais mamlaka ya "kuliitisha tena Bunge la Katiba lenye Wajumbe wale wale siku zijazo kwa ajili ya kutunga masharti ya Katiba kabla ya kuizindua Katiba inayopendekezwa kwa lengo la kurekebisha masharti yaliyomo kwenye Katiba iliyopendekezwa." Maana halisi ya maneno haya ni kwamba Rais atakuwa na mamlaka ya kuita tena Bunge la Katiba ili lifanye marekebisho ya mambo ambayo yeye au Serikali yake au chama

chake hawayapendi katika Katiba Mpya kabla haijapigiwa kura ya maoni na wananchi! Kama chombo huru cha wananchi, Rais hawezi kujipa madaraka ya kupingana na kauli ya wananchi kupitia Bunge la Katiba.

Pili, wakati Ibara ya 32(3) inapendekeza kurudiwa kwa kura ya maoni endapo kura za "NDIYO" na "HAPANA" zitalingana, Ibara ya 32(4) inaelekeza kwamba "endapo wingi wa kura ya maoni utakuwa ni "HAPANA," Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977, itaendelea kutumika." Endapo pendekezo hili litapitishwa na kuwa Sheria, hii itakuwa ni kualika maasi kwa vile, kwa vyovyote vile, wananchi wa Tanzania baada ya kupitia mchakato mrefu wa kutengeneza Katiba Mpya hawatakubali tena kuvishwa minyororo ya Katiba ya sasa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba badala ya kurudi kwenye *status quo ante* kama inavyopendekezwa, mchakato wa Katiba Mpya uanze tena hadi hapo utakapopatikana muafaka wa Kitaifa wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, 2011 ni Muswada muhimu kuliko pengine Miswada yote ambayo Bunge la Kumi litapata fursa ya kuijadili na kuipitisha. Ni Muswada wa kihistoria kwa vile tangu Uhuru wa Tanganyika miaka hamsini iliyopita na tangu Muungano miaka karibu 48 iliyopita, Watanzania hatujawahi kupata fursa ya kujadili na kuamua mustakbala wa Taifa letu Kikatiba kwa utaratibu kama unaopendekezwa katika Muswada huu. Hata hivyo, kwa jinsi ambavyo Muswada huu ulivyoandaliwa na kwa maudhui yake na kwa jinsi ulivyoletwa Bungeni kwa kukiuka makusudi Kanuni za Bunge, ni wazi kama utapitishwa jinsi ulivyo Watanzania tutakuwa tumekosa fursa ya kuamua mustakbala wa Taifa letu kwa njia ya amani na maridhiano. Bunge hili Tukufu lina wajibu mbele ya historia na kwa vizazi vya sasa na vijavyo, kuhakikisha kwamba tunapata muafaka wa Kitaifa juu ya Tanzania tunayoitaka. *(Makofi)*

Hukumu ya historia, endapo Bunge hili Tukufu litaendekeza ushabiki wa kisiasa na kufanya maamuzi ya mambo makubwa kama haya kwa kupiga kelele au kwa kuzomea au kwa kugonga meza kwa nguvu, itakuwa ni kali sana. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiwezi kuwa sehemu ya maamuzi makubwa kama yanayopendekezwa na Muswada huu bila kwanza wananchi wa Tanzania na Wabunge wenyewe kupata muda wa kutosha wa kuyatafakari masuala haya yote kwa uzito unaoyastahili na kuyafanyia maamuzi ya busara.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hizi zote, naomba kutoa hoja chini ya Kanuni ya 86(3)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge hili Tukufu kwamba Bunge hili likatae Muswada huu Kusomwa Mara ya Pili kwa sababu Serikali imeleta Muswada Mpya na wenye mabadiliko makubwa na ya msingi bila kufuata masharti ya Kanuni ya 84(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge; na pia kwa sababu Serikali haijatekeleza maagizo ya Bunge hili Tukufu kuhusu kutoa muda zaidi kwa Kamati na wananchi kuufikiria, kuuelewa na kuutolea maoni Muswada huu kinyume na matakwa ya Ibara ya 18(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano juu ya uhuru wa wananchi kutoa maoni yao; Ibara ya 21(1) na (2) juu ya haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi na haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayowahusu wananchi, maisha yao au yanayolihusu Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae. Mheshimiwa Tundu Lissu anawasilisha hotuba ya maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6), hiyo haitoi hoja ni maoni yake na alipomalizia sawa sawa hayo ni maoni ya Kambi ya Upinzani. Tunaendelea na majadiliano.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. FELIX MKOSAMALI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Hoja ya Kuahirisha Mjadala.

**SPIKA:** Mimi siruhusu kwa sababu tunapoteza muda. Karibu Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

*(Hapa baadhi ya Wabunge wa Upinzani wakiongozwa na Wabunge wa CHADEMA walitoka Ukumbini ikiwa ni ishara ya kupinga Muswada wa Mabadiliko ya Katiba)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitoe shukrani ya pekee kwako wewe mwenyewe binafsi Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuwatendea haki Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wote tuliopo hapa ndani tumechaguliwa na wananchi wanataka Katiba Mpya. Mbunge ambaye hana nidhamu ndivyo anavyofanya tunaomba mtoke tuendelee na mjadala. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Watanzania wanakusikia.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Tokeni tuendelee na mjadala.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Hakuna utaratibu endelea Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.
**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee dakika zangu zimepungua.

**SPIKA:** Naomba uendelee Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Na sisi tunatoka.

**WABUNGE FULANI:** Toka.

*(Hapa baadhi ya Wabunge wa Upinzani waliendelea kutoka ukumbini)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru sana Mheshimiwa Spika, lakini naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuamua kukubali na kuona umuhimu wa kutoa fursa hii kubwa ya kwamba Serikali yake imekubali tuunde Katiba Mpya. Suala la Katiba Mpya limekuwa ni suala la Watanzania. Serikali yetu imekuwa ni Serikali sikivu ikaamua kukubali. Rais alizungumza, akikubali bila ya shinikizo.

Lakini naomba nizungumze neno moja ambalo liwe katika historia ya nchi yetu. Ni nchi nyingi sana zimeingia katika machafuko wakati wa kutengeneza Katiba Mpya. Iwapo Serikali haitakuwa makini ikiwaachia watu wanaopotosha wananchi wetu, ikawachanganya wananchi wa Tanzania wataifanya nchi yetu ambayo ni nchi iliyotulia iwe nchi ya vurugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Majimbo yote yamewakilishwa humu ndani mimi ninazungumza kama Anne Kilango Malecela, lakini siyo mimi anayezungumza hapa ni wananchi wa Same Mashariki. Hapa ndani kuna wananchi wa Igunga, hapa ndani kuna wananchi wa Nzega wanawawakilishi. Kwa hiyo, huu Muswada tunaozungumza leo sisi tukiwa kama wawakilishi ni wananchi wa Tanzania tunawafanyia kazi na tutawatendea haki naomba Watanzania watulie wajue hatukuja hapa kuwaumiza, tumekuja hapa kuwatendea haki. Naanza kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kujadili Sehemu ya Tatu inayohusu madaraka ya Rais. Rais baada ya kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar atateua Wajumbe wa Tume. Nipo kwenye Muswada, imeandikwa Sehemu ya Tano, Rais baada ya kukubaliana na Rais wa Zanzibar kwa ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar kwa kupitia tangazo la Serikali ataunda Bunge la Katiba. Hakuna nchi isiyo na kiongozi wa nchi. *(Makofi)*

Naomba nirudi kwenye Katiba, ukienda kwenye Katiba Sehemu ya Kwanza Sura ya Pili, Ibara ya 33 kutakuwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano. Hii Ibara ya 3 inayosema kutakuwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano hapa ni Kiongozi wa Taifa. Inachukuliwa kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Kiongozi wa Taifa. Sasa mamlaka makubwa ya kuteua Tume, mamlaka makubwa ya kuteua Bunge la Katiba nani mwingine atoe kama siyo Kiongozi wa Taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi haliniingii akilini watu wanapoona kwamba Rais amerundikiwa madaraka nani ateue Tume? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mia moja haikuanza mia moja imeanzia kwenye moja. Tunakwenda kutengeneza Katiba Mpya lazima tuanze kwa mchakato wa kuunda Tume, ni lazima tuanze hivyo. Mimi nimewashangaa ambao wametoka nje ndio waliokuwa wanataka Katiba Mpya hao, ndio waliokuwa wanawaambia Watanzania tunahitaji Katiba Mpya. Katiba Mpya hiyo tutaipataje, lazima twende hatua kwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini iwapo tutaendekeza watu ambao wana *passport* mbili, kukitokea machafuko wanakimbilia India, wanakimbilia Uingereza nchi itaingia kwenye machafuko. Nawasihi Watanzania wajue tupo hapa sisi Wabunge wametuchagua kwa kura kwa ajili ya kuwatendea haki, kuwatendea haki wanawake, kuwatendea haki wanaume na vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba nirudi tena kwenye uteuzi wa Tume yenyewe ukurasa wa 30 sehemu ya tatu, Ibara ya 4 bila ya kujali Ibara ya 3 mtu hatakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume endapo mtu huyo ni; hapa mahali pia kuna utata wanapapiga vita, mtu huyo ni Mbunge tumeelewa, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi sawa, Diwani sawa, ni mtumishi katika vyombo vya usalama sawa, ni mtu aliyewahi kuhukumiwa, si raia wa Tanzania. Hawa ni viongozi wa kisiasa pia hawaruhusiwi. Haina maana kwamba mwanasiasa haijafunga kwamba mwanasiasa, maana yake viongozi wa kisiasa ni viongozi wa kisiasa. Lakini kuna wanasiasa, nitoe mfano, mfano wa Jaji Warioba siyo kiongozi wa kisiasa lakini ni mwanasiasa. Sijui naeleweka, kwa hiyo, isifike mahali tukawataka wenzenu wakamfunga mno Rais wakafike mahali wakamwachia, sijui watamwachia nani wakienda kwa maaskofu, maaskofu wengi ni viongozi wa kisiasa. Mchungaji Mtikila ana Chama na ni kiongozi wa kisiasa, Mchungaji Msigwa, sasa Rais aende akachukue wapi? Mimi nirudi niwasihi Watanzania kwa unyenyekevu, watuamini wawakilishi wao, nchi ina wananchi milioni 45 hii watu milioni 45 hawawezi kuingia hapa lakini wapo hapa ndani. Same Mashariki ipo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo na kusema kwamba naunga mkono hoja na tuendelee mbele, tusiwasikilize watu ambao wanataka kuleta vurugu katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya pili katika jambo hili muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu. Mimi kama Mbunge niliyekuja Bungeni hapa kupitia Chama ha Wananchi *(CUF)* leo ni miongoni mwa siku ambayo nimefurahi sana. Nimefurahi kwa sababu Chama changu kimekuwa mstari wa mbele kuiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi na viongozi wa nchi hii kuandaa mazingira ya kupatikana Katiba Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tulifanya hivyo kwa madhumni ya kuwasaidia Watanzania. Chinua Achebe anasema; *"he who pave the way to the great pave the way to his own greatness."* Tulifanya vile ili heshima hii ikipatikana inarudi kwetu wenyewe. Huo ulikuwa utangulizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana umefanya juhudi kubwa kwa niaba ya Bunge hili kuhakikisha kuwa Muswada unapata nafasi inayostahili ya kujadiliwa. Lazima tukubali ulipokuja mara ya kwanza ulikuwa na matatizo mengi lakini kwa juhudi zao umelisaidia Bunge letu kuweza kuwa katika mazingira mazuri ya kujadili Muswada. *(Makofi)*

Pili, napenda nishukuru hatua zote zilizochukuliwa na upande wa pili wa Muungano kwa ushirikiano na viongozi wa Zanzibar katika kufanikisha Muswada huu. Ushirikiano umekuwa zaidi ya asilimia 95 hiyo ni *+A.* Sasa unapofikia hapo binadamu lazima uone kuwa wenzako wamefanya juhudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nastuka kidogo kwa sababu kwa mujibu wa Katiba ambayo tunayo, Rais ana madaraka makubwa, angeweza tu kama alivyofanya katika Tume nyingine za Nyalali, Jaji Kisanga na nyingine angeteua Tume tu hivi nani angeweza kuipinga? Yeye ni *President,* yeye ni *Head of State* na ni Amiri Jeshi Mkuu. Inashangaza sana kuwa tumesoma ni watalaam sana lakini tumeshindwa kuviona vitu vidogo tu. Kama madhumuni ya elimu ni haya ya kuwapotosha watu basi ni vizuri kuwa wengine hatukusoma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi namshukuru Rais, juhudi hii aliyoifanya mimi naamini ana nia nzuri, nawaomba Wabunge wenzangu na Watanzania wenzangu tumsaidie kwa hili kwa sababu mwisho wa siku historia ya Katiba Mpya itaandikwa Wabunge walio ndani ya Bunge hili pamoja na Rais wa Tanzania wa Awamu ya Nne. Ni makosa makubwa sana kulauma kitu kwa sababu kakifanya fulani. Mtu kama kafanya kitu kizuri kubali kuwa kafanya kitu kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesikia hapa lugha nzuri sana za asilimia 70 ya mjadala uliotoka upande wa Kambi ya Upinzani ambao mimi sikubaliani nao kwa hoja hizi umeigusa Zanzibar hee! Zanzibar inaonekana ni tatizo kubwa. Kwa nini? Sijui. Watu hawa kama walipata ridhaa ya kuongoza dola ya nchi hii nawahakikishieni Watanzania wenzangu Muungano ungekuwa haupo hivi sasa. Lazima tuwasifu sana Watanzania waliofanya maamuzi haya kwa sababu watu wanahukumiwa kwa wanayoyasema na wanayofanya. Maneno haya ya leo yanathibitisha kuwa watu kumbe hawawataki Wazanzibar na hawautaki Muungano. *(Makofi)*

Napenda niseme wazi hapa Wazanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano na kimsingi na sisi wadau muhimu wa Jamhuri ya Muungano iliyopo. Hatukuja sisi hapa mwaka 1964 kuja kuomba sahani ya chakula, tulileta mchele kilo mbili na wenzetu wakatoa kilo mbili tukapika kilo nne cha chakula hiki wanachokula watu leo. Loo! Hii ni kasumba ya ajabu sana kudhani kuwa labda haya yanayofanywa katika kuleta maelewano mazuri eti ni haki isiyokuwa ya msingi wanayopewa Wazanzibar kwa nini? Rais wa Zanzibar anapokuja hapa nyuma yake kuna Jeshi, maana yake kuwa yule ni Mkuu wa Nchi ya kule. Rais wa Muungano nyuma yake kuna Jeshi na tumekubaliana mapema kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano kwa sababu ya Muungano yenyewe. Kwa hiyo, hii haijaondoa hata kidogo haki ya kuwa Wazanzibar wamekuja kinyemela nyemela kwa kuombaomba hapa kwa vile lazima tupewe haki yetu na tunawashukuru waliotupa wametupa kwa sababu kuamini kuwa ni sehemu ya nchi hii. Sasa wenzetu hawa wanaokuja na kudhani kuwa labda sisi tunafanyiwa *favour,* mimi nafikiri wananchi lazima wawaelewe, sasa naomba niondoke hapo.

Napenda niwaambie Watanzania kuwa fursa hii ambayo wataipata ni ya kwao wasimkubali mtu yeyote ambaye atajaribu kuwatisha kwa namna moja au nyingine, wasichangie maoni yao katika Katiba yao. Kwa sura hii inaonekana watu watatisha, Watanzania wenzangu nawaomba msikubali kutishwa. Nafasi hii ni yetu, tuseme tuliyonayo kwa faida ya nchi yetu na Katiba tunayoitaka, mwisho wa siku yale matatizo ambayo tulikuwa tunayazungumza pembeni tutakaa juu ya jukwaa na kuyasema hili hatulitaki, hili tunalitaka. Hivi tulikuwa tunataka zaidi ya hicho? Maana yake mimi nastuka unaposema unazuia leo Muswada hapa usijadiliwe, maana yake ni kuwa unazuia hiyo dhana ya Katiba Mpya isipatikane kwa sababu kama haukujadiliwa Muswada hautakuja hivi hii ndio maana yake ndio tumetumwa na Watanzania kwa ajili ya hiyo? Watanzania wenzetu wametuleta hapa kwa ajili ya kusema kuwa hatutaki Katiba Mpya? *This is contrary to the will* maana yake *will,* ni kuwa tupate Katiba Mpya. Halafu tunasema mjadala tunauzuia, ni kichekesho kikubwa ndio niliposema kuwa elimu maana yake ni hii basi mimi nafikiri ni bora kuwa sisi wengine kuwa hatukuipata sana. *(Makofi)*

Mimi nafikiri nina wasiwasi kuwa huu ni woga kuwa watu watapata kusema na watakayoyasema ni baadhi ya mambo tunayoyafanya sisi viongozi tusiowatakia mema, ndiyo wasiwasi wangu na mtu muoga ndiyo inavyokuwa. Shakespear alisema: *"cowards die many times*

*before their death."* Yeye alisema: *"all of the wonders that I yet have had is to hear that men fear death, seeing that death is a necessary end that will come when it will come."* Katiba itakuja tu, Katiba mpya itakuja tu. Kama watu wanaiogopa, basi waiogope, lakini mwisho wa siku Watanzania watajadili na Katiba mpya itakuja. *(Makofi)*

Nakuombeni sana Watanzania wenzangu, natumia fursa hii niliyoipata kusema nanyi, msikubali kwa namna yoyote kuja mtu akakutisheni mkaacha fursa ya kutoa maoni yenu kwa ajili ya kutaka Katiba yenu, hii ni heshima tuliyoipata, huko nyuma haijawahi kufanyika, toka limeundwa Taifa hili hii ni heshima kubwa tuliyoipata, tuitumieni vizuri, tulilonalo kuwa ni tatizo hata kama hayo madaraka ya Rais tunayaona makubwa si tuseme basi ni makubwa? Si tuseme ni makubwa, kwani ukisema tu kuwa yapo kama hukusema yapunguzwe ndiyo yatapungua? Hayapungui hayo. Tuwape fursa wananchi waseme madaraka yaliyopo ni makubwa bwana, Rais yeye inakuwa mengi, sasa bora apunguziwe afanye hili na hili na hili na ndivyo ilivyo kwa wenzetu si ajabu, hapa kwetu Rais anachagua Mkuu wa Majeshi, anachagua Mkuu wa Polisi, anachagua Majaji kwa wenzetu Marais hao hao wanachagua watu wao lakini wanawapeleka katika Mabunge kwa ajili ya kuwa-*rectified* halafu wanakuwa wakomavu, wanakuwa wakubwa si jambo kubwa, lakini ni suala la kulizungumza na kukubaliana.

Sasa huu mwenendo ambao tunaufanya, mimi nafikiri hatuwasaidii wananchi, hatuwasaidii wananchi hata kidogo, tunawapotosha wananchi kwa kuamini kuwa kila linalofanyika lina dhamiri mbaya, hili halina dhamiri mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoendelea maana yake tunawazuia Watanzania wasipate fursa ya kujadili au ya kutoa maoni yao kuhusu Katiba, naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba upo, umeshashirikiana vizuri na wenzako katika kufanya hatua tunayotoka nayo, naomba kaa *with confidence*. *(Makofi)*

Peleka maoni watakayoyasema Wabunge kwa wateuzi, wateue Tume ipite kwa wananchi, ichukue maoni. Anayesema Wazanzibari wamependelewa waache wapendelewe, anayesema Serikali ya Tanganyika muache aseme ije, anayesema ije Serikali ya mwanzo, muache aseme ije, anayetaka Serikali ya wapi muache aseme ije, mwisho wa siku Bunge la Katiba litaamua ni Katiba ya namna gani, mambo gani yakubaliwe, mambo gani yakataliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa. *(Makofi)*

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu, mimi nimeamua nitabaki hapa hapa, mchango nilionao nitautolea hapa hapa na naomba wananchi wa Vunjo na Watanzania wanielewe, sina mahali pengine pa kusemea ni hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulivyokuwa unatukaribisha ulisema watu wawe wakweli na mimi naomba Watanzania katika hili kama unataka umoja wa Kitaifa, unataka nchi hii isisambaratike, tusianzishe vita vya wenyewe kwa wenyewe. Tunapojadili huu Muswada wa Katiba, tuongozwe na ukweli na tuwe wakweli kwenye dhamira zetu na mbele ya Mwenyezi Mungu ndipo tutafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna aya moja nzuri sana ya *Quran* inazungumzia juu ya mnafiki na Mwenyezi Mungu anasema mnafiki hataonja pepo, ataenda kwenye *Jehanam* na Mwenyezi Mungu akasema kwenye ile aya mnafiki ana sura tatu; akisema anasema uongo na mimi mtu mzima kwa umri huu siwezi kuja hapa Bungeni kuja kusema uongo, kuja kudanganya Watanzania, la kwanza. Akiahidi hatekelezi, mimi watu wa Vunjo na Tanzania nimewaahidi kwamba nitashirikiana na Serikali kutafuta Katiba mpya ya nchi hii. Na sura ya tatu ya mnafiki ni kwamba akiaminiwa, haaminiki. *(Kicheko/Makofi)*

Leo nilikuwa naona ni siku ya kihistoria kwa sababu kama kuna zawadi ambayo nchi hii itatoa kwa Tanzania, zawadi ya Krismasi ni hii Katiba mpya na kama kuna zawadi ambayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaweza kutuachia baada ya miaka yake kumi, ni hii Katiba mpya sioni kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nimejaribu kuangalia kinachotufanya tugombane ni nini, tufarakane ni nini, tuelewane vibaya ni nini? Nimeangalia hii Tume inayotaka kuundwa, Tume ya Rais, sio mara ya kwanza nchi hii kuundwa Tume ya Rais na watu hawakufanya maandamano. Mwaka 1991 tulikuwa na Tume ya Rais ya Nyalali iliyokwenda kuratibu maoni ya watu kuhusu mabadiliko ya Katiba na mfumo wa vyama vingi au chama kimoja, lakini tofauti na hii ni kwamba walivyoratibu yale maoni yalifika kwa Rais, Rais alichagua yale ambayo anaona yanamfaa, yale mengine akaacha na hatukuwa na uwezo wowote sisi kama wananchi kwenda kuhoji, mbona hili la Serikali limesemwa mbona Rais umelikataa? Hatukuwa na uwezo, tofauti na huku tunakokwenda sasa hata mwaka 1998 Tume ya Jaji Kisanga, kutafuta maoni ya watu kuhusu maswali mbalimbali, Tume iliratibu mambo mengi, mengi yakakubaliwa na mengine yakakataliwa, lakini wananchi hatukuwa na uwezo wa kwenda hoji kwa nini haya yamekataliwa, lakini sasa hivi kwanza naomba niseme Bunge hili sisi, huu mchakato unaanzia hapa kwa hiyo sisi ndiyo tulichaguliwa mwaka jana na wananchi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu anaweza kuliambia Bunge hili tusifanye hii kazi, mtu wa pili ambaye amechaguliwa mwaka jana ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tutamuenguaje? Na wa tatu ni wananchi wenyewe ambao madaraka yote yanatoka kwao.

Kwa hiyo, Watanzania waelewe hakuna kitakachopitishwa, Bunge hili litashirikishwa katika hatua hii ya leo, baadaye itaundwa hiyo Tume ya kwenda kukusanya maoni ya wananchi na wananchi mna uhuru wa kusema mnataka Rais wa namna gani, hakuna mtu atakayewapiga wala atakayewatisha, ikitoka pale inakwenda kwenye, aha! Maoni yanakwenda kwa Rais, Rais hatuwezi kumkataa hata kule Libya mlisikia wale watu baada ya vita vile ametokea mtu pale anajiita mkuu wa nchi anasema ataunda Katiba mpya na yeye ametoka porini huko huko *from nowhere* licha ya huyu Rais wa hapa amechaguliwa na watu kuna Katiba inayomuweka kwenye madaraka, hatukutoka msituni kuja kuikamata nchi hii jamani, tunakwenda wapi? Tutamtoaje?

Sasa Tume inachukua yale maoni, ikitoka pale inampelekea Rais, Rais anaunda Bunge la Katiba na lile Bunge la Katiba limefafanuliwa, Wabunge wote, Wawakilishi kutoka Zanzibar na Wajumbe 116, kutokana na asasi mbalimbali kutokana na watu wa dini.

Sasa mimi ninachotaka kusema hapa leo hatutungi Katiba, hatutungi Katiba leo, Watanzania waelewe, tusije tukagombana bure, tukatafutana uchawi. Leo tunatafuta mchakato namna gani hicho chombo kitapatikana na wananchi mtakuwa na haki na uwezo wa kushiriki kwenye hiyo Tume kusema mnachokitaka, mkisema hata Rais hatumtaki Rais wa namna hii mnataka Rais malkia au mfalme hakuna atakaye wahoji, hakuna atakaye wadai, ni maoni yenu. Maoni yale yatakwenda kwa Rais, Rais atakuja nayo kwenye Bunge la Katiba, Bunge la Katiba tupo sisi wote hapa na Zanzibar watakuwa hapa, Bunge la Katiba watu wote ni mashuhuri, asasi za dini kama Maaskofu, Mapadri, Wachungaji, muumini katika nchi hii watakuja hapa ndani. Wasomi wa Vyuo Vikuu hata Wanaharakati wataletwa huku ndani, tutajadili wote kwa pamoja hapa ni kitu gani tunakitaka, mimi siamini vichwa vyetu viko hapa kuchakachua, watamchakachua nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mwisho wake wananchi nataka kusema mambo ya kutoka Bunge la Katiba mnapelekewa, wananchi mtapelekewa mliko huko mjiandae, msiporidhika na jinsi mambo yalivyoendeshwa na Bunge hili na Tume ya Katiba hata Bunge la Katiba lilivyoendesha mambo, hata Rais kama mnafikiri kuna kitu ameweka huko ndani bado mna uwezo wa mwisho wa kukataa hii Katiba, mkapiga kura ya ndiyo au hapana, kama mnaona mambo yenu hayako kule ndani, hata tukisema kwamba tuanze maandamano sasa, maandamano dhidi ya nini? Mbona hatujasema? Mbona wananchi mna sauti? Hili jambo nataka niwaambie wananchi, msifikiri mwaka 1991 kwenye ile Katiba wananchi mliulizwa juu ya mfumo wa chama kimoja au vyama vingi, asilimia 80 mkasema mnataka chama kimoja CCM, ndiyo kama sio Mwalimu Nyerere aliyesema kwa dunia hii tuliko haifai kuendelea kuwa na chama kimoja tutafika wakati watu watataka vyama vingi, kama sio Nyerere hata hivi vyama vingi vya sasa hivi wananchi wengi walikwisha vikataa mwaka 1991. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hata nyie wananchi lazima muwe macho sana kuhusu huu mchakato, msishikwe masikio, hii nchi tunaweza tukaivuruga sisi wenyewe kwa wenyewe. Kwa hiyo, mimi

ninachotaka kusema tuwe watulivu, tutumie akili zetu, hili jambo tulifanye kwa stahaa, hii nchi ni yetu, wote ni wazalendo, hakuna mtu mwenye nia mbaya hapa na hii nafasi ni *golden opportunity*, tumepewa hii nafasi tuitumie vizuri, tusipoitumia tukazira hatutafika huko tunakotaka twende. Kwa hiyo, mimi nimebaki hapa kama mzee mwenye heshima yangu, kuja kuhasi vizazi hivi. Mimi nimekuwa Mbunge kwa miaka 20, nimekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, najua mambo mengi, Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana, Naibu Waziri Mkuu, nchi hii naijua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua matatizo tuliyopata huko tulikopitia mpaka leo tumefika hapa, leo tumempata Rais ambaye anatuelekeza tupite hapa, sasa *as we go* kama kuna mahali pa kusahihisha, tutasahihisha, kama kuna mahali pa kusema tutasema, lakini mimi sioni kama tunavyotaka kufanya itakuwa ni sahihi, Rais ana nia njema, Serikali ina nia njema. Kama wangekuwa hawana nia njema wangefanya kama ile Katiba ya mwaka 1991, mbona walifanya mapendekezo hatma yake Rais akachagua fulani wengine akaacha, mwaka 1998 mbona mambo yalikuwa hivyo? Leo hakuna hapa katikakatika, tunaanza hapa, leo ndiyo tunazungumza hicho kitu tukiunde, hiyo Tume ya kutafuta maoni, tukimaliza maoni yakipatikana, wananchi semeni yatakwenda kwa Rais, Rais ataunda Bunge la Katiba, yatakuja hapa watu zaidi ya 500 mimi sioni uwezekano wa watu 500 wakae hapa watengeneze kitu kisichowafaa wananchi na mwisho wake wananchi, sauti ya mwisho itakuwa yenu. Mkiona yale mambo mliyokuwa mnataka hayako kwenye Katiba si mnapiga kura ya hapana? Mkiona yale mliyokuwa mnataka yako si mnasema ndiyo? Katiba itakuwa imepita, kwa hiyo, Katiba itakuwa imeshirikisha wananchi. Wananchi mtakuwa mmeshiriki kikamilifu, Rais kama kiongozi wa nchi, Rais utamtoaje? Haya madaraka yatatoka porini, yatatoka wapi? Si mpaka kuwe na mtu ambaye tayari yupo kwa mujibu wa Katiba ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninachotaka kusema nakupongeza sana kwa jinsi unavyojaribu. Naomba watu wawe watulivu, naomba watu tusaidiane mpaka Katiba ya nchi hii tunayoitaka ipatikane. Mimi nafikiri kukiwa na *good will* hii Katiba itapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa muda uliopo hauwezi kumtosha mtu mmoja kusema, napenda kusema kwamba kesho tutakapoingia wachangiaji wa mwanzoni watakuwa Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Dokta Faustine Ndugulile, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed atafuatiwa na Mheshimiwa Ismail Rage na atafuatiwa na Mheshimiwa Moses Machali. Kwa hiyo, hawa ndiyo watakaokuwa mwanzoni kesho. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyomaliza, sisi sasa hivi tumemaliza mwaka mzima wa kutumia Kanuni zetu, tumetumia vibaya sana kauli ya mwongozo, mtu akiwa na tatizo lake yeye anasema mwongozo, mwongozo, sio utaratibu wa Kikanuni, utaratibu wa Kikanuni kifungu cha 68(7) kinaeleza kwamba unapotaka mwongozo, kunakuwa na kitu kilichotokea.

Sasa mimi nimekuja hapa kuwasilisha Muswada watu wanaanza mwongozo, sasa unamwongoza kitu gani wakati tunatakiwa kuanza kusoma mtoa hoja, Mwenyekiti na hakuna mwongozo, taarifa unampa taarifa nani kwa sababu yule anatoa taarifa yake anasoma sasa taarifa ya kutoka wapi? Tumekuwa na muda mwingi wa kutumia vibaya Kanuni zetu na hivyo kupoteza muda. Kwa hiyo, kuanzia sasa tutafuata Kanuni kama zilivyo na hakuna mtu yeyote mwenye msahama kwa hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kama tulivyosema wananchi wa Tanzania lazima waambiwe, tunachokifanya hiki ndicho kinachotuwezesha sisi, mwananchi mmoja mmoja kule aweze kuzungumza kuhusu hatma ya Katiba, ndiyo hiki tunachokifanya. Kama walivyosema wengine Rais angeweza kuunda Tume yake tu, mbona alishafanya hivyo nani alimbishia? Lakini kwa uungwana wake akatuletea sisi Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, mimi naona mnataka kukataa kutunga sheria na huo ndiyo wajibu wenu wa Kikatiba kutunga sheria, ndiyo kazi yetu moja kubwa kutunga sheria sio kukimbia

sheria na nyie wasomi wazuri sana *amendment* leteni hapa liwe furushi zima tutakaa hapa mpaka tutaziingiza kama mnataka mabadiliko. *(Makofi)*

Kitu kingine ambacho ukisema wewe sio lazima uliyosema wewe yakubalike, mtajadili, ndiyo maana ya mjadala. Unaweza kuwa umesema unayofikiria wewe, lakini wenzio wakafikiria vinginevyo ni lazima ufike mahali ukubali ya wenzio pia, sasa kama itakuwa unayosema wewe ndiyo yenyewe na wenzako wanayosema siyo yenyewe basi sio sahihi pia.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mimi nasema wananchi watuamini, Bunge hili wameliunda wao wenyewe, tupo hapa kutunga sheria ili baada ya sheria hii ikiweza kupita vizuri, wananchi wapate fursa ya kuongea na Tume kile wanachotaka kiwe ndani ya Katiba yetu, kama madaraka ya Rais yapunguzwe huko kwa sasa hivi hamuwezi kupunguza kwa sababu Katiba ipo. Lakini kwa mchakato huu wanaweza kujadili hayo, kama tunataka Serikali iwe namna gani wakati huo ndiyo watapata nafasi. Lakini haiwezi kupatikana nafasi mpaka tumepitisha Muswada huu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi kama kiongozi wenu mkiniambia niliwakataza kwenda mikoani, niliwakataza pia kwenda Ulaya. Haikuwa mikoani tu niliwakataza pia Kamati kwenda Ulaya, maana yake nilisema kuanzisha hii kitu mtaenda Ulaya kutafuta nini na sisi tunatengeneza wenyewe? Kwa hiyo, sikuwakataza tu mikoani na Ulaya niliwakataza. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge sina matangazo yoyote muhimu, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.38 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne,*
*Tarehe 15 Novemba, 2011 saa tatu asubuhi)*